

**JINSIA NA KABILA KATIKA MUUNDO WA MAZUNGUMZO NA  
UTENDAJI WA UNYENYEKEVU: MFANO WA BIASHARA YA MIRAA  
MIONGONI MWA WASOMALI NA WAMERU  
MTAANI EASTLEIGH, NAIROBI-KENYA**

**KING'ANG'I JUDITH GAKII**

**Tasnifu iliyowasilishwa katika Shule ya Masomo ya Shahada za juu kwa minajili  
ya kutimiza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili,  
Chuo Kikuu Cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**NOVEMBA, 2018**

## **UNGAMO NA IDHINI**

### **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na hajatolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote kile.

Sahihi: ..... Tarehe .....

**King'ang'i, Judith Gakii**

**AM12/33515/14**

### **IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi..... Tarehe:.....

**Prof. Furaha Chai, PhD**

Idara ya Luga, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Pwani

Sahihi ..... Tarehe :.....

**Dkt. Fred Simiyu Wanjala, PhD**

Idara ya Kiswahili na Luga Zingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Kibabii

## **HAKIMILIKI**

©2018, King'ang'i Judith Gakii

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga, kutafsiri, kunakili au kuhifadhi tasnifu hii kwa jina au mfumo wowote ule pasi na idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa Bw. Isaac King'ang'i M'ithai na Bi. Margaret Kalayu King'ang'i. Kwa mapenzi yenu kwangu yasiyo na kipimo, Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Kwanza shukrani zangu za dhati ninamtolea Mwenyezi Mungu kwa neema, rehema na fadhilli zake ambazo ni mpya kila siku, na kwa ulinzi wake tangu nilipoanza masomo yangu hadi kukamilika kwake. Wakati mwingine mambo yaliniwia magumu lakini kwa kumtegemea, niliweza kufua dafu.

Pili, shukrani kutoka moyoni mwangu ziwaendee wasimamizi wangu wapendwa Prof. Furaha Chai na Dkt. Fred Simiyu Wanjala kwa kunipa wosia, kunishika mkono na kunielekeza kwa subira katika safari nzima ya elimu yangu ya uzamili. Kazi hii ilianza kama wazo tu ambalo halikuwa hata limenakiliwa karatasini. Wazo langu lilikomaa na kuwa pendekezo la utafiti ambalo sasa hivi ni tasnifu! Ninawashukuru sana kwa kuisoma kazi yangu na kunirekebisha kwa umakini na uvumilivu mwingi. Ninawavulia kofia wasimamizi wangu hawa! Chuo kilinipa wasimamizi lakini niliibuka na marafiki mwishoni. Mola awazidishie siku zenu hapa duniani ili muwafaidi wengi katika safari zao za kiakademia.

Tatu, ninawashukuru wahadhiri katika Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu chuoni Egerton kwa mchango wao wenye busara na hekima. Dkt. M. Gwachi, Dkt. A. H. Taib, Dkt. Kipsabit, Dkt. Khaemba, Dkt. Bartoo, Dkt. Gacheiya, Bw. Amollo, Bw. Muindi, Bw. Kwambai, Bw. Kahiro na Bw. Mayoyo ambao wote kwa njia moja au nyingine walinihimiza na kunitia moyo wa kuendelea na masomo yangu pasi na kukata tamaa. Bw. Amollo, kwa kuisoma kazi yangu na kunisaidia katika utafsiri wa baadhi ya dhana, nakushukuru sana. Prof. Kitetu kwa mchango, maelekezo na wosia ulionipa ili kuiboresha kazi yangu-Mungu akubariki. Bila mwongozo wenu nisingeweza kusafiri salama katika bahari hii ya elimu.

Nne, shukrani zangu za dhati namtolea mwalimu wangu Dkt. Gacheiya aliyenifundisha tangu nikiwa mwaka wa kwanza hadi wa nne chuoni Egerton na kunitia mshawasha wa kuendeleza masomo yangu nikiwa ningali kijana. Baada ya kukamilisha shahada katika sanaa, nilimwendea mwalimu kwa mawaihda kuhusu kuendeleza masomo yangu katika Kiswahili. Hapo ndipo alinichukua na kunielekeza hadi ofisini kwa Dkt. Chai (ambaye sasa ni Prof. Chai) na kunieleza kuwa “iwapo unataka kuzamia Kiswahili huyu ndiye ‘daktari’ sasa.” Na kweli hapo sasa alikuwa ameniweka katika mikono salama ambayo ingenibeba hadi mwisho.

Tano, natoa shukrani zangu kwa wanafunzi wenzangu, Bw. E. Sifuma, Bi.W. Maryanne, Bw. H. Omanga, Bw. R. Musembi na Melvine O. kwa kuwa karibu nami. Mijadala na mihadhara yetu ilitupa nguvu za kulisukuma gurudumu la usomi pamoja hadi mwisho.

Sita, shukrani zangu za dhati pia ziwaendee wote walionifaidi na kutoa mchango katika kufanikisha utafiti wangu nyanjani. Sitawasahau Bw. J. Kimathi, Bw. Ayale, Bw. Sabir, Bw. Ali Kuss, P. Mugaa, ‘Mende’, Bw. Gitonga, Sammy, ‘Omosh’, Brian, Simon, Stanley, David, Murangiri, Zakayo, Thuranira, ‘Mende’, Mama Zainabu, Mama Farhiya, Mama Fiona, Gakii, Karani, Pius, Patrick, Mwere, Muthuri, Baariu, Thangicia na ‘Kidero’ kwa kujitolea kunisaidia kila nilipohitaji msaada wenu. Mngelisusia kunipa data ambayo niliihitaji, basi tasnifu hii isingelikuwepo. Kwa hilo ninawaombea Mungu ili na wana wenu pia waweze kusaidiwa kama mlivyonisaidia mimi.

Saba, ningependa kuwashukuru wazazi wangu wapendwa Bw. Isaac King’ang’i M’ithai na Bi. Margaret Kalayu King’ang’i kwa mapenzi, malezi na mawaidha tangu utotoni. Ninawashukuru kwa kunitia mshawasha kusoma kwa bidii tangu nilipokuwa mdogo huku mkinihimiza kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Pia, kwa kuyafadhili masomo yangu hadi kiwango hiki. Babangu mzazi kwa mapenzi yako ya Kiswahili tangu ukiwa kijana ulikuwa umenunua riwaya na tamthilia nyingi ulizokuwa ukisoma. Bila shaka ninaiendeleza ndoto yako. Mungu awabariki wazazi na awalinde siku zote za maisha yenu. Pia, ninawashukuru ndugu zangu Martin, David, Joachim, Robert, Juster, Brian na Roy kwa kunihimiza na kunitia moyo hata pale nilipohisi kutokuwa na nguvu za kuendelea. Mlikuwepo nami kwa hali na mali mkinijuza kuwa mliona fahari sana kwangu, jambo ambalo lilinichochea kufanya bidii hata zaidi.

Mwisho, sitosahau kumshukuru binamu yangu L. Kibwi kwa kunikaribisha nyumbani kwake Kilifi, kwa wiki mbili ambazo nilienda kumwona mhadhiri wangu kwa ajili ya tasnifu. Ulinitunza na kunipa malazi mema kwa kipindi kizima hicho. Kwa hilo sitousahau uhisani wako. Na iwapo kuna wengine ambao nimesahau kuwataja lakini walinisaidia kwa njia moja au nyingine kufanikisha kazi hii, nyote kwa pamoja ninawashukuru asante na kuwatachia baraka zake Mungu.

## IKISIRI

Mazungumzo huwawezesha wanadamu kuitisha hisia zao na kumudu mazingira yao. Umahiri wa kimawasaliano ni chombo muhimu katika kuwasaidia wanadamu kufanikisha maingiliano yao. Kujihusisha na kudumisha mahusiano yasiyo na migogoro huhusisha ushirikiano na utendaji wa unyenyekevu baina ya waingilianaji. Katika utafiti huu, mtatini alichunguza muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi wa miraa pamoja na mikakati ya unyenyekevu waliyoitumia. Malengo matatu mahususi yaliyouongoza utafiti huu yalikuwa ni: ubainishaji muundo wa mazungumzo baina ya wanunuzi na wauzaji wa miraa, kisha kutathmini namna vigezo vya jinsia na kabile la washiriki vilivyoathiri muundo wa mazungumzo na kutathmini namna vigezo vya jinsia na kabile vilivyoathiri utendaji wa unyenyekevu katika maingiliano hayo ya biashara ya miraa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Uchanganuzi wa Uzungumzaji na Nadharia ya Unyenyekevu. Mbinu za ukusanyaji data zilikuwa utazamaji katika hali asilia madukani pa kuuzia miraa, kurekodi mazungumzo na mijadala katika vikundi viini. Data ilinukuliwa kwa Kiswahili na kufanyiwa uchanganuzi wa yaliyomo. Uteuzi wa sampuli ulifanywa kimakusudi na kwa kuzingatia Mtazamo wa Maingiliano ya Kijamii ili kubainisha washiriki 48. Data ilikusanya katika barabara za 8, 10 na 12 mtaani Eastleigh katika jimbo la Nairobi, nchini Kenya. Data iliwasilishwa katika nukuu na majedwali ili kuonyesha umaratokezi wa mikakati mbalimbali ya unyenyekevu. Utafiti huu ulibainisha kuwa washiriki wa biashara ya miraa walizingatia misamiati mbalimbali ya kufungua, kujirekebisha, kukata kalima na kufunga maongezi yao. Muundo wa mazungumzo wa mzungumzaji-mmoja-kwawakati-mmoja haukuzingatiwa na kukawa na aina mbili za ubadilishaji zamu: sahili na changamano. Mikakati mbalimbali ya unyenyekevu ilitumiwa na wanunuzi na wauzaji kila walipozungumza. Kwa mfano: kuamkua kwa kuita mnunuzi *boss, baba, brother, wariah, Engineer* ili wasionekane kushinikiza wanunuzi wao, kubadili msimbo, matusi, kushukuru na kuagana. Utafiti huu umetoa maarifa na mchango katika masomo ya uchanganuzi wa usemi kwa kuzingatia mahusiano ya kijinsia, kikabila, kimamlaka na unyenyekevu. Matokeo haya yatawafaidi wachanganuzi wa muundo wa mazungumzo ikizingatiwa ufunguzi, ubadilishaji zamu na ufungaji katika miktadha anuwai ya kijamii. Waundaji sera nchini Kenya watafaidi pia, kwani lugha ikitumiwa vyema itawaunganisha wanajamii wa jamii mbalimbali.

## ABSTRACT

Conversations surround our daily encounters and its the successful conversations that we undertake, that help us conquer the challenges that we face. However, for an interaction to be successful, co-operation while doing turns is needed amongst the participants. Interactants involved in a conversational exchange should try to maintain each other's self-esteem by employing politeness strategies since social interactions are geared towards co-operation. Therefore, this study aimed at analysing the conversation structure among the selected negotiations between miraa buyers and sellers. The research was based on three objectives: firstly, identifying the conversation structure of miraa negotiations by traders, secondly, establishing the implication of gender and ethnicity of the traders on the conversation structure during the negotiations and thirdly, determining the implication of gender and ethnicity on the politeness strategies employed by traders during the conversational exchange. The study was guided by two theories: Conversation Analysis theory and Politeness Theory. Direct Observations, audio-recording and Focused Group Discussions were conducted to obtain data. Purposive sampling and Milroy's Social Network Approach were used to identify the 48 participants from 8<sup>th</sup>, 10<sup>th</sup> and 12<sup>th</sup> streets in Eastleigh, Nairobi Kenya. The spoken samples of the conversations between the miraa buyers and sellers were later on transcribed in Kiswahili. Content analysis was done on the transcripts and tables showing the politeness strategies employed were derived. The study revealed that the traders used simple and complex turntaking structures, the repair process was either self or other-initiated. The females' communication style shifted to the 'rudeness standards' set by the male while meekness was associated with buyers with ill-intentions. They employed different politeness strategies such as use of honorifics like *boss*, *brother*, *Engineer* to minimize imposition. Codeswitching was another politeness strategy that intercultural participants made use of especially whenever the seller or buyer was tempted to utter mean statements to the other conversant. The findings from this study will be important to scholars in applied linguistics and interactional sociolinguistics. The findings will have wider implications on important concepts like; gender, intercultural relations, power relations, and politeness in intercultural communication. This study will also contribute positively to policies towards national integration whereby language can be used as a tool to break or maintain the existing social ties in intercultural interactions.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINI .....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI .....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU .....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKRANI.....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vii</b>
<b>ABSTRACT.....</b>	<b>ii</b>
<b>DIBAJI YA MAJEDWALI.....</b>	<b>v</b>
<b>DIBAJI YA VIPUPISHO VYA MANENO .....</b>	<b>vi</b>
<b>SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti .....	5
1.4 Maswali ya Utafiti.....	6
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .....	7
1.7 Ufafanuzi wa Istilahi .....	9
<b>SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA .</b>	<b>10</b>
2.1 Utangulizi .....	10
2.2 Mapitio ya Maandishi.....	10
2.2.1 Miraa kama Bidhaa ya Biashara .....	10
2.2.2 Maingiliano ya Kibiashara.....	12
2.2.3 Maingiliano ya Kikabila .....	13
2.2.4 Uchanganuzi Usemi .....	14
2.2.5 Muundo wa Mazungumzo .....	15
2.2.6 Unyenyekevu katika Mazungumzo .....	22
2.2.7 Unyenyekevu wa lugha kutegemea jinsia .....	23
2.3 Misingi ya Nadharia .....	25
2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Uzungumzaji .....	25
2.3.2 Nadharia ya Unyenyekevu.....	27
2.4 Hitimisho .....	30
<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>31</b>
3.1 Utangulizi .....	31

3.2 Muundo wa Utafiti .....	31
3.3 Mahali pa Utafiti .....	32
3.4 Umma Lengwa .....	32
3.5 Uteuzi wa Sampuli .....	32
3.6 Ukusanyaji wa Data .....	33
3.6.1 Utazamaji.....	33
3.6.2 Kunasa na Kurekodi Sauti .....	34
3.6.3 Mijadala katika Vikundi Viini.....	34
3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data.....	35
3.8 Maadili ya Utafiti .....	35
<b>SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA .....</b>	<b>37</b>
4.1 Utangulizi .....	37
4.2 Muundo wa Mazungumzo.....	37
4.2.1 Vifunguzi vya Mawasiliano.....	38
4.2.2 Ubudilishanaji Zamu.....	42
4.2.3 Ukataji Kalima.....	45
4.2.4 Urekebishaji.....	48
4.2.5 Ufungaji wa Mazungumzo .....	50
4.3 Athari ya Kabilia na Jinsia kwa Muundo wa Mazungumzo mionganoni mwa Wauzaji na Wanunuza .....	53
4.3.1 Jinsia na Muundo.....	54
4.3.2 Ukabila na Muundo .....	62
4.4 Mikakati ya Unyenyekevu .....	70
4.4.1 Maamkuzi .....	72
4.4.2 Maneno ya Heshima ya Kutaja.....	73
4.4.3 Mzaha au Utani na Vichekesho .....	75
4.4.4 Maombi.....	77
4.4.5 Ubudilishaji Msimbo .....	79
4.4.6 Makaribisho .....	81
4.4.7 Matumizi ya Misamiati ya Biashara .....	82
4.4.8 Upungungakaji wa Unyenyekevu.....	85
4.4.9 Matusi .....	86
4.4.10 Kushukuru na Maagano.....	90

4.4.11 Hitimisho .....	92
<b>SURA YA TANO:MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>93</b>
5.1 Utangulizi .....	93
5.2 Muhtasari wa Matokeo.....	93
5.3 Hitimisho .....	95
5.4.1 Muundo wa Mazungumzo katika Biashara ya Miraa .....	95
5.3.2 Mikakati ya Unyenyekevu katika Biashara ya Miraa.....	97
5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti.....	98
<b>MAREJELEO.....</b>	<b>99</b>
<b>KIAMBATISHO 1: FOMU YA IDHINI.....</b>	<b>105</b>
<b>KIAMBATISHO 2: RATIBA YA UCHUNGUZI.....</b>	<b>106</b>
<b>KIAMBATISHO 3: MWONGOZO WA MAHOJIANO KATIKA VIKUNDI KIINI.....</b>	<b>107</b>
<b>KIAMBATISHO 4: KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI.....</b>	<b>108</b>
<b>KIAMBATISHO 5: RAMANI YA JIMBO LA NAIROBI, ENEO LA EASTLEIGH.....</b>	<b>109</b>
<b>KIAMBATISHO 6: ALAMA ZA UNUKUZI .....</b>	<b>110</b>
<b>KIAMBATISHO 7: TUNUKUZI YA DETA .....</b>	<b>111</b>

## **DIBAJI YA MAJEDWALI**

Jedwali 1: Kielelezo cha Mikakati ya Unyenyekevu kutoka Brown na Levinson (1987:60).....	29
Jedwali 2: Uteuzi wa Sampuli.....	33
Jedwali 3: Vidokezo na Utokeaji wa Muundo wa Mazungumzo .....	37
Jedwali 4: Mikakati ya Unyenyekevu katika Mazungumzo kutokana na deta .....	71
Jedwali 5: Msambao wa misamiati iliyotumika katika maamkuzi .....	72

## **DIBAJI YA VIPUPISHO VYA MANENO**

- |        |                                 |
|--------|---------------------------------|
| K.H.J. | - Keshatajwa                    |
| K.M.   | - Kwa mfano                     |
| K.V.   | - Kama vile                     |
| UK     | - Ukurasa                       |
| S.S.J  | - Sacks, Schegloff na Jefferson |

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Lugha ndiyo huwasaidia wanadamu kujenga mahusiano ya muda au ya kudumu. Wanaohusiana kilugha huweza kubadilishana fikra au kusisitiza misimamo wanayoishikilia kuhusu maswala ya kimaisha. Mahusiano yote hufanyika kwa lengo la kukabili na kutatua matatizo ya kijamii ya kila siku. Baada ya kutoa kauli hii basi ni muhimu kusisitiza kuwa lugha humwezesha mwanadamu kujitambulisha kama mwanajamii-lugha mojawapo wa lugha zipatikanazo ulimwenguni. Jamii zote kwa hivyo zaweza kujitambulisha kwa kuzingatia lugha yao ya kwanza au lugha moja maalumu waliyofundisha kama lugha ya pili.

Maingiliano yoyote ya kijamii huzingatia lugha (Yule, 1996). Lugha ni chombo muhimu kinachowawezesha watu kuendeleza shughuli zao za kila siku. Lugha ni kama mafuta yawekwayo kwenye gari ili liweze kwenda. Goodwin na Heritage (1990), wanankuliwa na Liddicoat (2007) wakieleza kuwa wazungumzaji hupata kukubalika au kukataliwa kama watu binafsi au kama mmoja wa jamii mahususi wanayotoka kila wanaposhiriki katika mazungumzo.

Binadamu anaposhiriki katika mazungumzo huwa anawakilisha utamaduni, jinsia, kabilia, makazi, tabaka, umri, dini na hata nafsi zao wenye. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mwanajamii hujifunza mengi kutokana na jamii yake ya kuzaliwa. Anapokua basi huwa anafikiria na kutenda kulingana na imani za jamii yake. Imani hizi hujidhihirisha katika mazungumzo yake. Watu kutoka tamaduni na jinsia tofauti huwa na njia tofauti za kujieleza na kujionyesha katika mazungumzo (Coates, 2004).

Kila wakati watu wanapotangamana kimazungumzo, huwa wana nia kuu ya kukubalika au kupendeka na wenzao (Goffman, 1967). Nia hiyo ya kutaka kupendeka au kukubalika na wanakikundi, ndiyo huwashinikiza watumiaji lugha kutumia lugha kwa njia mbali mbali.

Kwa mfano, iwapo mzungumzaji anazijali hisia za mwenzake, hawezи akatumia maneno ‘machafu’ au akamatiza kauli mwenzake anapokuwa akizungumza. Baadhi ya sheria hizi hazijaandikwa mahali popote bali watumiaji lugha huzizingatia au kuzikiuka kutegemea uhusiano au muktadha ambapo wao hujipata kimazungumzo. Labov (1972) alisema kuwa ni umilisi wa lugha ambao huwasukuma wazungumzaji

kushirikiana katika mazungumzo. Ushirikiano katika mazungumzo waweza kuhusisha mchakato mzima wa kubadilishana zamu au kufanya urekebishaji wakati mtu anapomkatiza kauli mwenzake. Pia ushirikiano wa kimazungumzo unaweza ukashirikisha matumizi na utendaji wa unyenyekevu baina ya wazungumzaji.

Unyenyekevu ni njia mojawapo ambayo watu huzingatia ili pawe na ushirikiano katika maingiliano. Unyenyekevu husaidia kuleta mshikamano na kujali maslahi ya mwonekano wa washiriki wengine katika mazungumzo. Unyenyekevu hudhihirishwa kila mara lugha inapotumika. Hata hivyo, ambacho huchukuliwa kuwa kitendo chenye kusheheni au kudhihirisha unyenyekevu ni tofauti sana kutegemea muktadha, washiriki na asili ya kijamii ya wazungumzaji (Hoffman, 1991). Unyenyekevu katika mawasiliano huwasaidia washiriki kuwasiliana kwa njia sambamba. Hata hivyo, wakati mwingine dhihirisho la upole linapokosa kutambuliwa na watumiaji lugha, panatokea hali ya kutolewana na mawasiliano huenda yakavunjika. Hali kama hii inapotokea, washiriki wa uzungumzaji huhitajika kurekebisha mwelekeo wao wa kutumia lugha ili mawasiliano yaendelee na pia waonekane wanajali hisia za wenzao. Huku kujali hisia za watu wanaohusika katika mazungumzo, ndilo huwa dhihirisho la upole katika matumizi ya lugha (Leech, 1983).

Katika Afrika Mashariki, Kiswahili ni lugha ya matumizi mapana na lugha inayowaunganisha watu ya eneo hilo. Maingiliano mengi ya kijamii katika nchi za Afrika Mashariki huendelezwa kwa lugha ya Kiswahili. Japo watu katika eneo hilo hutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli nyingi ikiwemo biashara, Watanzania ni maarufu katika kutumia lugha iliyojaa misamiati yenye unyenyekevu wakilinganishwa na watu kutoka mataifa mengine kama vile Kenya (Ulimwengu, 2015).

Nchini Kenya, kuna makabila mengi yanayoingiliana na kushirikiana kilugha katika shughuli za kijamii. Wardhaugh (2006), anafafanua kuwa watumiaji lugha huzingatia vipengele kadha wanapotumia lugha; namna za kuzungumza, uchaguzi wa maneno na eneo la kijiografia, jamii, kabilia, ujinsia na sheria zinazoongoza mawasiliano kulingana na mahitaji ya kijamii. Kwa hivyo nchini Kenya, washiriki wa maingiliano, huingia katika maingiliano hayo wakiwa wametawaliwa na tamaduni za jamii yao na ujinsia wao. Kwa mfano, Njambi (2015), aligundua kuwa wauzaji na wanunuzi wa nguo kutoka jamii ya Gikuyu huzingatia vipengele vya jinsia na muktadha kwa namna wanavyozingatia unyenyekevu. Hivi kwamba iwapo ni katika mazingira ya dukani,

muuzaji huzungumza kwa kuzingatia unyenyekevu mwangi kwa kuwa anatangamana na mteja mahususi. Katika uuzaaji wa mahali palipo wazi, wauzaji hutumia misamiati ya jumla kuwaita wateja kwa sababu wanataka kuvutia wateja wa jinsia zote.

Maingiliano hutokea baina ya watu kutoka jamii na jinsia tofauti nchini Kenya. Maingiliano hayo huzuka kwa nia ya watu kufanikisha shughuli zao za kila siku. Biashara ni mojawapo ya maingiliano ambayo hutokea katika jamii. Kuna biashara za aina nyingi ambazo wanajamii hujihusisha nazo kama njia ya kujipatia mtaji na kutafuta riziki mifano ni kama vile uuzaaji nguo, nafaka, vileo na hata vitabu.

Kisayansi miraa huitwa *Catha edulis*. Beckerleg (2009) anaeleza kuwa miraa kwa kawaida, inajulikana kama *khat*, *qat*, *chat*, *gomba*, *veve*, *mairungi* au *miraa*. Ni mti ambao hukua katika sehemu kubwa ya Afrika na Asia ya Magharibi kati ya nyanda 5000 na 6500 juu ya usawa wa bahari. Kilimo na matumizi ya miraa ilitambuliwa tangu karne za zamani, na imekita mizizi katika tamaduni za Yemen, Ethiopia na sehemu ya Igembe na Embu nchini Kenya. Miraa hutafunwa na kutoa maji machungu na ni kileo cha wastani kitoacho kemikali ziitwazo *Cathinone* na *Cathine*. Kutoka sehemu hizi, huwa inatafunwa na pia kuuzwa ili kuinua uchumi wa wakulima. Miraa hutolewa shambani na kupakiwa katika vifurushi vya kilo kumi (*kibunda*), kilo moja (*gitundu*) na *shurba* (kifurushi kimoja kati ya vijifurushi sita vinavyounda kilo moja) (Carrier, 2007).

Vifurushi hasa vya kilo kumi kumi, ndivyo hupakiwa kwenye magari vikiwa vimefungwa katika magunia na kusafirishwa mijini tofauti nchini Kenya. Miraa husafirishwa kwa magari ambayo huendeshwa kwa mwendo wa kasi sana kwani ni bidhaa inayoharibika upesi, kwa hivyo kuchelewa kwake kwaweza kuleta hasara kubwa kwa wakulima na wafanya biashara. Miraa huwafikia watu wengi katika miji tofauti, takwimu zikionyesha kuwa kadri kilo 12,000 za miraa husambazwa nchini kila siku, na kilo 4,320,000 kila mwaka. Kiwango kikubwa cha miraa hufikishwa Nairobi na hasa sehemu ya Eastleigh, Pumwani-kituo kikuu cha usambazaji. Katika eneo hili pia, miraa ambayo husafirishwa hadi nchi nyingine hupakiwa katika maboxi maalumu na hufikishwa katika kituo cha ndege cha Wilson na nchi kama vile Somali, Ethiopia na magharibi hufikiwa. Kadri kilo 112,613 hupitia kituoni cha ndege cha Wilson kuelekea Somali kila mwezi na 1,351,356 kila mwaka. Hii ni ishara kuwa soko kubwa la miraa ni Wasomali (GOK, June 1996).

Ijapokuwa soko la Uropa na nchi nyingine za Ulaya uuzaaji wa miraa umesitishwa kwa sasa kutokana na madai kuwa miraa inatoa kemikali zenyenye kulevyo WHO (2014), ukulima na biashara yake itaendelea hapa nchini kutokana na faida za kiuchumi wanayopata watu wa jamii mbili (Wameru na Wasomali). Yeyote atajapo au kusikia miraa ikitajwa, ambacho humjia akilini huwa ni Wameru kama wauzaji na Wasomali kama watafunaji wakuu na ndio hulusika katika mauzo ya nje ya miraa (Beckerleg & Sheekh, 2005). Goldsmith (1988), anaeleza kuwa wanaume ndio hulusika sana katika biashara ya miraa na wengi ni wa kutoka eneo la Meru. Hata kama kuna wale wa kutoka jamii nyingine amba pia wameingia katika biashara hii ili kuondoa ukiritimba wa jamii hizo mbili kuhusika, watu kutoka jamii hizi mbili wamesalia kuwa wahusika wakuu.

Wameru na Wasomali kwa hivyo huingiliana katika biashara ya miraa tangu karne ya 18. Watu kutoka jamii hizi mbili wanajulikana kwa kutaka maendeleo na ufanisi kazini. Vilevile, jamii hizi mbili huwa na mitazamo tofauti kuhusu unyenyekevu na namna ya kufanya unyenyekevu. Miriti (2012), aligundua kuwa ijapokuwa watu kutoka jamii hizi mbili (Wasomali amba ni wasemiti na Wameru amba ni Wabantu) wanatoka katika jamii zenyenye ukoo tofauti kabisa, wao wanaunganishwa na lugha ya biashara katika soko la Muringene na Maua. Sababu kuu ni kwamba watu wanaotoka katika jamii na tamaduni zinazotofautiana, huelewa na kukubali sheria za kimaingiliano kabla ya kujihusisha na mazungumzo (Gumperz, 1982). Katika soko hilo la miraa, lugha inayoonekana kuwa mwiko katika jamii, inakubalika na inatumiwa na wauzaji na wanunuzi.

Katika mazingira ya biashara, huwepo pande mbili za watu wanaoingiliana; wanunuzi na wauzaji wa bidhaa. Fauka ya watu kuingia katika maingiliano ya kibashara wakiwa na tofauti za kikabilan na kitamaduni, watu hao huingia katika maingiliano wakiwa na sifa za ujinsia. Mukuni (2016), akizingatia utafiti wa Miriti (2012), alichunguza maingiliano ya wauzaji na wanunuzi wa miraa katika jimbo la Embu. Aligundua kuwa Wambeere wa jinsia zote hutumia maneno yaliyo mwiko katika soko la miraa. Maneno-mwiko hutumika ili kuwashawishi wanunuzi kununua na pia kujitambulisha na soko la miraa. Hata hivyo, King'ei (2010) anaeleza kuwa madhumuni makuu ya mawasiliano katika biashara ni kuwavutia wateja na kuwafanya kuamini kuwa bidhaa ama huduma wanazouziwa ni za kiwango cha juu na ni thamani bora kwa pesa zao. Kwa kuzingatia hoja ya King'ei (k.h.j), mtarufi alibaini kuwa kulikuwa pengo la kimaarifa kuhusu

muundo wa mazungumzo uliotumiwa washiriki wa biashara wa miraa, na namna walivyozingatia mikakati mbalimbali ya unyenyekevu. Utafiti huu kwa hivyo, ulitekelezwa ili kubainisha namna washiriki teule kutoka jamii za Somali na Ameru walibadilishana zamu na kutenda unyenyekevu kwani vipimo vyta unyenyekevu siyo lugha mwiko tu bali kuna mikakati mingineyo ambayo watu hutumia kudhihirisha unyenyekevu katika maingiliano. Mshawasha wa kufanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha katika biashara ya miraa, yalitokana na ukweli kuwa vijiti vyta miraa hupoteza ladha yake pindi tu vitolewapo kwenye miti ya miraa, Carrier (2005). Watumizi wake hupendelea sana kuinunua miraa hiyo ikiwa miororo iwezekanavyo kabla ya kupoteza madini yanayowaletea waraibu ladha. Hamu hiyo ya kuipata na kununua miraa ikiwa miororo ndiyo husababisha matumizi ya lugha iliyo ya kipekee. Tatizo hilo ndilo lilimsukuma mtafiti kuchunguza lugha katika muktadha husika.

### **1.2 Suala la Utafiti**

Mazungumzo huathiriwa na vipengele vyta kijamii kama vile; cheo, uhusiano baina ya wazungumzaji, umri, kiwango cha elimu, tabaka, muktadha, jinsia, kabilia na vinginevyo. Vipengele hivi huchukuliwa kuwa na athari nafsia au athari yenye mwingiliano kwa jinsi vinavyoleta mabadiliko katika muundo wa mazungumzo na utendaji wa unyenyekevu. Harakati zinazohusu mmea wa miraa huwa zinatendwa kwa wepesi sana. Muda huwa ni kiungo muhimu sana kiasi cha kila dakika na sekunde kugharamiwa. Wepesi huo huathiri hata matumizi ya lugha inayozingira biashara hiyo. Ijapokuwa tafiti za awali zilionyesha kuwa lugha ya soko la miraa ilisheni maneno mwiko, utafiti huo haukupambanua namna vipengele vyta kabilia na jinsia viliyoathiri mfanyiko mzima wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuvi wa bidhaa ya miraa.

Basi, utafiti huu ulichunguza namna kabilia na ujinsia wa washiriki ulivyoathiri muundo ambaa mazungumzo yalichukua na pia utendaji wa unyenyekevu baina ya washiriki wa jamii ya Somali na Ameru.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi ukabila na jinsia ya mshiriki inavyoathiri muundo wa mazungumzo na utendaji wa unyenyekevu baina ya washiriki wa biashara ya miraa kutoka jamii ya Ameru na Somali. Kwa hivyo, madhumuni mahususi yalikuwa ni:

- i. Kubainisha muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa.
- ii. Kutathmini namna muundo wa mazungumzo unavyoathiriwa na khabila na jinsia ya washiriki wa biashara ya miraa.
- iii. Kupambanua mikakati ya unyenyekevu inayotumiwa na washiriki wa khabila na jinsia tafitiwa katika mazungumzo ya biashara ya miraa.

#### **1.4 Maswali ya Utafiti**

- i. Ni muundo gani wa mazungumzo ulizingatiwa na wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa?
- ii. Je, khabila na jinsia ya washiriki inaathiri vipi muundo wa mazungumzo katika biashara ya miraa?
- iii. Ni mikakati ipi ya unyenyekevu inayozingatiwa na washiriki wa khabila na jinsia tafitiwa ili kufanikisha mazungumzo?

#### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Mtafiti anakusudia kubainisha muundo wa mazungumzo, na utendaji wa unyenyekevu katika muktadha wa biashara nchini Kenya, mahususi katika biashara ya miraa. Washiriki wakuu wa biashara ya miraa ni watu kutoka jamii ya Meru ambaao ni wakuzaji na waliobobe a katika biashara hiyo na watu wa asili ya Somali wanaoishi nchini Kenya. Watu kutoka jamii hizi mbili huwa wenye bidii na wanadaiwa kuwa wenye ‘hasira na ukali’ wakilinganishwa na watu wa jamii zingine nchini Kenya Kobia na Miriti (2014). Madai haya, huzua hisia kuwa washiriki hutumia lugha kwa njia ya ‘kipekee’ katika maingiliano yao. Mukuni na wengine (2016), wanaeleza kuwa soko la miraa huwa limesheheni lugha ilio na maneno makali na japo aligundua kuwa maneno hayo yana uamilifu wake katika soko kama vile ‘kujitambulisha na lugha ya soko la miraa’. Maarifa machache yanapatikana kuhusu jamii hizi mbili wanavyoingiliana katika biashara na namna wao huzingatia muundo wa mazungumzo na kutenda unyenyekevu ili kufanikisha maingiliano yao ya kibiashara.

Mwishoni mwa utafiti huu, mtafiti amefanikiwa kuonyesha matokeo yaliyodhihirisha muundo wa mazungumzo, na utendaji wa unyenyekevu baina ya watu wa jamii mbili na jinsia tofauti katika maingiliano ya kibiashara. Maarifa ya utafiti huu, yatatumika katika uwanja wa isimu jamii hasa uchanganuzi wa usemi kwani mazungumzo yalichanganuliwa kuonyesha hatua mbali mbali za mazungumzo na jinsi wazungumzaji

wanavyojadiliana hadi kuafiki mapatano. Vilevile, matokeo yatafaa wasomi katika uwanja wa pragmatiki kwani lugha iliyochunguzwa ilitumika katika muktadha mahususi wa kijamii kwa madhumuni ya kubainisha baadhi ya maswala ya kijinsia, kimamlaka na kikabila. Zaidi ya hayo, maarifa haya yatakuwa na umuhimu kwa waundaji sera kama vile watatuzi wa migogoro na wanaoeneza sera za utangamano na ushikamano wa kijamii hasa mikakati ya unyenyekevu ambayo huzingatiwa na washiriki wa biashara ya miraa (kama jamii wakilishi za makabila yanayotangamana nchini) ilipopambanuliwa. Mwisho, matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango kwa taasisi za kibashara hasa katika kuwafafanulia vitendo na maneno ambayo huvutia na kuimarisha uteja katika mazingira ya biashara ili kufaulisha biashara za watu binafsi na nchi nzima kuimarika kiuchumi kwa ujumla.

### **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ni wa kiisimu, na ulijikita kwenye uwanja wa pragmatiki. Mtafiti alijihuisha na matini zungumzwa na wala siyo matini andikwa. Mtafiti alichunguza muundo wa ubadilishanaji zamu katika mazungumzo ya kibashara na wala siyo miktadha mingine ya mazungumzo. Watafiti wa hapo awali kuhusu mada hii kama vile Miriti (2012) wamechunguza lugha katika soko la miraa katika eneo la Muringene na Maua, na Miriti akagundua kuwa ni lugha iliyosheheni maneno mwiko japo inakubaliwa hivyo katika mazingira hayo. Mukuni (2015) kwa kuendeleza utafiti awali wa Miriti (k.h.j.) anaeleza kuwa msamiati mwiko unaozingatiwa katika biashara ya miraa una uamilifu katika soko lile kwani ni njia mojawapo ya mshiriki kujitambulisha na kukubalika na vilevile kupata kupunguziwa bei ya bidhaa. Kwa hivyo, utafiti huu haukuchunguza lugha mwiko bali mtafiti alionyesha mikakati ya unyenyekevu na ubadilishanaji zamu baina ya wauzaji na wanunuzi. Nadharia ya unyenyekevu ya Brown na Levinson (1987) ni pana mno na mtafiti alijikita katika mikakati michache tu ili kubainisha vitendo vya unyenyekevu. Waliochunguzwa ni wauzaji na wanunuzi wa kike na kiume wa umri tofauti kutoka jamii ya Wameru na Wasomali wapatikanao katika eneo la Eastleigh. Kujikita katika utafiti wa maongezi yafanywayo na watu wa jamii hizi mbili, ni kwa sababu wao ndio washiriki wakuu wa biashara ya miraa nchini Kenya. Pia, uchunguzi wa mazungumzo baina ya watu wa makabila mawili tu, ulimfaa mtafiti kwani nchini Kenya kuna kadri makabila 43 na ingekuwa vigumu kuchunguza wanunuzi na wauzaji kutoka kila kabila. Baada ya kufanya utafiti, changamoto moja ilijitokeza kwamba, ilikuwa ni vigumu kudhibiti idadi ya watu waliofika dukani ili

kununua miraa. Hivyo tatizo la kimaadili la kutowaaarifu wanunuzi wote kuwa uzungumzi wao ulikuwa unarekodiwa lilichipuza. Hata hivyo, mtafiti alihakikisha kuwa mnunuzi aliyefika kununua akiwa wa kwanza pamoja na muuzaji wake walifarifiwa na kukubali kabla ya mazungumzo yao kunaswa.

## **1.7 Ufafanuzi wa Istilahi**

**Jinsia** ni hali ya kuwa mwanamke au mwanamme. Katika utafiti huu, istilahi hii ilitumiwa kurejelea mwanamke au mwanamume kutoka jamii za Wameru na Wasomali.

**Tahayuri** ni neno ambalo mtafiti ametafsiri kutokana na ‘Face’. Kulingana na utafiti huu, neno hili lilitumika kurejelea hisia au hali ya kawaida ya mtu baada ya kuambiwa jambo.

**Unyenyekevu** ni kukubaliana na wengine ili kupunguza utofautianaji kwa minajili ya kufanikisha maingiliano. Katika utafiti huu, neno hili lilitumika kuonyesha namna msemaji hutumia lugha ili kufaidi mwenzake au kupunguza kutokubaliana.

**Zamu** ni ambapo ‘angalau’ mtu mmoja huzungumza kwa kipindi kimoja.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imegawika katika sehemu mbili kuu; sehemu ya kwanza ni mapitio ya maandishi na sehemu ya pili ni nadharia za utafiti. Mtafiti alitathmini na kuhakiki maandishi mbalimbali ambayo yalihusiana na mada na akaonyesha namna maarifa hayo yalivyoufaidi na kutofautiana na utafiti lengwa. Vilevile, alitoa maelezo ya nadharia, mihimili ya nadharia hizo na jinsi nguzo za nadharia husika zilivyonumika katika utafiti huo.

#### **2.2 Mapitio ya Maandishi**

Katika sehemu hii, mtafiti alipitia maandishi yaliyohusiana na mada ya utafiti kulingana na mpangilio wa madhumuni ya utafiti na yalipewa vichwa kutegemea kilichojadiliwa katika sehemu hiyo.

##### **2.2.1 Miraa kama Bidhaa ya Biashara**

Kisayansi, miraa huitwa *Catha edulis*. Beckerleg (2009) anaeleza kuwa inajulikana kama *khat*, *qat*, *chat* nchini Ethiopia au *miraa*, *gomba*, *veve*, *mairungi* nchini Kenya. Ni mti ambao hukua katika sehemu kubwa ya Afrika na Asia ya Magharibi kati ya nyanda 5000 na 6500 juu ya usawa wa bahari. Kilimo na matumizi ya miraa hutambuliwa karne za zamani, na imekita mizizi katika tamaduni za Yemen, Ethiopia na sehemu ya Igembe na Embu nchini Kenya. Miraa hutafunwa na kutoa maji machungu yaliyo na kemikali *Cathinone* na *Cathine* ambayo ni kileo cha wastani (Schorno & Steinegger, 1978). Kemikali hii ndiyo husemekana kulevyia au kuzua msisimko wa mawazo. Utafiti lengwa ulizingatia lugha iliyotumika katika mazingira ya uuzaji na ununuzi wa bidhaa inayofikiriwa kuwa ‘kileo’ jambo ambalo lilitarajiwa kuzua maswala ya kimaadili baina ya wasomi.

Weir (1985) na Kennedy (1987) wanaeleza kuwa Wayemeni wengi hutumia pesa nyingi kununulia miraa na muda mwangi katika kutafuna miraa. Vilevile nchini Kenya, watu wengi hutafuna miraa kama njia moja ya kupitisha wakati, au ili wapate motisha wa kutekeleza majukumu kwani miraa huwawezesha kuwa macho kwa vipindi virefu vyta wakati. Nchini Kenya, kulingana na Chanler (1893) na Newmann (1982), miraa hupatikana kwa wingi katika sehemu ya mashariki mwa nchi na hasa katika jimbo la Meru- gatuvi dogo la Igembe (maeneo bunge ya Igembe ya kati, Igembe kusini na

Igembe Kaskazini). Goldsmith (1988), anaeleza kuwa watu wanaopatikana katika maeneo bunge hayo ni Watigania na Waigembe amba ni wazungumzaji wa lugha ya Kimeru. Watu hawa ndio huhusika kwa wingi katika uuzaaji wa miraa hapa nchini (Carrier, 2007). Hivyo, wameshiriki katika biashara zinazohusisha mmea wa miraa, huku asilimia 60 ikitegemea mapato yake. Kwa upande wa pili, Wasomali ni maarufu katika ununuzi na utafunaji wa miraa (Beckerleg & Sheekh, 2005). Hawa, wanafafanua kuwa Wasomali amba ni wengi wao ni wakimbizi kutoka Somalia huishi Eastleigh nchini Kenya na hufanya biashara za aina nyingi na zaidi hununua viwango vikubwa vyta miraa na hata kuhusika katika mauzo ya nje ya bidhaa hiyo. Maarifa haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu yalimsaidia mtafiti kufahamu na kujikita katika jamii mojawapo kuu ya wanunuzi wa miraa nchini Kenya. Vilevile, yalimsaidia mtafiti kufahamu eneo ambapo watu wa jamii ya Wasomali walipatikana kwa wingi- Eastleigh jambo ambalo lilimwezesha mtafiti kuwapata washiriki kwa urahisi.

Carrier (k.h.j.) naye anaeleza kuwa miraa hufungwa katika vifurushi vyta uzani wa kilo kumi *kibunda* au kilo moja *gitundu* na vilevile *shurba* ambavyo ni vijifurushi vidogo vidogo vilivyofungwa pamoja ili kuunda kilo moja. Vifurushi hivyo vyta kilo kumi ndivyo hupakiwa kwenye magunia na kusafirishwa kutoka eneo la Nyambene ambapo inakuzwa kwa kiasi kikubwa kupitia gari au ndege hadi sehemu tofauti hapa nchini kama vile Isiolo, Garrisa, Nairobi, Nakuru, na Mombasa. Kupitia mauzo ya nje, Wameru na Wasomali hufaidi kiuchumi ikikisiwa kwamba mauzo ya mmea huu ni dola 2345 za Marekani kila mwaka (CRA, 2013). Miraa huwafikia watu kutoka mataifa mengine kama vile Somali, Amsterdam USA, Canada, Sweden japo nchi nyingine kama UK miraa imepigwa marufuku na kutajwa kuwa dawa za kulevyta (WHO, 2014).

Goldsmith (1994), anawataja Wameru kama washiriki wakuu katika biashara ya miraa nchini Kenya. Jambo ambalo lilimsukuma mtafiti kuchunguza matumizi ya lugha ya watu kutoka jamii hiyo. Bernard (1972) anaipa miraa yenye kipaumbele kuwa ni sauti ya Wameru. Maarifa haya ni muhimu katika utafiti huu kwani yanaeleza jamii mojawapo kuu ya wanaohusika katika biashara ya miraa. Umaarufu wa Wameru katika biashara ya miraa ndio ulimsukuma mtafiti kuchanganua lugha waloyotumia Wameru katika uuzaaji na ununuzi.

## **2.2.2 Maingiliano ya Kibiashara**

Gumperz (1982), anaeleza kuwa wanajamii hutambua na kukubali sheria za maingiliano kila mara wanapoingiliana kilugha. Katika biashara, huwa kuna pande mbili za washiriki-wauzaji na wanunuzi. Kulingana na maarifa ya Gumperz, sharti waingilianaji wote watambue na kukubali sheria za kimaingiliano zilizopo katika muktadha wao wa mawasiliano.

Marriott (1993), aliyeshughulikia biashara baina ya Wajapani na Waustralia anaeleza kuwa mazingira ya kibiashara huwahitaji wauzaji kuwajali wateja wao kwa kudumisha huduma bora. Anaeleza kuwa ufanisi wa biashara hujengwa katika uteja na huduma njema. Vilevile, King'ei (2010), anaeleza kuwa muuzaji anapaswa kuyajali maslahi ya mnunuzi kwa kuwapa huduma bora na kuwauzia bidhaa zilizo za thamana. Mtafiti kwa hivyo alichunguza jinsi washiriki walivyozingatia lugha ili kuimarisha uteja na kuongeza mauzo, ili wateja wao wahisi kuwa huduma yao ilikuwa bora.

Hassan (2000), alifanya utafiti wake kuhusu watu wa jamii-lugha tofauti wanavyoingiliana kimazungumzo. Alibainisha kuwa wazungumzaji walishirikiana katika kufasili na kuelewa maana kwa kuzingatia mbinu kama vile; urudiaji, ufanuzi, kuuliza na kujibowi maswali. Utafiti huu una uhusiano na utafiti lengwa kwani mtafiti alitumia mbinu na vifaa vyta kukusanya deta kama alivyotumia Hassan. Vifaa hivi ni kama vile kurekodi mazungumzo na uchunguzi wa ushiriki.

Kwa upande wake, Miriti (2012), alichunguza maingiliano ya kibiashara ya miraa, baina ya Wasomali na Waigembe katika eneo la Muringene na Maua. Katika utafiti huu mtafiti alilenga kubainisha mikakati ya kimazungumzo ambayo wanajamii hawa waliitumia katika ununuzi na uuzaaji wa bidhaa hiyo. Alibainisha kuwa walizingatia mikakati kama vile, utengaji, ushirikishaji, ukosefu wa urasmi na ukavu wa kimsamiati (ambao mara nyingi ulikuwa ni matusi). Utafiti huu unalingana na utafiti-lengwa kwa namna nyingi kama vile; jamii- tafitiwa ilikuwa moja, mbinu na vifaa vyta kukusanya data vilikaribiana na upekee wa mazungumzo kati ya wauzaji na wanunuzi wa miraa ndio uliwasukuma watafiti wote wawili. Hata hivyo, utafiti-lengwa ulichunguza Wasomali na Wameru wakishiriki moja-kwa-moja kibiashara katika eneo la Eastleigh na wala siyo soko la Muringene au Maua. Pia, utafiti ulilenga kuchunguza namna muundo wa mazungumzo ulivyoendeshwa na washiriki wa biashara ya miraa pamoja na kuchunguza mikakati ya unyenyeketu waliyozingatia katika mazungumzo.

Naye Mukuni (2016), akizingatia matokeo ya utafiti wa Miriti (k.h.j.) alichunguza sababu za kinafsia-jamii zilizowapelekea wanabiashara katika soko la miraa (*muguka*) Kiritiri- Embu kutumia lugha–mwiko. Alibainisha kuwa utumizi wa lugha mwiko ulikuwa na umuhimu maalumu wa kutambulisha wauzaji na wanunuzi wa soko hilo. Washiriki walizingatia lugha mwiko kama kitambulisho cha rejesta ya sokoni mwa miraa. Lugha hiyo ilitumika ili kushawishi wauzaji kuwapunguzia bei ya bidhaa ya miraa. Maarifa yaliyotokana na tafiti hizi yalimsaidia mtafiti katika kubainisha vipashio vya kimuundo huku akichunguza mikakati ya unyenyekevu waliyozingatia wauzaji na wanunuzi. Jambo ambalo utafiti huu ulinuia kuchunguza ni jinsi washiriki wa biashara ya miraa walibadilisha zamu kimazungumzo pamoja na kuzingatia mikakati ya unyenyekevu.

### **2.2.3 Maingiliano ya Kikabila**

Watu kutoka jamii, tamaduni, taifa na lugha mbalimbali huingiliana kila mara ili kufanikisha shughuli zao za kila siku. Jamii kama vile za Kiasia, huwa na imani za ukomunisti-kujali maslahi ya watu wengine wanaotoka katika jamii zao. Jamii za kimagharibi kwa upande wake hushikilia misingi ya kibepari ambapo kila mtu hujali maslahi yake mwenyewe. Mawasiliano yanayohusisha watu kutoka kabilia tofauti husheheni chembechembe za utamaduni wa kila mmoja anayehusiana. Haya huwa ni matokeo ya lugha kwani lugha ni mali ya jamii (Scollon & Scollon, 2001). Kabilia kulingana na Phillips (2007), ni migawanyiko iliyojengwa kutokana na mbari mbalimbali katika jamii na huletwala na mirengo ya kisiasa kwani binadamu wote ni sawa. Utotfauti katika tamaduni, desturi, imani na lugha ndio huzua na kuendeleza tofauti za kikabila katika jamii (Brubaker, 1999).

Lugha ni chombo muhimu katika jamii. Eckert (2003) anaeleza kuwa lugha husaidia wanajamii kuendeleza mahusiano na kudhihirisha mipaka ya utangamano wao. Ni kupitia lugha mtu huwa mwanjamii halisi kwani lugha humwezesha kujihusisha na kujitambua kama mmoja wa kikundi fulani cha watu ulimwenguni. Maarifa haya kuhusu maingiliano ya kikabila yalitumika katika utafiti huu kupima semi za washiriki katika biashara ya miraa. Washiriki kutoka jamii hizi mbili wana mienendo sawa kwa mfano, wana bidii kazini, wana ‘hasira’ nyingi, na hawana subira (Miriti, 2012). Walichunguzwa wakifanya maingiliano katika mazingira asilia ya kibiashara, ili

kudhihirisha maarifa ya kimazungumzo ya unyenyekemu na muundo wa mazungumzo yao.

Hassan (2000) alichunguza namna mazungumzo hufanyika baina watu wa jamii tofauti. Alibainisha kuwa mazungumzo baina yao yalizingatia mikakati mingi ya kusuluuhisha matatizo ya kumuundo kama vile urekebishihi, ukataji-kalima, urudiaji na ufafafanuzi. Alieleza kuwa baadhi ya mikakati hii iliwasaidia wazungumzaji kupata kuelewana na kuafikia lengo la mazungumzo baina yao. Ujumbe huu ulimfaidi mtarifi kwa sababu utafiti wake ulihusisha watu walio wa jamii tofauti na kwa kuwa baadhi ya sifa za muundo wa mazungumzo alizoainisha Hassan (k.h.j.) zingemfaa.

#### **2.2.4 Uchanganuzi Usemi**

Uchanganuzi usemi ni taaluma ambayo imetafitiwa na wasomi wengi. Kwa mfano, Benveniste (1971), alifafanua kuwa uchanganuzi hufanywa kwa semi na matini zilizoandikwa au kuzungumzwa: kila usemi hukisiwa kuwa hutolewa kwa mshiriki ambaye huhusika moja kwa moja katika mbadilishano wa ujumbe. Foucault (1972) kwa upande wake, alitazama semi kama mpangilio wa maneno ya watu ambayo hutolewa katika maingiliano na ambayo huthibitiwa na muktadha maalumu. Mtarifi alizingatia maarifa haya kuwa semi huathiriwa na muktadha kuonyesha kuwa muktadha ambao huzingira biashara ya miraa ni maalumu na unaweza ukatafitiwa kwa kuzingatia maneno ambayo washiriki hutoa.

Crystal (1987), kwa upande wake, alieleza kuwa uchanganuzi usemi hulenga kubainisha muundo au mfanyiko wa mazungumzo ambayo hufanyika katika hali asilia za kijamii. Alichukulia semi kama mfanyiko ulioshikamana na kubadilishana maana baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Semi ambazo hutolewa katika mahusiano ya kijamii hubadilika kulingana na muktadha. Jinsi miktadha ya kijamii ilivyo mingi, ndivyo matumizi ya lugha kutegemea miktadha hiyo ilivyo mingi. Utafiti huu ulijikita katika muktadha wa kibiashara ambapo biashara ya miraa iliteuliwa kimakusudi na mtarifi. Mazungumzo kati ya wanunuzi na wauzaji pamoja na vikundi vya watu wanaozingira biashara hiyo walichunguzwa na kumsaidia mtarifi kuutumia mfano huo kama matini ya uchanganuzi. Hivyo usemi katika utafiti huu ulichukuliwa kama mfanyiko wa kijamii ambao huhusisha lugha.

Schffrin (1994) naye akaeleza kuwa uchanganuzi wa usemi ni usomi wa lugha unaovuka mipaka ya sentensi. Usemi ni matini itokanayo na mazungumzo au maandishi. Wasomi wa lugha hujikita na uchanganuzi wa semi ambazo mara nyingi huwa ni vipande vya lugha vinavyotumika katika miktadha ya kijamii. Semi hizi ni kama vile, uzungumzi baina ya daktari na mganjwa, mahojiano ya kikazi, zamu kama zinavyotukia baina ya wafanya biashara, mahusiano baina ya mzazi na mwanawe au mwalimu na mwanafunzi. Semi zitokanazo na mahusiano ya kijamii zinaweza kuchanganuliwa na kubainisha maarifa chungu nzima kuhusu muundo wa jamii kisiasa, kiimani, kiitikadi au kifalsafa. Haya yote yanawezekana kupitia matumizi ya pragmatiki ambayo hutusaidia kufafanua maongezi ya watu na kubainisha wanayomaanisha kutegemea muktadha (Yule, 1996).

Uchanganuzi wa semi kwa hivyo, husheheni maswala ya kijamii (Gee, 1999). Maarifa haya yalinufaisha utafiti lengwa kwa sababu wanunuzi na wauzaji wa miraa ni watu kutoka jamii tofauti na wote wanapotangamana wanabeba mawazo kutoka jamii zao. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza baadhi ya semi zao kwa kuzingatia vipengee vya ‘kufanya’ unyenyekevu kubainisha namna jinsia na watu wa tamaduni mbili teule walivyozingatia mpishano wa zamu na vipashio vingine vya lugha katika mazungumzo yao.

### **2.2.5 Muundo wa Mazungumzo**

Mazungumzo ndiyo huongoza mahusiano yote yanayozingatia lugha. Hata hivyo, mazungumzo hayo huchukua miundo tofauti tofauti kutegemea taasisi ya kijamii ambapo mazungumzo hayo hutolewa. Schegloff (1972), Schegloff na Sacks (1973) walionyesha miundo ya kijumla ya mazungumzo. Walijishughulisha na mazungumzo ya kawaida ambayo hufanyika kila siku mara tu lugha inapotumiwa kuwasilisha ujumbe. Kwa mfano, walikusanya data yao katika mazungumzo baina ya watu walioshiriki katika mijadala ndani ya mahakama, maongezi baina ya marafiki, maongezi ya kibashara, pamoja na maongezi baina ya daktari na mganjwa. Mazungumzo katika kila mojawapo ya miktadha hiyo ya kawaida walipodondo mifano na kuyachanganua, Schegloff (1972), Schegloff na Sacks (1973) walibainisha kuwa yalichukua muundo tofauti.

Muundo kulingana na Goodwin (1981) na Sacks na wengine (1974) ulihusu mchakato wa ubadilishanaji zamu baina ya washiriki wa mazungumzo. Schegloff (1968);

Schegloff na Sacks (k.h.j.) walisema kuwa muundo ulipaswa kuwa hali ambayo washiriki wa mazungumzo hujirekebisha na kurekebisha semi za wengine na taabu ambazo hutokea katika mchakato mzima wa urekebishaji, kusikia na kuelewa ujumbe maalumu.

Kwa maoni yao, Drew na Heritage (1992); Heritage (1997), mazungumzo yanapaswa kuangaliwa kama yanavyotokea katika taasisi mbalimbali za kijamii kwani washiriki katika taasisi zile wanasheheni uelewa wa sheria ambazo zinaongoza taasisi hizo. Kwa hivyo, matumizi ya lugha sharti yaathiriwe na sheria hizo. Katika utafiti huu, mtafiti alichanganua muundo wa mawasiliano baina ya washiriki wa biashara. Katika muundo ye ye alichanganua ufunguzi, ubadilishanaji zamu, urekebishaji, na ufungaji wa mazungumzo.

Yieke (2002) alifanya utafiti wake kuhusu namna jinsia mbalimbali hujieleza katika mazingira rasmi ya kikazi na iwapo palikuwepo na ubaguzi wa kijinsia. Katika utafiti wake, alichunguza namna maswali, ubadilishaji wa zamu, ukataji kalima na upangaji wa mada ulivyotekelawa. Alichunguza namna wanawake na wanaume walivyotangamana na walivyotumia lugha kujieleza katika mikutano pale kazini. Aligundua kuwa jinsia na mamlaka ya wahusika yalikuwa na athari ya moja kwa moja kwa namna wanawake na wanaume walivyotangamana kazini. Hata hivyo, ilitambuliwa jinsia ya iliathiri mahusiano zaidi kuliko mamlaka. Haya yalitokana na mitindo ya wanaume ya kuzungumza ambayo ilitofautiana na mitindo walivoitumia wanawake. Utofauti katika mitindo ya kimazungumzo miiongoni mwa wanawake na wanaume, ndiyo ilichangia katika kuendelea kubaguliwa kwa wanawake kazini. Utafiti huu ulimfaidi mtafiti kwani aliweza kubainisha mamlaka na utofauti wa kimuundo ulivyojitekeza katika mazungumzo yaliyoshirikisha wanawake na wanaume katika biashara ya miraa.

#### **2.2.5.1 Ufunguzi katika Mazungumzo**

Sacks (k.h.j.), anaeleza kuwa mazungumzo ya kawaida katika jamii huchukua muundo maalamu ambapo mmoja kati ya wanaowasiliana huwa na msukumo fulani wa kuanzisha mazungumzo. Anayetangulia basi huchukua nafasi ya mwanzilishi na ndiye huamua ni njia ipi atakayoanzisha yale maingiliano. Hivi kwamba, kila jamii, jinsia, umri na kiwango cha ukaribu wa uhusiano baina ya washiriki huamua namna kwa

mfano salamu hutolewa (Schegloff, 1979). Hivyo, kutegemea uhusiano, umri, jinsia, na utamaduni wake huamua atakavyozingatia lugha kimawasiliano.

### **2.2.5.2 Upishanaji Zamu katika Mazungumzo**

Upishanaji zamu ni mojawapo ya vijenzi nya muundo wa mazungumzo. Maoni ya wataalamu wa uchanganuzi usemi katika mazungumzo ya taasisi za kijamii zilizo rasmi ubadilishaji zamu unaweza ukakisiwa kuwa utachukua muundo maalumu ya taasisi ile. Katika maingiliano ya kawaida hata hivyo, huwa ni vigumu kukisia muundo wa ubadilishanaji zamu ambao maongezi yatachukua kwani hubadilika kulingana na muktadha na washiriki wa mazungumzo (Sacks, Schegloff, & Jefferson, 1974). Washiriki katika uzungumzi hubadilishana nafasi za msikilizaji- mzungumzaji katika tukio la maingiliano. Sacks (k.h.j) wazungumzaji hutakiwa washirikiane katika kujenga na kudumisha muundo sambamba wa mazungumzo. Mzungumzaji mmoja-kwawakati-mmoja ndiye hutakiwa kuzungumza. Mzungumzaji hushikilia nafasi yake na kudhibiti uzungumzi wakati anatoa kauli yake, kabla ya kumpa mwingine usukani huo. Haitakiwi kuwepo na nafasi wazi ambapo hakuna mtu anazungumza wala kukatitiza kalima mzungumzaji mwingine anapokuwa akizungumza. Kila mzungumzaji alipaswa kutambua ishara na videokezo nya sauti na ishara za mzungumzaji ili kutambua kukamilika kwa usemi huo kabla ya kutoa kauli yake. Huu ndio muundo wa mazungumzo walioupendekeza. Kulingana nao, ukataji kalima ni ukiukaji wa haki za mzungumzaji husika. Pia walieleza kuwepo kwa upishanaji zamu usio sambamba ni kufeli kwa mazungumzo baina ya wazungumzaji.

Edelsky (1981), hata hivyo akizingatia utafiti wa Sacks na wenzake (1974), alisema kuwa ingekuwa ni vigumu sana kudumisha muundo huo wa mzungumzaji mmoja-kwawakati-mmoja katika mazungumzo ya ana kwa ana. Kulingana naye, zamu katika mazungumzo ya kawaida baina ya watu wengi haziwezi kudhibitika kwa kuwekewa kanuni. Alitambua aina nyingine ya jukwaa au nafasi za uzungumzaji ambayo ilishirikisha watu wengi kwa wakati mmoja. Kulingana naye, watu wengi wanawenza kuzungumza kwa nafasi moja na wote wakawa wanachagiza na kusaidiana kuwasilisha wazo lililoanzishwa na mmoja wao. Kulingana naye, siyo nafasi ya mzungumzaji mmoja ya kuzungumza iliyo na umuhimu baina ya watangamanaji bali ni kuwepo kwa mawasiliano.

Mawazo ya Edelsky yalitiwa nguvu na utafiti wa baadaye uliofanywa na (Coates, 2013). Alibainisha kuwa washiriki wa kike walio marafiki wanapokuwa wakizungumza katika makundi, huzungumza kwa kukatizana na kuongeza kauli ya wazungumzaji wenza. Kila anayechagiza au kuendeleza kauli ya mwenzake hakuwa akikatiza kauli bali alikuwa akitoa mchango wake na kushiriki katika mchakato mzima wa mazungumzo. Coates alieleza kuwa kukatiza kauli au kuzungumza kwa watu wengi wakati mmoja baina ya wazungumzaji wa kike kulidhihirisha urafiki. Pia, kulifasiriwa kuwa si ukiukaji wa haki za mzungumzaji. Kila kauli iliyotolewa iliongeza ladha na ushirikiano wa wazungumzaji. Alibainisha kuwa wazungumzaji wa kike waliweza kuzungumza na kusikiliza kwa usambamba.

Kwa upande wake Meinhof (1997), washiriki wa kiume walipendelea kuzungumza mmoja baada ya mwingine bila kuchagiziana usemi na bila kukatizana kauli hadi wakamilishe semi zao. Kulingana naye, wanaume walipendelea kuzungumza kila mmoja kwa wakati wake. Lakini iwapo kulikuwa na nia ya kujitambulisha kama marafiki, basi palikuwepo na washiriki wawili au zaidi waliota kauli za kuchagiza usimulizi au habari iliyotolewa na mmoja wao. Matokeo ya tafiti hizi yalimsaidia kuchunguza namna wazungumzaji wa biashara ya miraa walivyopishana zamu zao katika mazaungumzo yaliyoshirikisha jinsia moja au za mseto.

Katika utafiti wake uliohusu maongezi katika simu Schegloff (1986), alibaini kuwa anayepiga simu huwa ndiye wa kwanza kuchukua zamu ya kwanza na pindi inapolia katika ng'ambo ya pili, anayeishika au kuitika huwa ndiye mpokezi. Pia anaeleza kuwa kushikwa kwa simu katika ng'ambo ya pili kunaashiria ukubalifu wa mpokezi kushiriki katika mawasiliano. Ile hali ya kupokea simu ya anayepigwa pia ni ukubalifu wa kuchukua zamu yake ya mazungumzo. Anaeleza kuwa hali ya kupigwa na kuitikwa kwa simu inaonekana kuwa jambo la kawaida japo huwa limebeba maana ya kijamii hasa kutegemea uhusiano wa washiriki. Hivi kwamba kuitika ile simu ni ufunguzi wa maingiliano kati ya anayepiga na anayetika na watakachokisema pia kinadhibitiwa na uhusiano uliopo baina yao.

Kulingana na Sacks (1992), kuna sheria katika mazungumzo ya Kiingereza cha Amerika inayosema kuwa ‘mtu mmoja asiongee zaidi ya mara moja bali awape wengine nafasi ya kuzungumza kabla ya kuongea mara nyingine.’ Katika mazungumzo ya kawaida, washiriki hupishana zamu ili kufanikisha mawasiliano baina yao. Hata

hivyo wakati mwingine hali ya kukatana kalima hutokea pale ambapo wazungumzaji hushindwa kubaini ni nani kati ya washiriki anayepaswa kuzungumza. Hali hii ya ukataji kalima hutatiza mawasiliano kuendelezwa kwa njia iliyo sambamba.

Tannen (1984) anaeleza kuwa ukataji kalima mara nyingine hudhihirisha maswala ya kimamlaka au mshikamano katika mazungumzo. Anazidi kueleza kuwa wazungumzaji wengine huamini kuwa ndio walio na ujumbe kuhusu mada husika na hivyo kuchukua zamu kubwa kuliko wale washiriki wenzao katika uzungumzi. Vilevile, kuzungumza kwa wakati mrefu basi huleta hali ya wenzake kutaka kuzungumza na ndio huzua ukataji kalima. Hali hii ya ukataji kalima ilichunguzwa kwa mintarafu ya kabilia na jinsia katika maingiliano ya kibiashara ili kubainisha iwapo wanaokata kalima wanajaribu kudhihirisha mahusiano yapi kutokana na jinsia ya washiriki wenza.

Mills (2003) anaeleza kuwa kuna tofauti za kimuundo kuhusu mazungumzo ya wanawake na wanaume kwa namna wanavyozingatia upishanaji zamu huku akidhihirisha kuwa wanaume ndio hukatiza kalima kwa wingi wakilinganishwa na wanaume. Kwa kuzingatia maarifa haya, mtafiti alichunguza namna jinsia tofauti katika biashara ya miraa hupishana zamu. Na ni jinsia gani hukata kalima kwa wingi. Iwapo pana ukataji kalima kwa wingi ina maana ipi kuhusu uhusiano wa washiriki.

Coates (2003) alifanya utafiti kuhusu mazungumzo yanayofanyika baina ya vikundi vilivyojumisha wanawake au wanaume pekee na vingine vilivyoshirikisha mseto wa jinsia zote. Alibainisha kuwa wanawake hushirikiana na kuchagiziana kauli zao. Wanaume kwa upande wao huzungumza kwa namna inayowatambulisha marafiki ‘walio katika kundi-ndani’ kwa kushiriki katika kicheko au kuwadhihaki wanaotanbiliwa kuwa wa ‘kundi-nje’. Pia washiriki wa kiume walitoa kauli ndefu mmoja kwa wakati mmoja ikilinganishwa na wanawake ambao walizungumza wengi kwa wakati mmoja. Washiriki wa kiume katika vikundi vilivyojumisha wanaume pekee. Katika vikundi vya kimseto, washiriki walidhihirisha sifa zilizochanganya mtindo wa kike na ule wa kiume katika mazungumzo. Sifa za mazungumzo baina ya jinsia mbalimbali katika tafiti za Coates, zilimsaidia mtafiti katika kuchanganua na kudondoa mifano katika tunukuzi zilizotokana na deta wake.

### **2.2.5.3 Urekebishaji katika Mawasiliano**

Urekebishaji katika Uchanganuzi wa Uzungumzaji, ni hali ambapo mzungumzaji hugundua makosa katika usemi alioutoa au usemi uliotolewa na mwenzake na kujaribu

kuukosoa aidha kwa kuurudia usemi ule akizingatia marekebisho au pale ambapo pametokea mgongano katika mazungumzo baina ya wazungumzaji (Fromkin, 1971).

Kwa upande wake, Liddicoat (2007) alifafanua kuwa urekebishaji ni hali ambayo hutokea baina ya wazungumzaji ili kutatua baadhi ya shida ambazo hujitokeza mazungumzoni. Shida hizo hutokana na hali za ubadilishanaji zamu na ukatanaji kalima ambazo hudhihirika mara nyingi maongezini. Urekebishaji huweza kutokea pale ambapo mzungumzaji amekosa msamati mwafaka wa kutumia mazungumzoni, na huenda akarejelea usemi wake pindi tu akumbukapo msamati ule. Kila hili linapotokea, huwa ni urekebishaji.

Schegloff *et al.* (1977) waliorodhesha na kufafanua aina nne za urekebishaji;

- a. Ujirekebishaji binafsi; msemaji hugundua makosa katika usemi wake na kuurudia upya akizingatia marekebisho ya makosa aliyoagundua katika usemi wake uliotangulia.
- b. Ujirekebishaji uliochochewa na msikilizaji wa usemi kugundua kuwa kuna makosa yaliyotokea katika usemi wa mwenzake.
- c. Mwingine kujirekebisha baada ya kugundua kuwa amekosea katika usemi wake. Au iwapo usemi wake umedhuru hisia za mwenzake.
- d. Mwingine kujirekebisha kwa sababu ameelezwa na msikilizaji kuwa amekosea katika usemi wake. Msikilizaji humwacha msemaji ajikosoe mwenyewe (Hutchby & Wooffit, 2002).

Wazungumzaji hubadilishana nafasi za kufanya urekebishaji katika mazungumzo ilimradi pasitokee matatizo baina yao. Baadhi ya matatizo hayo yaweza kuwa na madhara ya kukosa kuelewana au hata kudhuru hisia za washiriki wa mazungumzo. Schegloff na wenzake (1977), alimalizia mjadala wake kwa kuasa kuwa ijapokuwa mchakato wa urekebishaji ni mwelesi na hutokea bila ya wazungumzaji kugundua, waweza kuleta madhara na kuvunja mahusiano hasa unapokosa kutekelezwa ipasavyo. Mtafiti basi alichunguza njia tofauti tofauti walizozingatia washiriki katika biashara ya miraa ilmradi mazungumzo yao yakamilike kwa usambamba. Mahusiano hayo yalihuisha watu kutoka jamii tofauti hali ambayo ilikuwa ya muhimu sana katika kutathmini urekebishaji. Pia mtafiti alichunguza urekebishaji uliotokana na kauli zilizotolewa kwa lugha isiyofahamika na mshiriki mwezake kwa sababu za kuwa

wazungumzaji wa jamii tofauti. Pia, mtafiti alichunguza urekebishaji uliotokana na ukatizanaji kauli kati ya wazungumzaji.

#### **2.2.5.4 Ufungaji wa Mazungumzo**

Schegloff na Sacks (1973), walieleza kuwa mazungumzo hayafungwi kwa mpigo mmoja bali hukamilishwa kwa utaratibu fulani ambao huwafaa wazungumzaji husika. Madai yao yalitokana na hali ambayo ilikuwa inawasumbua wasomi kuhusu muundo ulioafiki wa kufunga mazungumzo. Katika jarida lao kuhusu kubainisha ukamilishaji wa mazungumzo, Schegloff na Sacks walieleza kuwa wazungumzaji huhakikisha wamemaliza yale yote walitaka kuzungumzia kabla ya kufunga mazungumzo baina yao. Mawazo haya, yalikuwa na umuhimu katika utafiti huu kwani wazungumzaji wa biashara ya miraa walipokamilisha mchakato wa kukagua, kuchagua na kulipa pesa ya bidhaa ndipo tungenesema kuwa walikuwa wamekamilisha kilichowapelekea kuzungumza. Kwa hivyo, mtafiti alichunguza mazungumzo na kutathmini jinsi ambavyo wanunuzi walitamatisha mazungumzo baada ya kukabidhiwa au kulipia bidhaa ya miraa.

Liddicoat (2007) alifafanua kuwa wazungumzaji huzingatia mbinu tofauti za kutua mazungumzo yao. Mambo muhimu ambayo yalionyesha kufungwa kwa mazungumzo ni kama vile;

- a) Msamiati wa kuaga. Pindi tu wazungumzaji walipoanza kusema maneno ya kuaga kama vile kwaheri, basi mazungumzo hayo yalikuwa yanamatika. Hata hivyo alifafanua kuwa mazungumzo hayo yangekuwa yamekamilika tu, iwapo pande zote mbili za wazungumzaji waliagana. Mtafiti alichunguza maneno hasa ya kutamatisha mazungumzo baina ya washiriki wa biashara ya miraa.
- b) Msamiati wa kukubaliana na mzungumzaji mwenza. Iwapo wazungumzaji walikubaliana kwa jambo sawa, basi mazungumzo yalikuwa yanafika tamati. Maarifa haya yalimfaidi mtafiti kwani alichunguza muundo wa lugha ya kujadili bei ya bidhaa hadi muuzaji na mnunuzi walipokubaliana bei sawa.
- c) Mmoja wa wazungumzaji kuomba kuondoka. Iwapo mmoja wa wazungumzaji alihisi kuwa alipaswa kuondoka, basi hiyo ilikuwa ishara kuwa mazungumzo yao yangekatika kwa ghafla. Katika mazungumzo ya washiriki wa biashara ya miraa, walichunguzwa wakijadili bei ya bidhaa na walivyotumia lugha kuomba kuondoka baada ya kununua.

- d) Ahadi za kupata kuwasiliana baadaye. Iwapo mazungumzo yalifungwa kwa ghafla, au kukawa na jambo la dharura ambalo liliwahitaji wazungumzaji kutamatisha mazungumzo yao kwa ghafla, huenda mmoja wao akaahidi kuendeleza mazungumzo baadaye (Button, 1991). Ahadi hiyo, iliashiria kuwa palikuwa na uwezekano wa kuendeleza mahusiano baina ya wazungumzaji, na kuwa palikuwa na nafasi nyingine ya kuwasiliana au kutangamana baina ya washiriki. Katika biashara ahadi kama hizi zilipotolewa na wanunuzi ilikuwa ni ishara kwamba huduma za kununua miraa siku ifuatayo au baadaye ilikuwa imehakikishwa. Ahadi hiyo pia ilionyesha uhusiano wa muuzaji na mnunuzi na uteja wake.
- e) Shukrani. Schegloff (1974), katika uchanganuzi wa mazungumzo ya simu alieleza kuwa wakati mmoja wa wazungumzaji kwenye simu walipotoa shukrani zao, basi ilikuwa ni ishara kuwa mazungumzo yao yalikaribia kukamilika. Katika mazungumzo ya biashara ya miraa pia, mtatifi alichunguza shukrani zilizotolewa na wauzaji au wanunuzi wa miraa kama ishara ya kutamatisha mazungumzo baina ya washiriki. Mtatifi alichunguza aina mbalimbali za utamatishaji wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi huku akidondoa mifano kutoka kwenye mazungumzo yao.

### **2.2.6 Unyenyekevu katika Mazungumzo**

Unyenyekevu ni dhana ambayo imeelezwa na wasomi wengi. Katika utafiti huu, dhana ya unyenyekevu inachukuliwa kama tukio la kipragmatiki. Hii ina maana kuwa unyenyekevu unatambulika iwapo muktadha maalumu wa mazungumzo umebainishwa. Fraser (1990) alieleza unyenyekevu katika vikundi vitatu; kikundi cha kwanza alikiita kanuni zinazothibiti mazungumzo ('conversational-maxims') ambazo zilirodheshwa na Leech (1983). Kulingana na Leech, wazungumzaji hushiriki katika ubadilishanaji wa mawazo ambayo huongozwa na kanuni maalumu.

Politeness is 'Costly to the speaker' or 'beneficial to the hearer'.

(Leech (1983a: 107-8))

Msemaji hutoa usemi ambao unaonyesha upole kwa malengo ya kumfaidi mpokeaji ili maongezi yaendelee kwa njia isiyoleta mgogoro.

(Tafsiri ya mtatifi).

Msemaji huchukulia kuwa ni jukumu lake kujali athari ambayo maneno yake yatakuwa nayo kwa mpokeaji. Kwa kufanya vile, mazungumzo huendelezwa na wazungumzaji

kwa njia isiyozua mgogoro baina ya washiriki wa mazungumzo. Kikundi cha pili, alieleza kuwa msemaji hujali tahayuri yake katika jamii ('Face management') kama ilivyoordheshwa na Goffman (1967). Kikundi cha tatu, Fraser (1990) alipendekeza unyenyekevu uangaliwe kama sheria ambazo huongoza maingiliano. Hivi kwamba, kila anayeingia katika tukio la kuingiliana, sharti atambue sheria na kuzielewa kabla kujitosa na kutoa mchango wake kama mmoja wa washiriki wa uzungumzi.

Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika mwongozo wa mwonekano ulioasisiwa na Goffman. Kulingana na Goffman, kila binadamu huwa na matamanio ya kukubalika na kupendeka na wenzake wanaoingiliana nao. Binadamu pia hupendelea kutoshinikizwa kufanya jinsi ambavyo ye ye binafsi hapendelei kufanya. Kwa hivyo, mwingilianaji huwa na mwonekano ambao angependa kuudumisha na unaovutia. Hali ya kutaka kupendeka na wengine husababisha waingilianaji kujali maslahi ya wenzao hali ambayo baadaye ilipata kurejelewa kama unyenyekevu.

Brown na Levinson (1987) nao waliendeleza dhana ya tahayuri na kutambua aina mbili za mwonekano. Walitambua mwonekano hasi na mwonekano chanya mtawalia. Mwonekano chanya walifafanua kama vitendo au maneno ambayo mshiriki wa maingiliano hutamani kusikia kutoka kwa wenziwe. Kwa mfano usemi kama vile, "Gari lako lapendeza sana." Usemi kama huo unaujenga mwonekano wa anayeupokea kwa sababu anafahamu kuwa vitu vyake ni vya thamani kwa macho ya wenzio. Anayezingatia aina hii ya unyenyekevu huwa na nia ya kutaka kupendeka, kukubaliwa au kuonyesha mshikamano baina ya kundi anaoingiliana nao.

Kwa upande mwingine, Brown na Levinson (k.h.j.) walifafanua mwonekano hasi kama matamanio ya kila binadamu kwamba maombi au vitendo vyake havipingwi au kuzuiliwa na ye yote. Mata kwa haya ya kutotaka maombi yao kipingwa na wengine ndiyo huwashinikiza watu kutumia misamiati kama vile; tafadhali, naomba, sumile, kwa hisani yako na mengine katika semi zao. Brown na Levinson (k.h.j.) waliorodhesha mikakati mitano ambayo inaweza kutumika kubainisha unyenyekevu katika semi za washiriki wa uzungumzi. Mikakati hiyo ilifafanuliwa kwa kina mwishoni mwa sura hii.

### **2.2.7 Unyenyekevu wa lugha kutegemea jinsia**

West na Zimmerman (1975) walichanganua maongezi baina ya washiriki wa kiume na kike katika duka la vyakula na kugundua kuwa utofauti mkubwa baina ya maongezi kati

ya wanaume na wanawake. Baadhi ya utofauti hutokana na viwango vyatunyenyeketu ambavyo hutumika katika usemi za jinsia hizi mbili.

Labov (1966), (1972), Trudgill (1972), Eckert na McConnell-Ginet (1992) wanaeleza kuwa wanawake ndio hutumia lugha sanifu, ya upole na yenye unyenyekevu mwingi. Sababu wanazotoa ni pamoja na kuwa wanawake hujali lugha ambayo watoto kama waendelezi wa jamii watajifunza wanapokua, kwani wanawake wanahusika moja kwa moja katika malezi ya watoto wakilinganishwa na wanaume. Maelezo yao kuwa wanawake hawatumii maneno yenye kuzua unyanyapaa na hujali hisia za wenzao wakilinganishwa na wanaume, ambao hutumia lugha kavu na isiyo na hisia nyingi kuashiria uhuru, umahiri na kujiamini katika ujuzi wao wa lugha. Wanawake kwa upande wao hutumia lugha yenye upole na heshima jambo ambalo hudhihirisha unyonje wao, kujali hisia za wenzao, kujieleza kihisia na utangamano baina yao. Maarifa haya yalimsaidia mtarufi katika kutambua mifano ya semi ziliviyotolewa na washiriki wa jinsia zote. Alidondo vipande hivyo kulingana na sifa zilizoorodheshwa na namna jinsia tofauti ziliviyotumia lugha na wateja wao katika muktadha wa kibashara.

Hata hivyo, De Klerk (1997) anasema kuwa mifumo ya lugha inayoeleza Labov na Eckert (k.h.j.), imebadilika kutokana na mpito wa wakati pamoja na tofauti za unyenyekevu baina ya jinsia zote mbili kukosa kudhihirika wazi. Chanzo cha mabadiliko hayo ni kuwa, masuala ya uana na jinsia yamebadilika kutokana na ukengeushi na pia mahusiano ya kijamii na matumizi ya lugha kubadilika. Maarifa haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu mtarufi alichunguza muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi wa jinsia tofauti ili kubaini iwapo muundo wa lugha ya wanaume na wanawake ultofautiana.

Njambi (k.h.j.), kwa upande wake, alitafiti kuhusu mifumo ya unyenyekevu ambayo wanabiashara wa jamii ya Gikuyu hutumia katika soko la nguo. Aligundua kuwa katika soko, wauzaji hudinda kutaja wanunuzi wa jinsia yoyote wanaponadi bidhaa. Haya huongeza nafasi ya kununuliwa kwa bidhaa zao na watu wa jinsia mbili. Pia, kutotaja majina ya watu kunadhihirisha unyenyekevu kulingana na jamii ya Wagikuyu. Katika utafiti huu, maarifa haya yalikuwa muhimu kwani yalimsaidia mtarufi kuangalia kwa kina jinsi wauzaji na wanunuzi walivyotaja wateja wao.

Miriti (k.h.j.), akizingatia lugha ya wafanya biashara baina ya Waigembe na Wasomali katika soko la Muringene na Maua, aligundua kuwa wafanya biashara wa kiume hutumia lugha mwiko kwa kiwango kikubwa. Kulingana naye, mitazamo ya kutisha ya Brown na Levinson (1987) inadhihirika na kudumishwa baina ya wauzaji.

Kwa kuzingatia maarifa haya, mtafiti alichunguza iwapo muundo wa mazungumzo ulizingatiwa bila kujihusisha na maneno mwiko wanayotumia wauzaji na wanunuizi.

Kutokana na mapitio ya maandishi aliyoyaeleza mtafiti, ni dhahiri kuwa tafiti za awali hazijachunguza muundo wa mazungumzo baina ya jamii mbili tafitiwa (Wasomali na Wameru). Ijapokuwa utafiti wa Miriti ulichunguza mikakati ya mazungumzo baina ya watu wa jamii hizo mbili, ye ye alitafiti mazungumzo ya sokoni kwa jumla. Utafiti huu kwa hivyo ulizama ndani na kuchunguza muundo wa mazungumzo ya ana kwa ana baina ya watu mahususi dukani pa kuuziwa na wala siyo sokoni tu.

### **2.3 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Nadharia ya Uchanganuzi wa Uzungumzaji iliyoasisiwa na Sacks, Schegloff na Jefferson (1974), na Nadharia ya Unyenyekevu mkabala wa Brown & Levinson (1987). Mtafiti alieleza kwa kifupi waasisi wa nadharia moja baada ya nyingine, mihimili yake na jinsi zilivyotumika katika utafiti huu.

#### **2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Uzungumzaji**

Nadharia hii iliasisiwa na mwanasosholojia Sacks katika miaka ya (1960). Aligundua kuwa mazungumzo yanayotekelawa na binadamu huwa yana mpangilio fulani kama vile ubadilishanaji zamu katika maongezi ya simu au baina ya watu katika taasisi za kijamii. Sacks alitoa mifano ya maongezi baina ya daktari na mgonjwa, mwalimu na mwanafunzi, hakimu na mshtakiwa au mzazi na mwanawewe ili kuonyesha muundo wa maongezi yao ya ana kwa ana. Akichochewa na maarifa ya Sacks, mwanasosholojia mwingine Goffman (1967), alieleza kuwa maongezi ya ana kwa ana, huchukua mpangilio maalumu na washiriki hushirikiana katika kudumisha mwonekano wa wenzao katika mkabala mzima wa maongezi. Garfinkel (1967), kwa upande wake alichangia katika kuendelea kwa nadharia hii kwa dhana ya ethnometholojia. Garfinkel, alieleza kuwa watu huzingatia tamaduni zao wanapotumia lugha na jinsi tamaduni zilivyo nyingi basi ndivyo watumizi lugha wanazo njia tofauti tofauti za kutumia lugha kwa minajili ya kuendeleza mazungumzo na mawasiliano. Garfinkel pia, alieleza kuwa watu hutumia maarifa waliyojifunza kutokana na jamii walizozaliwa katika

kuhusiana na wenzao kwa sababu lugha ni mojawapo ya kitambulisho cha utamaduni wa mtu.

Sacks (1974), alieleza kuwa zamu ndicho kiini cha maongezi yoyote yale yawe ya ana kwa ana au ya simu. Alieleza kuwa msururu wa kupishana zamu baina ya wazungumzaji hudhibiti mazungumzo. Washiriki wa uzungumzaji hubaini vidokezo vyta kuonyesha nafasi za kuchukua zamu. Wakizingatia miadhara ya Sacks, Jefferson na Schegloff (1974), walieleza kuwa wazungumzaji hubainisha zamu zao na kuwa ‘angalau mtu mmoja tu anapaswa kuzungumza katika kipindi kimoja cha wakati (Sacks, 1992)’. Pia walieleza kuwa mazungumzo yanapaswa kufanyika pasi na ukataji kalima wala kuwepo na hali kutobaini zamu ipi ni ya nani. Iwapo basi watu wengi watazungumza kwa wakati mmoja basi mfanyiko wa mazungumzo utakuwa umejaa ukataji kalima ambalo huzuia mafanikio ya mazungumzo. Kulingana na Sacks na wenzake (k.h.j.) kuzungumza kwa watu wengi kwa wakati mmoja au kukosa kuelewa zamu bayana, ni uvunjaji wa kanuni na haki za mzungumzaji anayezungumza.

### **2.3.1 Mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi wa Uzungumzi**

Heritage (1984) anaeleza misingi mitatu ya nadharia hii;

- i. Mazungumzo huwa na vifunguzi na vitamatishi. Hivi kwamba, mazungumzo hufuata misamiati maalum ambayo huashiria kuwa yanaanza na vilevile kukamilika.
- ii. Mazungumzo ya kawaida yana mpangilio wa kimuundo; kwa kawaida mazungumzo huwa na mpangilio wa kiwango fulani. Hivi kwamba angalau mtu mmoja azungumze kwa kipindi kimoja cha wakati.
- iii. Mazungumzo huwa yamejengeka katika muktadha mahususi kama vile; darasani, hospitali, kanisani, kazini, sokoni, shuleni, na biasharani.
- iv. Hali ya muundo inaweza kukiukwa na kukiukwa kwa muundo pia kukawa na maana yake.

Katika utafiti huu, mihimili mitatu ya nadharia hii ilitumika kwa sababu muktadha umebainishwa (maingiliano baina ya wauzaji na wanunuzi wa miraa kutoka jamii ya Wameru na Wasomali wanaopatana Eastleigh, Nairobi).

- i. Mazungumzo huwa na vifunguzi na vitamatishi. Mtafiti alichunguza jinsi wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa waliyafungua mazungumzo pamoja na kuyatamatisha.

- ii. Mazungumzo ya kawaida yana mpangilio wa kumuundo. Mtafiti alizingatia mhimili huu kubainisha muundo wa ubadilishaji zamu baina ya washiriki wa biashara ya miraa.
- iii. Hali ya muundo inaweza kukiukwa na kukiukwa kwa muundo huo pia ukawa na maana yake. Mtafiti atachunguza ukiukaji wa muundo hasa kuhusu mpishano zamu na masharti ya angalau mtu mmoja kuzungumza kwa kipindi kimoja cha wakati unavyoathiri utendaji wa unyenyekevu katika mahusiano ya biashara ya miraa.

Hata hivyo, nadharia hii haikumfaa mtafiti kikamilifu kubainisha namna watu wanavyoshirikiana katika kubadilishana zamu na kufahamu njia za utendaji unyenyekevu katika mawasiliano ili kudumisha muundo wa kimaingiliano. Ndiposa mtafiti aliangazia nadharia ya pili.

### **2.3.2 Nadharia ya Unyenyekevu**

Nadharia hii ililiasiwa kutokana na mawazo ya Goffman (1967) ya mwonekano wa mtu mbele ya washiriki wa uzungumzi. Alieleza kuwa mtu huwa na nia ya kupendeka na vitendo vyake kukubalika na wengine pasi na kushinikizwa na yejote kutenda mambo kwa njia fulani. Alieleza kuwa mwonekano huo hupata kutishiwa na wengine kila mara maingiliano hutokea. Kutokana na mawazo hayo ya Goffman, Brown na Levinson (1987) walibainisha aina mbili za mwonekano ambazo ni aina mbili za unyenyekevu. Aina ya kwanza waliyooita mwonekano chanya, ni mbinu anayoitumia mshiriki wa maingiliano, kuzua semi zenye kukubalika ili watimize malengo yao ya maingiliano (kukubaliana au kupendeka na wengine ndilo lengo la kutenda aina hii ya unyenyekevu).

Kwa upande wa pili, mwonekano hasi ni hali ambapo mshiriki wa maingiliano hupenda kujitambulisha kama mshiriki aliye na mwelekeo binafsi na wengine bila kutaka kushinikizwa kutenda kwa njia fulani (lengo lake ni kutotaka matendo yake kuzuiliwa au kucheleweshwa na yejote katika kipindi fulani cha wakati. Kwa mfano, iwapo anataka kumwona mwalimu, anataka amwone wakati huo huo. Iwapo utamwambia kuwa asubiri kidogo kwa kuwa mwalimu anashughulikia mwanafunzi mwingine, basi utakuwa unaathri mwonekano wake kwa njia iliyo hasi. Brown na Levinson (k.h.j.) walieleza kuwa, wakati mwingine waingilianaji huhisi kuwa matendo au maneno ya wengine hudhuru au kukandamiza mwonekano wao. Kutokana na vitendo au maneno

yanayotishia mwonekano, walieleza njia za kuokoa mwonekeno (kujiepushia tahayuri) ambayo kwa neno jingine ndilo huitwa unyenyekevu.


Unyenyekevu basi ni namna ya kutumia lugha kwa nia ya kuhifadhi hisia au mwonekano wa wale wanaohusika katika maingiliano, huku kila mwingilianaji akitilia maanani kuwa mwonekano wa mwenzake uko hatarini kila mara na kwa hivyo kuamua kuchagua mikakati ya namna fulani. Brown na Levinson (k.h.j) mbinu mbili za kutambua kuwa mwonekano umethuriwa na namna za kukabiliana na tishio hilo;

- Matendo ya kujiepushia tishio kwa mwonekano ulio chanya (unyenyekevu chanya)
- Matendo ya kujiepushia tishio kwa mwonekano ulio hasi (unyenyekevu hasi)

Kutokana na mionekano hii miwili ya unyenyekevu, Brown na Levinson waliorodhesha mikakati mitano ya kukabiliana na tishio kwa mwonekano na hii ndiyo mihimili ya nadharia hii kama ifuatavyo:

- i. Sema waziwazi kumaanisha kuwa useme chochote unachopenda bila kujali maslahi au mwonekano wa mwenzako
- ii. Unyenyekevu chanya-utakachokisema kiwe ni kwa ajili ya kutaka kupendwa au kukubaliana na kikundi cha watu mnaoingiliana nao.
- iii. Unyenyekevu hasi – utakachokisema ni kwa minajili ya kutotaka kushinikizwa au kuzuiliwa kutenda kwa njinsi utakavyo.
- iv. Usiseme chochote- nyamaza tu na utende bila kusema maneno yoyote.
- v. Usifanye au kusema kitakacholeta tishio kwa mwonekano wa wenzako.

Brown na Levinson walitumia kielelezo matawi kifuatacho kuonyesha njia ambazo hutumika kuteua mkakati wa kutumia unyenyekevu;



*Jedwali 1: Kielelezo cha Mikakati ya Unyenyekevu kutoka Brown na Levinson (1987:60)*

Mhimili mitatu ilitumika katika utafiti huu.

- i. Sema chochote unachokisema bila kujirekebisha kwa kutishia mwonekano wa mwingine. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kubainisha semi ambazo zilionekana kuzua tahayuri na ambavyo waliopokea au kuzitoa walihisi kuhusu kauli kama hizo.
- ii. Unyenyekevu hasi. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kubainisha jinsi wauzaji waliitisha au kuomba kuuzziwa miraa na maneno yaliyotumika ili wasihisi kuwa mionekano yao imetishiwa au kugandamizwa.
- iii. Unyenyekevu chanya. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kubainisha kama ukabila au ujinsia wa mshiriki uliathiri namna alivyotumia lugha yake. Hivi kwamba aliyetumia lugha alifanya vile kwa kutaka kupendeka na mwenzake kwa sababu walitoka katika kabilia lake au walikuwa wa jinsia moja au tofauti. Mhimili huu pia ulimwezesha kutambulisha iwapo kulikuwa na faida au gharama ambayo mnunuzi au muuzaji alipata kwa kutumia lugha kwa kutimiza malengo ya kikundi-ndani.

## **2.4 Hitimisho**

Katika sura hii, maandishi ya awali yалиhakikiwa yakiwemo ya miraa kama bidhaa ya biashara, uchanganuzi wa usemi, upishanaji zamu katika maingiliano, urekebishaji, maingiliano ya kikabila, maingiliano ya kijinsia, unyenyekevu misingi ya nadharia na mihimili ya nadharia. Kutohana na yaliyopitiwa ilibainika kuwa muundo wa mazungumzo kama vile; upishanaji zamu, ufunguzi, ukataji kalima, urekebishaji pamoja na utendaji wa unyenyekevu katika maingiliano ya kibiashara baina ya Wameru na Wasomali haukuwa umechananuliwa na ndiposa utafiti huu ulilenga kujaza pengo hilo la kimaarifa.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inaeleza muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, umma uliolengwa, vifaa na ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data pamoja na masuala ya kimaadili.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ulizingatia muundo wa kithamano. Mkabala wa kiufasiri maelezo. Maelezo fasiri mengi yalitumika kwa kutolea mifano na kufafanua baadhi ya semi au vitendo vya washiriki wa utafiti. Kothari (2004) anaeleza kuwa tafiti za kimaelezo ni zile ambazo hutumika kupima viwango vya tabia fulani ya binadamu kwa kuifafanua ili kudhihirisha ni nini haswa huwasukuma watu kutenda au kusema namna wanavyotenda katika jamii.

Creswell (2009) anaeleza kuwa utafiti wa kithamano hutumia maelezo mengi badala ya takwimu. Huwa ni njia ya kueleza baadhi ya tabia ambazo hudhihirishwa na wanajamii katika miktadha halisi ya jamii. Mtafiti huchunguza namna watu wanaotafitiwa hutenda na kuhisi au kuzungumzia maswala yao katika mazingira asilia ya kijamii ambapo ni mtafiti huenda kuwatafuta watafitiwa nyanjani na wala si kuwaleta katika maabara. Kutokana na tabia na matendo yanayorudiwa rudiwa na watafitiwa, mtafiti huweza kukisia au kuelewa ni kwa nini watafitiwa hutenda kama wanavyotenda.

Katika utafiti huu takwimu chache pia zilizingatiwa ili kuonyesha umaratokezi wa mikakati ya utendaji wa unyenyekevu baina ya washiriki. Kiambatisho 2 kilionyesha baadhi ya matendo na tabia ambazo mtafiti alikuwa akizitazama katika maingiliano ya moja kwa moja baina ya mnunuzi na muuzaji. Kiambatisho 3 nacho kilionyesha mada ambazo zilijadiliwa na mtafiti na washiriki katika vikundi viini. Mtafiti alizingatia tafiti za Schegloff (1987) zilizohusu mawasiliano ya kimaingiliano katika miktadha ya kijamii ili kubainisha na kueleza sifa asili na bainifu za sajili walizoteua washiriki. Data katika utafiti huu ilikuwa ni maongezi yaliyotokana na maingiliano baina ya muuzaji na mnunuzi pamoja na majadiliano yaliyotekelawa katika vikundi viini.

### **3.3 Mahali pa Utafiti**

Utafiti ulifanyika katika mtaa wa Eastleigh, jimbo la Nairobi, kaunti ndogo ya Kamukunji, eneo bunge la Kamukunji katika wadi ya Eastleigh Kaskazini. Mtaa huu upo upande wa mashariki kutoka katikati mwa jiji la Nairobi (**Tazama kiambatisho 5 cha ramani katika ukurasa 109**). Idadi ya wakaazi wa Eastleigh kutokana na takwimu ni 44,037,656 wengi wao ni wakiwa ni watu wenye asili ya nchi jirani ya Somali waliofika mtaani humo kama wakimbizi katika miaka ya 1990. Jamii hii hujihusisha na biashara za aina nyingi na kuchangia pakubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi ya Kenya. Wasomali ni wengi katika eneo hili ambapo miraa imekuwa ikiuzwa na jamii ya Wameru kwa miaka kadha (Carrier, 2007). Eastleigh ni eneo lililo maarufu sana katika uuzaaji na usambazaji wa miraa (Beckerleg & Sheekh, 2005) na ndiyo maana mtafiti alichagua eneo hilo la utafiti.

### **3.4 Umma Lengwa**

Katika utafiti huu, umma uliolengwa ni wauzaji na wanunuzi wa miraa nchini Kenya. Umma uliotafitiwa ni wauzaji na wanunuzi miraa kutoka jamii ya Wameru na Wasomali wa jinsia ya kike na kiume waliopatikana katika eneo la Eastleigh, katika jimbo la Nairobi. Washiriki 48 walichunguzwa katika maingiliano yao asilia ya kibashara. Matokeo yaliyotokana na utafiti huu yalijumulishwa kwa umma unaoshiriki katika shughuli za ununuzi na uuzaaji wa miraa nchini Kenya baina ya makabila makuu mawili - Wameru na Wasomali.

### **3.5 Uteuzi wa Sampuli**

Sampuli iliteuliwa kimakusudi. Mtafiti aliwateua washiriki kwa kuzingatia jinsia na khabila lao. Mtazamo wa kimaingiliano ya kijamii au uelekezi wa Milroy (1987) ulitumika katika kuteua washiriki, ambapo mshiriki wa kwanza aliteuliwa kimakusudi, kisha muuzaji wa kwanza alimwelekeza mtafiti kwa mshiriki mwingine aliye na sifa kama zake kutegemea jinsia au khabila hadi mtafiti akawatambua idadi ya washiriki 48 walitumika katika utafiti huu. Mtafiti pamoja na msaидизи wake walifika dukani waliyoteua kimakusudi na kujitambulisha kwa muuzaji (ambao wengi walikuwa ni marafiki au wenye uhusiano wa kibashara na mtafiti msaидизи). Baada ya utambulisho, mtafiti na msaидизи wake walitembelea maduka hayo kwa mara nyingi hadi (mtafiti) akawa haonekani kuwa mgeni tena kwa washiriki wa biashara hiyo. Mtafiti alirekodi mazungumzo ya moja kwa moja kati ya muuzaji na mnunuzi kumi, baada ya kuwajuza

kuwa alikuwa anarekodi uzungumzi wao. Kulingana Dornyei (2007), tafiti za kiisimu zinaweza kujumisha washiriki thelathini pekee. Hii ni kutokana na uwezekano wa urudiaji kwani deta huwa ni ya kimazungumzo. Hata hivyo kurekodi mazungumzo pekee hakukutosha, kwa hivyo mtafiti alishirikisha washiriki wengine katika mijadala ya vikundi viini ili kupata ufanuzi wa baadhi ya dhana zilizogunduliwa katika kurekodi. Washiriki ishirika ni na wanane waliwekwa kativikundi viini vitatu -kila kikundi kikiwa na washiriki tisa na kujadili maswala kuhusu utumizi-lugha katika biashara ya miraa. Jumla ya watu 48 ilitumika kama idadi wakilishi ya washiriki wa biashara ya miraa katika eneo la Eastleigh.

Washiriki katika maingiliano ya moja kwa moja (kuuza na kununua) <b>20</b>				Washiriki katika majadiliano ya vikundi viini <b>28</b>				Jumla <b>48</b>
Wameru 10		Wasomali 10		Wameru 14		Wasomali 14		48
Kiume 5	Kike 5	Kiume 5	Kike 5	Kiume 7	Kike 7	Kiume 7	Kike 7	48

*Jedwali 2: Uteuzi wa Sampuli*

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kwa kuzingatia utazamaji muundo (wa kushiriki na usio wa kushiriki) na majadiliano yaliyofanyika katika vikundi viini.

#### 3.6.1 Utazamaji

Muundo wa utazamaji wa kushiriki na usio wa kushiriki ulizingatiwa katika utafiti huu. Mbinu ya utazamaji usio wa kushiriki, kama alivyoeleza Kothari (2004), ni hali ambapo mtafiti huenda mahali ambapo kitendo anakichotafiti kinatendekea lakini yeye mwenyewe hashiriki katika kutenda vitendo hivyo. Pia, anaeleza mbinu ya kushiriki katika utazamaji kama hali ambapo mtafiti huenda nyanjani na kushiriki moja kwa moja katika yale yanayoendelezwa na washiriki lengwa wa utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti alishiriki katika kununua na kuuza miraa ili apate data asilia pasipo kuonekana au kuchukuliwa na wenyeji kama mtu aliyejidukiza katika maingiliano yao.

Vilevile, mtafiti kama mshiriki katika utangamano wa kuuza na kununua bidhaa aliuliza ya maswali moja kwa moja ili kupata ufanuzi wa baadhi ya tabia na matumizi ya lugha ambazo zilimvutia na kuchangia katika kufanikisha malengo ya utafiti wake.

Fauka ya hayo, baadhi ya matendo au mambo muhimu ambayo mtafiti aliyashuhudia yalinukuliwa daftarini na yakafafanuliwa katika mijadala ya vikundi viini (Tazama **kiambatisho 2 katika Uk. 106**) ambacho ndicho kilikuwa mwongozo wa Utazamaji).

Utazamaji usio wa kushiriki pia ulimfaidi mtafiti. Mtafiti alitazama tu mara 14 na hakushiriki bali aliwaacha washiriki 28 wa ununuzi na uuzaji kutenda vitendo vyao kwa njia ilio asilia. Kutoshiriki kulimfaa mtafiti kwani washiriki walitoa semi zao pasi na kuathiriwa na uwepo wa mtafiti. Data iliyotokana na utazamaji ilikuwa nzito mno kwani ilikuwa ni matokeo ya hali halisia ya vitendo na maneno kama yalivyotolewa na wasemaji. Hata hivyo, mbinu ya utazamaji ilikuwa na upungufu wake. Upungufu huu ni kama vile data kukosa ufanuzi kwani mtazamaji alitazama tu. Upungufu huu ndio uliomshinikiza mtafiti kutumia mbinu ya kurekodi.

### **3.6.2 Kunasa na Kurekodi Sauti**

Kunasa ni kurekodi kisauti matukio asilia kama yanavyojitokeza nyanjani. Hii ni mbinu mojawapo ambayo mtafiti alitumia ili kunasa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuvi pamoja na mijadala katika vikundi viini. Kinasa-sauti kiliwekwa chini ya meza ambayo iliwatenganisha wauzaji na wanunuvi. Mazungumzo ya moja kwa moja baina ya muuzaji na mnunuvi yalinaswa, yakasikilizwa na hoja muhimu zikadondolewa ambazo zilitumiwa kuongoza mijadala katika vikundi viini. Ukusanyaji huu wa data ulizua data iliyotunukuliwa na kutumika katika uchanganuzi.

### **3.6.3 Mijadala katika Vikundi Viini**

Baada ya kukusanya na kurekodi maingiliano ya moja kwa moja baina ya wauzaji na wanunuvi, mtafiti na washiriki teule waliokuwa wamerekodiwa huku wakinunua au wakiwa walishiriki katika mijadala. Kulingana na Stokes na Blackburn (2001), vikundi viini, ni nyenzo muhimu ya kutafiti hasa pale ambapo maoni ya watafitiwa kuhusu jambo fulani linalotafitiwa hujadiliwa. Stokes na Blackburn (k.h.j.) wanazidi kueleza kuwa, jinsi watafitiwa wanavyotumia lugha kueleza suala husika huwa ni muhimu sana kwani huashiria wanavyohisi. Mtafiti alitumia mbinu hii kupata maelezo na hisia za watafitiwa kuhusu lugha na utendaji wa unyenyekevu katika biashara ya miraa mtaani Eastleigh. Mtafiti alikuwa na maswali aliyokuwa ameyanukuu kutohakana na utazamaji ambayo aliwauliza washiriki.

Mijadala ilifanyika katika vikundi viini vitatu. Kila kikundi kilikuwa na washiriki tisa walioteuliwa kimakusudi na mtafiti. Njia aliyotumia mtafiti kuamua walioshiriki katika mijadala, ni pale aliwaomba baadhi ya wanunuzi kushiriki baada ya kununua miraa yao. Pia mtafiti alifika Eastleigh mapema kabla ya miraa kufika madukani na hapo alipata nafasi ya kujadili mada tofauti na wauzaji. **Kiambatisho 3 katika Uk. 107** kilitumika kama mwongozo wa mijadala baina ya mtafiti na washiriki katika vikundi viini. Mtafiti alielekeza mijadala hiyo huku akiandika hoja muhimu katika daftari pamoja na kunasa majadiliano baina ya washiriki wa vikundi kwa kinasa sauti.

### **3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data**

Mtafiti aliichanganua data kithamano kwa kuzingatia mfumo wa unukuzi wa Heritage (1984), ambapo mtafiti alinukuu maongezi, ili kubainisha baadhi ya uzingatiaji wa vipengele vya kimuundo k.v. ufunguzi, ubadilishanaji zamu, ukataji kalima, ufungaji na utendaji wa unyenyekevu katika lugha zungumzwa baina ya wanunuzi na wauzaji wa miraa. Cameron (2001), anaeleza kuwa Nadharia ya Uchanganuzi wa Uzungumzi huhusisha kunukuu maneno na vitendo vya watumizi lugha katika hali asilia na kisha kuchanganua semi zao ili kupata maarifa mengi tu, ambayo yaweza kupatikana katika kipande hicho. Kwa kuzingatia maarifa ya Cameron (k.h.j.), tunukuzi baina ya wanunuzi na wauzaji pamoja na majadiliano katika vikundi viini yalifanyiwa uchanganuzi wa yaliyomo bila kubadilisha chochote.

Mazungumzo baina ya washiriki yalinukuliwa kwenye karatasi kwa lugha ya Kiswahili na wakati wa kunukuu mazungumzo yalipewa kodi maalumu kutegemea jinsia na kabilia la washiriki. Maarifa kuhusu mikakati ya unyenyekevu waliyoitumia na mabadilishano ya zamu baina ya washiriki wa biashara ya miraa kitongojini Eastleigh yalibainishwa kulingana na madhumuni ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia. Data iliwasilishwa kwa kutumia majedwali na maelezo ili kuonyesha umaratokezi wa mikakati ya unyenyekevu miongoni mwa washiriki wa jinsia na kabilia tofauti.

### **3.8 Maadili ya Utafiti**

Katika tafiti za nyanjani, mtafiti hutarajiwu kuzingatia maadili ya utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti aliwajulisha wasimamizi wa soko na viongozi wa serikali tawala katika eneo la utafiti kuhusu utafiti aliokuwa akitekeleza ili awe huru kutangamana na watu sokoni bila kuogopa kushukiwa na washiriki wa biashara. Kufanya hivi, kulimsaidia mtafiti kukusanya data iliyo asilia kabisa kwani washiriki hawakubaini wala kushuku

kuwa maingiliano yao yalikuwa yanarekodiwa. Kabla ya kurekodi mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi wa kwanza. Hata hivyo, changamoto iliyokumba utafiti ni kwamba mtarufi hangeweza kuwaarifu wanunuzi wote kuwa mazungumzo yao yalikuwa yakirekodiwa. Washiriki waliokuwa tayari kurekodiwa wakinunua waliombwa kushiriki katika mijadala ya vikundi viini. Waliodinda kushiriki au mazungumzo yao kurekodiwa pia walihakikishiwa kuwa hawangerekodiwa. Vilevile, katika vikundi viini, mtarufi alijieleza kwa washiriki kuwa anashughulikia vipashio vyta lugha wanayotumia katika biashara, na wala siyo miraa kama bidhaa. Zaidi ya hayo, aliwaeleza washiriki wa mijadala katika vikundi viini kuwa maongezi yao yangerekodiwa na yanetumika kwa sababu za kitafiti pekee. Fauka ya hayo, aliwahakikishia kuwa majina yao halisi yangebanwa na kupewa kodi maalumu (k.m. MM001A, SM001B **tazama Kiambatisho 6, Uk. 110**) katika uchanganuzi wa data. Mtarufi aliwahakikishia wenye maduka kuwa majina ya maduka yao pia yangebanwa katika unukuzi wa data iwapo kuna pale yanapotajwa katika maongezi baina ya mnunuzi na muuzaji.

Watafiti wasaidizi wanaofahamika kama wanunuzi au wauzaji walitumika katika kurekodi baadhi ya maingiliano. Eastleigh ni mojawapo ya maeneo nchini Kenya ambayo yamehusishwa na ukosefu wa usalama hivyo ilibidi mtarufi kutembea katika eneo hilo mchana na akiandamana na marafiki wanaofahamika katika sehemu hiyo ili kurahisisha maingiliano na ushiriki kwenye utafiti. Vilevile, mtarufi aliwaeleza washiriki wa vikundi kiini kuhusu madhumuni ya utafiti wake. Mtarufi alitafuta vibali kutoka afisi za uongozi katika eneo la Eastleigh na taasisi ya utafiti wa sayansi na teknolojia (NACOSTI)-**Tazama kiambatisho 4, Uk. 108** kabla ya kutangamana na kutekeleza utafiti katika eneo hilo.

## SURA YA NNE

### UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amewasilisha data kufuatia mpangilio wa madhumuni matatu ya utafiti na nadharia mbili za utafiti; Uchanganuzi wa Uzungumzi Sacks, Schegloff na Jefferson (1974) na Nadharia ya Unyenyekevu Brown na Levinson (1987). Maswali ya utafiti ambayo yalikusudiwa kupata majibu katika sura hii yalikuwa ni; kwanza, mazungumzo baina ya wanunuzi na wauzaji huchukua muundo gani? Pili, vigezo vyta ukabila na jinsia ya wauzaji na wanunuzi huathiri vipi muundo wa mazungumzo baina ya watu kutoka jamii ya Wasomali na Wameru? Tatu, ni mikakati gani ya unyenyekevu huzingatiwa na wanunuzi na wauzaji kutoka jamii ya Wasomali na Wameru katika biashara ya miraa? Matokeo yaliwasilishwa kuitia maelezo fasiri na majedwali ya kuonyesha umaratokezi .

#### 4.2 Muundo wa Mazungumzo

Sehemu hii inashughulikia lengo la utafiti huu, ambalo lilikuwa ni kubainisha muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa. Kuhusu muundo wa mazungumzo, Heritage (1984), anaeleza kuwa muundo ambao uzungumzi huchukua hutekelezwa na washiriki pasi na ufahamu wao wa moja kwa moja (unconsciously). Kwamba, washiriki hawaamui mpangilio wa mazungumzo yao kabla ya mazungumzo yenyewe kufanyika, bali hutokea tu kiuasili. Kwa hivyo, washiriki huwa wanashirikiana katika kuendeleza mazungumzo yao ili kufanikisha lengo lao la kuzungumza. Kuhusu muundo, mada zilizojadiliwa ni pamoja kama zinavyoodheshwa kwenye **jedwali 3** ni: ufunguzi wa mazungumzo, ubadilishanaji zamu, ukataji kalima, urekebishaji na ufungaji wa mazungumzo katika biashara ya miraa.

VIGEZO	VIASHIRIA	KUWEPO	KUTOKUWEPO
VIFUNGUZI	SALAMU	√	×
UBADILISHAJI ZAMU	ZAMU SAHILI	√	×
	ZAMU CHANGAMANO	√	×
UKATAJI KALIMA	MNUNUZI MMOJA	×	√
	WANUNUZI WENGI	√	×
UREKEBISHAJI	KIBINAFSI	√	×
	MWINGINE	√	×
UFUNGAJI	MAAGANO	√	√

Jedwali 3: Vidokezo na Utokeaji wa Muundo wa Mazungumzo

#### **4.2.1 Vifunguzi vya Mawasiliano**

Vifunguzi ni maneno ambayo mshiriki wa kwanza anayeanzisha mazungumzo hutoa, kabla ya yule mshiriki mwingine katika mchakato wa maingiliano. Vianzo vya mazungumzo yoyote yale yafanywayo huegemea kwenye muktadha (Schegloff E. A., 2007). Kwa hivyo yote ambayo wanaoshiriki katika mazungumzo husema, hutegemea ni wapi na ni kina nani wanaotangamana nao. Katika muktadha wa kibiasara ya miraa (muktadha maalumu), mtafiti alichunguza mazungumzo baina ya wanunuzi na wauzaji yalivyoanzishwa na ni nani aliyeanzisha na maneno yake ya ufunguzi yalihusu nini haswa. Katika utafiti huu maamkuzi na semi za mwanzo za aliyeanzisha mazungumzo ndizo zilichukuliwa kuwa vifunguzi vya mawasiliano baina ya washiriki. Pia, yote yaliyojiri baina ya mnunuzi na muuzaji kabla ya mnunuzi kukabidhiwa kifurushi cha miraa, yalichukuliwa kuwa ni ufunguzi wa mazungumzo. Katika biashara ya miraa, mpangilio wa vifunguzi ufuatao ulibainishwa,

**F-Kike, MTF- mtafiti, M-Kiume, S- Somali, m-meru, n, mnunuizi , z - mnunuizi,  
A, B, C- vikundi viini. k.m. Mm<sub>N</sub>1= ni Mwanamume mmeru mnunuizi wa  
kwanza(1) na FS002B ni F- kike Somali mzungumzaji wa pili katika kikundi kiini B.**

## Mfano 1:



(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)

Katika **mfano 1**, mnunuzi alianza kupaaza sauti yake kutoka mbali kabla ya kufika katika duka lenyewe. Kisha anaendelea kusema anachokihitaji kabla ya kuwaamkua wauzaji waliopaswa kumhudumia. Vilevile  $S_{M_N}7a$ , hampi nafasi mshiriki mwenzake achukue nafasi ya kujibu iwapo miraa ilikuwepo au haikuwepo. Alisema hatu pesa ambazo alitaka kununua hiyo miraa “Nataka *Giza* ya elfu moja.” Kulingana na **mfano 1**,  $S_{M_N}7a$  alifungua mazungumzo kwa njia hiyo kwani alikuwa na haraka. Na alikuwa anataka kufanyiwa huduma ya haraka kwani alikuwa na kazi nyingi iliyomsubiri. Ujumbe huu tuliupata katika kauli zake za baadaye katika mfano ufuataao.

### **Mfano 2:**

1. Sm<sub>N</sub>7a: [giza] giza mzuri kilo moja lete..((anakabidhiwa kilo moja ya miraa na anaanza kuikagua))
2. Mm<sub>z</sub>1a: si umerudisha?
3. Sm<sub>N</sub>7a : leta kilo mzuri. Tafadhalii.
4. : Iko Kazi mingi
5. : wewe iko na mchezo eeh
6. Mm<sub>z</sub>1a: [wee shika
7. : Wariah hakuna miraa.

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)**

Sm<sub>N</sub>7a alikuwa na haraka, ndiposa alifika dukani akiomba miraa aina ya giza na alitaka auziwe bei ya shilingi elfu moja. Haya yote aliyatenda ilmuradi aokoe muda ambao angekuwepo pale dukani. Kutokana na mifano hii, ufunguzi wa mazungumzo haya yalikuwa ya kimakusudi tu, na kwa sababu za kuokoa muda wa mnunuzi Sm<sub>N</sub>7a. Pia, maamkuzi yalizingatiwa na baadhi ya wanunuzi na wauzaji kama njia mojawapo ya kufungua au kuanzisha mazungumzo. Maamkizi hayo yalikuwa ya aina tofauti: kuna wanunuzi waliofika dukani na kumwita muuzaji kwa jina lake, pili kuna wauzaji waliojituma kuwaamkua wateja wao.

### **Mfano 3:**

1. Mm<sub>z</sub>8d: Sema my brother (sema ndugu yangu)
2. Mm<sub>z</sub>8d: hii miraa mzuri kabisa
3. Sm<sub>N</sub>11d: haina maji?
4. Mm<sub>z</sub>8d: Hapana haina maji hata
5. Sm<sub>N</sub>11d: haiya haiya haiya
6. Mm<sub>z</sub>8d: Kwani unataka miraa kavu?
7. :Hii iko na maji?
8. :Wewe iko meno si ndio?
9. Sm<sub>N</sub>11d: aa hii ni safi
10. Mm<sub>z</sub>8d: Mbili?
11. Sm<sub>N</sub>11d: Nifungie hii moja eeh.
12. Mm<sub>z</sub>8d: Haya sawa Engineer. Sawa brother (sawa ndugu) (mnunuzi anaondoka)

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo d Uk. 116)**

Katika **mfano 3**, Mm<sub>z</sub>8d anamwamkua mnunuzi wake kwa kusema, "sema my brother." Kwa kumuuliza mnunuzi amweleze hitaji lake, Mm<sub>z</sub>8d alikuwa tayari kumhudumia. Kisha baada ya salamu, anamkabidhi Sm<sub>N</sub>11d miraa na kuisifia bidhaa yake, "ni miraa mzuri kabisa" ili Sm<sub>N</sub>11d ashawishike kuinunua.

Salamu zilipotolewa na mhudumu katika mazingira ya kikazi, zilimshawishi anayepewa huduma kuhisi akiwa huru zaidi katika utangamano anaoshiriki Rice na wenzake (2013). Mfano 3 unakubaliana na mawazo ya Rice na wengine (2013), kwani  $SM_N 11d$  anapokosa kuipenda miraa aliyokabidhiwa na  $MM_z 8d$  anahisi kuwa anao uhuru wa kuitisha miraa nyingine hadi ainunue ile inayomridhisha.

Katika mazingira ya biashara ya miraa, kuulizwa useme ultaka nini na muuzaji, ilikuwa ni kama salamu (**Tazama mazungumzo katika Kikundi Kiini B**). Hii ni kwa sababu kuwa muuzaji alikuwa amekamilisha kuwauzia walotangulia na kwa wakati huo, msaada wake angeutoa kwako. Katika mazungumzo mengine, maamkuzi yalikuwa ya aina tofauti. Mnunuzi alipofika dukani, alimwita muuzaji kwa jina lake rasmi au la utani. Kuitwa kwa jina, ulikuwa ni kifunguzi cha mawasiliano baina ya aliyeitwa na aliyeita. Kwa mfano;

#### **Mfano 4:**

1.  $SM_N 2h$ : *Patrick Lumumba, nipe quarter*
2.  $MM_z 2h$ : *Sema askofu, wewe ni askofu kweli? Wewe imani yako ni ya pastor*
3.  $SM_N 2h$  : *Imani kidogo eeh*
4.  $SM_N 2h$  : *Hii imani ya mapastor ndio inatusumbua sana...*

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo h Uk. 122)**

Katika mfano 4,  $SM_N 2h$  anamwita muuzaji Patrick Lumumba. Kiasili jina lake lilikuwa ni Patrick lakini kutokana na ulumbi na umaarufu wa Patrick Lumumba anayejulikana hapa nchini Kenya, aliinika tu. Ijapokuwa halikuwa ndilo jina lake rasmi,  $MM_z 2h$  aliinika na kugundua utani aliokuwa nao  $SM_N 2h$ . Ndiposa katika kauli ya pili,  $MM_z 2h$  alimwita ‘askofu’ na kisha kuendelea kusema kuwa alikuwa na imani ndogo ndogo. Kwa hivyo, kutokana na uhafifu wa imani wa  $SM_N 2h$ ,  $MM_z 2h$  alitarajia kuwa  $SM_N 2h$  angetoa pesa kidogo kwa miraa aliyotaka kuinunua. Ufunguzi kati ya washiriki hawa wawili  $SM_N 2h$  na  $MM_z 2h$  ni wa kikaribu sana ndiposa kuna kutaniana. Ni kinaya kuwa anamwita askofu kwani mwislamu hawezu kuwa askofu. Uhusiano wa kikaribu baina ya washiriki ndio unaoeleza aina hii ya ufunguzi wa mawasiliano kati yao. Ukaribu huu kati ya waweza kuwa umeletwa na uteja wa mara nyingi wa  $SM_N 2h$  katika duka la  $MM_z 2h$ .

## **Mfano 5:**

1. F<sub>S</sub>1a: xxxxx...
2. M<sub>m</sub>1a: eeh
3. S<sub>m</sub>2a: xxxxx!mambo
4. S<sub>m</sub>6a xxxxx!
5. M<sub>m</sub>3a: Sema boss

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 110)**

Katika **mfano 5**, kauli 1,3 na 4 muuzaji anitwa kwa jina lake na wanunuzi ambao wanamwita kwa kusudi la kuteka nadhari yake ili aanze mazungumzo nao. Kuita kwa jina la muuzaji katika mfano huu ni vifunguzi vyta mazungumzo.

Maoni ya wanakikundi kuhusu salamu na ufunguzi wa mazungumzo kati ya washiriki wa biashara ya miraa yalikuwa ni haya.

MTF: Je, kuna wateja hufika dukani na kusema sasa, mambo, nuizie?

MM001B: Hakuna. Labda wale wamekuja kununua miraa na wanataka deni tu.

SM001B: Eeeh

MTF: So ukiona mtu anakuja kununua na kuanza kukwambia ooh sasa, poa, umekuwaje

SM003B: Lakini iko, iko kidogo wenyewe wanakuja na kukusalimia kwa upole na wanakupigisha stori na hata wanunua miraa bado. Iko.

MM002B: Lakini unajua eti huwa inalingana na watu kulingana na vile ameingia.

MM003B: Kama mtu ameingia akiwa *rude*, itabidi apelekwe hivyo hivyo.

SM003B: Iko kama 10% wenyewe wanakuja na upole, wanakuuliza mambo, habari za watoto, na wanakugotesha tu, iko..

MM003B: Lakini wengi wao wale wanakuja na salamu na *stori* nydingi wanakuja kukopa au pesa yao haitoshi.

MTF: Kwa hivyo ukiona mtu amekuja na *stori* nydingi, wewe kama muuzaji unaanza kufikiria kuhusu kukopwa...

### **(Rejelea kiambatisho cha Kikundi Kiini B Uk. 141)**

Kutokana na mfano huu, washiriki wanahisi kwamba asilimia 10% tu ya wanunuzi ndio hufika dukani na kutoa salamu zilizo halisi. Asilimia 90% ya wanunuzi wengine wanapofika na kuanza kutoa salamu na kumjulia muuzaji hali yake na ile ya familia yao, ilikuwa ni njama tu ya kutaka kupata mkopo kwani fulusi zao za kununulia miraa huenda hazitoshi. Ujuzi wa kutambua ujanja wa salamu ambazo hutolewa na wanunuzi ndizo huenda zimechochea wauzaji na wanunuzi kutofungua mazungumzo yao kwa salamu au maamkuzi ya aina yoyote, kama tutakavyoona baadaye. Mazungumzo yalianza katika upeo ambapo ni kupewa bidhaa na kuanza kuikagua pasi hatu kuzungumza mara nyingine.

#### **4.2.2 Ubadilishanaji Zamu**

Kulingana na Jefferson (1986) na Schegloff (1996), zamu ni usemi uliokamilika unaotolewa na mshiriki mmoja wa mazungumzo ambao haujakatizwa na mshiriki yule mwingine. Kwa hivyo, katika mazungumzo kuna msururu wa washiriki kutoa semi zao mmoja baada ya mwingine. Hizi ndizo waliziita vijonzi. Vijonzi ni zamu mbili ambazo hupaswa kuandamana, hivi kwamba sehemu ya kwanza inapotokea hulazimisha kuwepo kwa sehemu ya pili. Mifano ya vijonzi ni kama vile, salamu-kiitikio, maombikusaidiwa au kukataliwa, mwaliko- kukubalika au kukataliwa (Schegloff & Sacks, 1973). Katika biashara ya miraa pia, kuna zamu ambazo zilitokea baina ya wauzaji na wanunuzi. Zamu hizi zinatokea kwa muundo mbalimbali kama ifuatavyo:

#### **Mfano 6:**

1. Mm<sub>z</sub>7c: unataka karatasi ngapi leo?
2. Sm<sub>N</sub>10c: Hapana leo mimi sitaki nyingi. Mimi nataka karatasi moja tu.
3. Mm<sub>z</sub>7c: shika. ((Akimkabidhi sm<sub>n</sub>10 ajifungie kifurushi chake cha miraa mwenyewe))
4. Sm<sub>N</sub>10c: Hapana. Wewe ndio utajua utafunga vipi. Mimi sijui.
5. Mm<sub>z</sub>7c: wewe ndio utazoea kujifungia sasa
6. Sm<sub>N</sub>10c: eeh. Mimi nitazoea kuzishikashika. nitazoea. Next time mimi nitajifungia mwenyewe. Hakuna haja nikusumbue mimi daddy.. nitazoea tu.

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo c Uk. 115)**

Katika **mfano 6**, tunaona kuwa kauli 1, 3, 5 zinatolewa na M<sub>mz</sub>7. Na kauli 2, 4, 6 kutolewa na S<sub>mN</sub>10c. Kama Yule (1972) anavyoeleza, mazungumzo huchukua muundo maalumu ambapo mzungumzaji wa kwanza hutoa kauli yake, kisha mzungumzaji wa pili 2, kisha mzungumzaji 1 tena na mzungumzaji 2 tena na muundo huo hurudiwa kila mara. Mfano wa 6, unakubaliana na mawazo ya (Yule k.h.j.). Maelezo yanayoweza kutolewa ni kuwa, hakukuwa na wateja wengi katika wakati huo hivyo muuzaji 7 alikuwa na wakati mzuri tu wa kumsikiliza mnunuzi 10, au walikuwa marafiki hivi kwamba aliona ni vyema amhudumie vizuri kwani katika kauli 6 anamuuliza “unataka karatasi ngapi leo.” Hiyo ni ishara kwamba alikuwa mteja wake wa kila siku. Pia, huenda muuzaji alikuwa amechoka kwa hivyo hakutaka kelele nyingi. Sababu nyingine yaweza kuwa alikuwa amemaliza miraa na mteja S<sub>mN</sub>10c, alikuwa baadhi ya wateja wa mwisho kabla ya kulifunga duka lake.

Pia kuna zamu ambazo hutokea ambapo mnunuzi anaomba na maombi yake kukataliwa.

#### **Mfano 7:**

1. M<sub>mz</sub>5b: *wariah hii ni pesa ngapi?*
2. S<sub>mN</sub>8b: [Nipatie mimi miraa yangu
3. M<sub>mz</sub>5b: [nikupatie nini? nikupatie miraa?, hii ni pesa ngapi?
4. : unaota ama?
5. : [wewe uko na wazimu?

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 112)**

Kutokana na **mfano 7**, muuzaji alikataa kumuuzia kwa sababu pesa zake ni kidogo au kila alipokuja dukani aliwasumbua wauzaji. Ndipo M<sub>mz</sub>5 alimuuliza maswali ya balagha katika kauli 3,4 na 5. Maombi ya wanunuzi yaliweza kukataliwa kwa wateja ambao walizoea kuwasumbua wauzaji au kila mara kutaka kuuziwa bei ya chini zaidi ilhali miraa waliyotaka ni ghali. Maelezo haya yalipatikana katika maelezo ya muuzaji M<sub>mz</sub>1

### Mfano 8:

1. sm<sub>N</sub>7a:harakisha please wee..
2. sm<sub>N</sub>8a: leta shamba ya maana ...shamba ya maana leta..
3. :leta....leta miraa wariah lete miraa
4. Sm<sub>Z</sub>2a: miraa mimi siuzi..
5. Mm<sub>Z</sub>1a: Maongezi ya kando ((akimzungumzia Mm<sub>Z</sub>2 kwa lugha yake ya kwanza)) (*nukwona kinya ##### atikwenda umwenderia... gutiri ukwenda umwona.kuru ii guti muntu uticie waa bwake. Ontu igoro naracokerie miraa ugoro na akugite ekirwe. (Unaona hata ##### hataki kumuuzia? Kila mtu hataki kumuuzia kwa sababu ya ujinga wake. Huyu ni mbwa huyu, hakuna mtu anataka kumwona. Kama jana alirejesha miraa masaa ya usiku na alikuwa amesema awekewe)*)

### (Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)

Wauzaji Mm<sub>Z</sub>1a, Mm<sub>Z</sub>2a na Sm<sub>Z</sub>2a walimweleza kuwa hawakuwa wakiuza miraa ilhali walikuwa dukani pale kuwauzia watu bidhaa hiyo. Katika kauli ya 5, Mm<sub>Z</sub>1a alieleza kuwa mteja huyo husumbua na kwamba hakuna mtu hutaka kumwona. Maelezo hayo yalionyesha kuwa ijapokuwa aliiona miraa na wale waliofika dukani baada yake walipata huduma ilhali yeye aliambiwa kuwa hawakuwa wakiuza miraa au hakukuwepo na miraa.

Zamu zilizingatiwa na washiriki ijapokuwa si kwa umakini sana kwa sababu watu wengi walifika dukani na kuhitaji huduma za wauzaji wachache ambao walikuwa dukani. Iwapo ulifika pale na ‘hadithi’ nyingi ilhali biashara ilikuwa ‘imeshika’ ilibidi ufukuzwe ili uwaondokee wengine wanunue na kuuziwa kwani hadithi zako nyingi zingetatiza maelewano baina ya muuzaji na wateja wake **(Rejelea mjadala katika Kikundi Kiini B Uk. 140)**

Kulingana na matokeo ya utafiti, ilibainika kuwa mazungumzo katika biashara ya miraa huchukua mipangilio mbalimbali ya ubadilishaji zamu. Mipangilio hiyo ilibadilika kutegemea wanunuvi waliofika dukani kwa wakati mmoja. Iwapo wanunuvi waliofika dukani ni wengi (kama sita), na walihitaji msaada wa muuzaji mmoja au wawili, basi palikuwa na ukatanaji kalima mwingi na zamu za mnunuzi mmoja zilibaki zimesubirishwa hadi pale ambapo mnunuzi mwingine alihudumiwa kwanza, kisha

zamu yake kurejelewa. Hatimaye, wanunuzi wote walishughulikiwa. Mpangilio huo wa zamu ulionekana kuwa changamano mno, na ultokana na udharura wa kuuza na kununua katika biashara ya miraa kutokana na hali ya kuharibika haraka kwa bidhaa hiyo. Ingawa kusubirishwa kwa zamu kungeonekana kama sababu ya kuonyesha ujeuri kwa wanunuzi, washiriki walielewa kwamba wasingeweza kuhudumiwa wote kwa wakati mmoja na hivyo basi walikubali kusubiri pasipo na kuudhika. Mpangilio wa moja kwa moja wa zamu pia ulidhihirika pale ambapo muuzaji hakuwa na wanunuzi wengi hivyo akawa na nafasi ya kuwasiliana na mteja wake kwa utaratibu. Jukwaa la mazungumzo lilimilikiwa na kila mnunuzi. Hii ndiyo sababu kuu iliyomfanya kila mnunuzi kufika na kuomba huduma bila kutambua uwepo wa waliofika mbele yake ambao walikuwa wanapata huduma. Matokeo haya yanakubaliana na yale ya awali aliyofanya (Edelsky, 1981).

#### **4.2.3 Ukataji Kalima**

Kulingana na Jefferson na Schegloff (k.h.j.), zamu ni usemi uliokamilika unaotolewa na mshiriki mmoja wa mazungumzo ambao haujakatizwa na mshiriki yule mwingine. Sacks (k.h.j.), anaeleza kuwa mazungumzo ya kawaida katika jamii huchukua muundo maalumu wa ubadilishanaji zamu, ambapo mmoja kati ya washiriki huwa na msukumo fulani wa kuanzisha mazungumzo. Kulingana na Sacks, mazungumzo hupaswa kuwa yenye mpangilio. Kwamba, mtu asizungumze kabla ya zamu yake ya kuzungumza ama huku mwenzake akizungumza hali ambayo huzua ukataji kalima. Alieleza kuwa ukataji kalima hutatiza mawasiliano.

Katika mazungumzo ya wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa kwa mfano, watu wengi walipatikana wakizungumza kwa wakati sawa. Mazungumzo yanayoshirikisha jinsia ya kiume pekee, Coates (2013) anafafanua kuwa huwa yamesheheni kukatizana kalima. Ukatizanaji kalima huu hutokana na hali ya kila mwanamume mshiriki wa uzungumzi kuwa na ubabe (Meinhof, 1997). Ubabe huo ndio humsukuma kutaka kuzungumza kabla ya mwenzake, kwani iwapo utamruhusu mwenzako kuzungumza yako, basi ni ishara ya unyonge. Katika mazungumzo ya biashara ya miraa kama mtarifi atakavyodhihirisha kwa mifano, wanunuzi na wauzaji walikatikazana kalima.

## Mfano 9,

1. ((SM<sub>N</sub>13e na SM<sub>N</sub>14e wakizungumza kwa kisomali))
2. SM<sub>N</sub>13e : leta gazeti((anajifungia mwenyewe miraa yake kisha anataka kuondoka ))
3. SM<sub>N</sub>14e:mimi [nifungie] yangu
4. Mm<sub>Z</sub>9e : [unaenda wapi] wewe Kwenda
5. SM<sub>N</sub>13e: [Gitonga
6. MM<sub>Z</sub>9e eeh]
7. SM<sub>N</sub>13e: ni [mbili amechukua] Quarter [mbili Moja na moja
8. MM<sub>Z</sub>9e : [wewe wacha haramu wewe]
9. SM<sub>N</sub>13e: aa wewe wacha wewe bwana
10. SM<sub>N</sub>14e: hii [ni halali bwana]
11. SM<sub>N</sub>13e: hii ni halali angalia..
12. MM<sub>Z</sub>9e: ((akimkaripia SM<sub>N</sub>14e)) [wee! kaa huko bwana..
13. : Kaa na miraa mbali huko ]sawa?

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 117)**

Katika **mfano 9**, SM<sub>N</sub>13e na SM<sub>N</sub>14e baada ya kuuziwa, SM<sub>N</sub>13e anataka kujifungia miraa mwenyewe kabla ya Mm<sub>Z</sub>9e aone iwapo kiwango cha miraa alichotaka kujifungia kilikuwa sawa- yaani iwapo SM<sub>N</sub>13e hakuwa amejifunga kiwango kikubwa kuliko ile aliyoilipia. Kwa hivyo, katika kauli ya 4 Mm<sub>Z</sub>9e anabidika kumuuliza iwapo anataka kwenda wapi haraka hivyo kabla ya Mm<sub>Z</sub>9e kudhibitisha kiwango alichokuwa amefunga SM<sub>N</sub>13e. Katika kauli zao, wanakatizana kauli kwa nia ya kutaka kujua iwapo miraa ya kiwango kinachofaa imechukuliwa na wanunuvi ni sawa.

Wakati SM<sub>N</sub>14e anajaribu kujiingiza katika mazungumzo yaliyoshirikisha Mm<sub>Z</sub>9e na SM<sub>N</sub>13e, katika kauli ya 12, Mm<sub>Z</sub>9e anamkaripia kwani yuko katika kazi yake na lengo lake kuu ni kuuza na wala si kuacha wateja wakachukua miraa iliyo mingi. Kuhusu ukataji kalima, wanakikundi walikuwa na haya ya kusema,

MTF: Je kuhusu muundo na hasa ukataji kalima, nimegundua kuwa watu wengi huongea kwa wakati mmoja na hakuna mtu humwacha mwingine aongee kwanza. Je hiyo *system* ya kuongea mmoja kwa mmoja iko kweli? Juu mimi nimeona watu hufanya *interruption* sana . Je nyinyi mnaonaje kuhusu hilo?

MM003B:Eeh iko

MM001B: **Unajua unaweza ukasema hivyo, kwa maana huenda umekuja ile peak hours. Sasa wewe umekuja kupeana stori nyingi badala ya kusema ile miraa unataka upewe na ukianza kupeana story nyingi unaweza ukaambiwa sema kile unataka**

**ama uende. Hasa wakati biashra imeshika sana na kuna watu wengine wanataka kuuziwa na wewe uko hapo na maneno mingi mingi. Lazima ukatizwe.**

**SM002B: Ee lazima ukatizwe kwa sababu kila mtu anataka kuuziwa haraka haraka ili aende kuanza starehe yake mapema.**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 136)**

Starehe katika muktadha huu ni kuenda kutafuna miraa yake mapema. Kwa hivyo ule ukataji kalima unatokana na haraka na uharibikaji wa miraa kama alivyoeleza Carrier (2005). Kulingana na Carrier, shughuli zote zinazozingira bidhaa ya miraa hufanyika kwa upesi kwani miraa huwa na kemikali *Cathinone* inayoharibika haraka pindi mmea wenyewe unapotolewa kwenye mti wa miraa. Uharibikaji huu wa miraa basi huenda ndicho chanzo cha wateja wafikapo dukani na kuzungumza kwa wakati sawa kwani kila mmoja wao hutaka kuhudumiwa haraka.

Katika **mfano 10**, wanunuzi watatu walifika dukani kwa wakati sawa. Wote wanamwita muuzaji mmoja na wote wanahitaji huduma kutoka kwake. Kwa hivyo mazungumzo yao yanaonekana kama ifuatavyo:

**Mfano 10,**

6.  $F_{S1a}$ : xxxx
7.  $M_{m1a}$ : eeh
8.  $S_{m2a}$ : xxxx!mambo
9.  $S_{m6a}$ : xxxxx!
10.  $M_{m3a}$ : Sema boss...

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Katika **mfano 10**, wanunuzi  $F_{S1a}$ ,  $S_{m2a}$  na  $S_{m6a}$  walitaka huduma kutoka kwa muuzaji  $M_{m1a}$ . Kwa hivyo, ili mazungumzo yawe na mpangilio,  $M_{m1a}$  alimwitika mnunuzi aliywewita kwanza  $F_{S1a}$  na kisha akanyamaza alipoitwa na  $S_{m2a}$  na  $S_{m6a}$  kwanza aliwa anashughulikia mteja wake wa kwanza  $F_{S1a}$ . Kwa kuwa muuzaji sharti awape wateja wake huduma nzuri na ya kuwardhisha Walya (1995), ilibidi muuzaji mwenzake  $M_{m3a}$ , aingilie kati ili wateja  $S_{m2a}$  na  $S_{m6a}$  wasione kana kwamba wanapuuzwa. Kuna dhihirisho la ukataji kalima baina ya wazungumzaji katika soko la miraa kwani wengi wao huenda dukani wakiwa na haja ya kuhudumiwa pindi tu wanapofika pale. Kwa mfano, kauli yake  $M_{m3a}$ , aliwa ikatize uzungumzi uliokuwa ukiendelea baina ya kauli 6 na 7. Hata hivyo nia yao

haikuwa kukata kalima, bali uharaka wa kutaka huduma ndio uliowalazimisha kukatiza kalima.

Cha msingi mno kuhusu miraa ni uharibikaji wake wa haraka. Kemikali *Cathinone* hubadilika na kuwa cathine pindi tu inapotolewa mtini. Ijapokuwa kuna ile ambayo hukaushwa na kuuzwa nchini Ethiopia, hapa nchini watafunaji hupendelea kuipata miraa yao ikiwa freshi. Uharibikaji huo wa miraa ndio huathiri biashara ya miraa na vivyo hivyo lugha inayotumika kwenye biashara huathirika (Carrier, 2007).

#### 4.2.4 Urekebishaji

Urekebishaji ni hali ambapo mzungumzaji hugundua makosa katika usemi wake au wa mwenzake na kuchukua jukumu la kujikosoa au kumrekebisha mwenzake. Kulingana na Grundy (2000), urekebishaji au ufanuzi wa kauli aliyoitoa msemaji, huwa ni mojawapo ya mikakati ya unyenyekevu ambayo hutumiwa na wazungumzaji. Urekebishaji huweza kufanywa na mzungumzaji mwenyewe baada ya kugundua hitilafu katika usemi wake, au ukafanywa na mzungumzaji wa pili baada ya mgongano wa kauli za wazungumzaji wawili. Katika mazungumzo haya tulichunguza baadhi ya urekebishaji baina ya wazungumzaji na kupata urekebishaji katika mazungumzo yafuatayo;

#### Mfano 11,

1. SM<sub>Z</sub>lf: Kitambo si amenunua kwako?
2. :Wee kwenda huko wewe.
3. :mkundu yako>>
4. Sm<sub>Z</sub>lf: Hii ni biashara ee..
5. MM<sub>N</sub>lf : ((Mnunuzi mwingine akiingia)) ((Akicheka)) .. hata hajalipa
6. Sm<sub>Z</sub>lf : aa xxxxx
7. MM<sub>N</sub>lf: Ikwega (salama)
8. SM<sub>N</sub>lf: fyam (salama)
9. Mm<sub>N</sub>lf: Hata hii inatosha ((karatasi ya kufungia miraa))
10. Sm<sub>Z</sub>lf: Ni ya watu tofauti
11. MM<sub>N</sub>lf: Weka yote tu kwa hii moja
12. :Ninaweza nikewithdraw?
13. Sm<sub>Z</sub>lf : Ee
14. MM<sub>N</sub>lf : Mbona hukuwa unanikumbusha wewe...
15. Sm<sub>Z</sub>lf : Ee ni sawa sawa baba. Asante. Welcome lakini sawa?
16. : Karibu karibu ee baba ee ...
17. : Sindio kila siku mimi nakuona...ee
18. : xxxxxx ni Mutonyakwe (ndugu wa kiume)mimi ni msomali sawa?

19. :Sawa sawa mukuru (Mzee) ?
20. MM<sub>N1f</sub>: Ee?
21. Smz1f: Gikundi kwako ni mutanonyakwe (ndugu wa kiume)mimi ni msomali ee
22. : yeye ndiye anasema hata ukikata hamsini, unapata hata risasi...
23. : na hata si wewe peke yako, miraa inauzwa hivyo kila mahali sivyo?
24. :Eeh kweli\*2
25. :ee sawasawa baba
26. :aa Mimi hata sijakuongelesha mbaya
27. :Sawa?  
:ee sawa sawa boss ((MM<sub>N1f</sub> anaondoka))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo f Uk. 119-120)**

Katika kauli 4 ya **mfano 11**, Smz1f anamkumbusha kuwa aliyokuwa akiifanya ni biashara. Hii ilikuwa njia moja ya kumtaka asiichezee kazi yake kwa kutolipa miraa aliyouziwa. Pia anamkumbusha katika kauli ya 18 na 21 kuwa yeye alikuwa anafanya kazi ambayo ametumwa na kuwa hawezি aksa bei ya chini. Baada ya kugundua kuwa alidhuru hisia za mwenzake, ndipo alipofafanua na pia kuomba msamaha. Katika kauli 26 na 27, Smz1f alimuuliza MM<sub>N1f</sub> iwapo ‘alimwonglesha mbaya’ na iwapo ilikuwa vile, basi amsamehe.

Urekebishaji unaonekana pia anapomweleza kuwa yeye ni msomali na kuwa ambaye anamiliki miraa alikuwa ndugu ya mnunuzi (yaani ni Mmeru mwenzake) na wala siyo ndugu yake yeye (kwani yeye ni Msomali). Kwa hivyo si kwamba alikataa kumpunguzia bei ya miraa kwa sababu ya kabilia lake (msomali) bali ni kwa sababu ya masharti ambayo alikuwa amepewa na mmeru aliyemiliki miraa hiyo.

**Mfano 12,**

18. Smz1f : xxxxxx ni Mutonyakwe (ndugu wa kiume)mimi ni msomali sawa?
19. :Sawa sawa mukuru (Mzee) ?
20. MM<sub>N1f</sub>: Ee?
21. Smz1f: xxxx kwako ni mutanonyakwe (ndugu wa kiume)mimi ni msomali ee
22. : yeye ndiye anasema hata ukikata hamsini, unapata hata risasi...
23. : na hata si wewe peke yako, miraa inauzwa hivyo kila mahali sivyo?

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo f Uk. 120)**

Pia, Smz1f aliendelea kumweleza MM<sub>N</sub>1f kuwa si yeye pekee aliyeuziwa vile bali ni kila mteja aliyefika kununua. Urekebishaji huu ulifanyika mradi kumridhisha ambaye alihisi ni kama kwamba alibaguliwa. Urekebishaji pia, ulijitokeza pale ambapo wazungumzaji wawili walikatana kauli kutokana na kuzungumza katika mpumuo mmoja. Katika tukio kama hili, mmoja wao aliyegundua kwanza, alirudia usemi wake. Katika **mfano 13**, MM<sub>Z</sub>9e na SM<sub>N</sub>13e wanakatana kalima kwani inaonekana kuwa hawakuelewana kuhusu bei na aina ya miraa ambayo SM<sub>N</sub>13e alitaka kuinunua.

### **Mfano 13,**

1. SM<sub>N</sub>14e: xxxxxxxx
2. MM<sub>Z</sub>9e: mmmm
3. SM<sub>N</sub>13e: Mimi bado ninakungoja.../
4. MM<sub>Z</sub>9e:/Unaningojea kwa nini?
5. SM<sub>N</sub>13e: Ili miraa mzuri unipatie
6. MM<sub>Z</sub>9e: Na hiyo uko nayo ni nini?
7. SM<sub>N</sub>13e: Ebu pia wewe shika uangalie hata wewe
8. MM<sub>Z</sub>9e: Hiyo ni miraa ya maana hata mimi najua
9. SM<sub>N</sub>13e: Ebu shika angalia// hata wewe
10. MM<sub>Z</sub>9e: //Naangalia nini
11. SM<sub>N</sub>13e: Wewe nduqu yanqu,... angalia wewe mwenyewe
12. : Hata wewe mwenyewe hukuli// hii hata nikikupatia
13. MM<sub>Z</sub>9e: sikuli kwa nini miraa yangu yote

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 118)**

Katika kauli 11 na 12, SM<sub>N</sub>13e anamweleza kuwa hiyo miraa si mizuri na hata akimpa yeye MM<sub>Z</sub>9e hatatafunu. Hata hivyo, MM<sub>Z</sub>9e anamrekebisha na kumweleza katika kauli 13 kuwa yeye ataitafuna yote akijapewa kwani ni yake yote. Urekebishaji unaofanya na MM<sub>Z</sub>9e ni mojawapo ya mikakati tu ya lugha ya biashara, ambapo muuzaji wa bidhaa atazisifu bidhaa zake zote mbele ya mnunuzi.

### **4.2.5 Ufungaji wa Mazungumzo**

Kama alivyoeleza Schegloff na Sacks (k.h.j.), mazungumzo huwa hayakamiliki tu, bali wanaoshiriki hushirikiana katika kuyahitimisha. Liddicoat (2000), akidondoa mifano kutoka kwa mazungumzo na tafiti zilizofanywa awali, aliorodhesha kadri mbinu tano za kuonyesha namna hufungwa na wa shiriki wa uzungumzi. Nazo ni kama vile; maagano, shukrani, ahadi za kuzidi kuzungumza baadaye, kukubaliana kuwa wakamilishe uzungumzi na mmoja wa waungumzaji kuomba kuondoka. Katika

muktadha wa biashara ya miraa, wazungumzaji walizingatia mbinu zifuatazo kuyakamilisha mazungumzo yao.

#### **Mfano 14,**

1. SM<sub>N</sub>1g: Xxxxxx ni hivyo? Ni xxxxxxxxx?
2. MM<sub>Z</sub>1g: Wee hapana nani anaitwa xxxxxx hiyo pesa imeenda kwa kikuyu wewe bwana
3. SM<sub>N</sub>1g: itarudi tu. Sawa lakini?
4. MM<sub>Z</sub>1g: Eeh ni sawa. Tutaonana siku ingine Mungu akipenda eeh
5. SM<sub>N</sub>1g: Eeh sawa( (huku akiondoka) )

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 121)**

Katika **mfano 14**, mazungumzo haya yanaanza kukamilika baada ya SM<sub>N</sub>1g kulipia bidhaa aliyochagua kwa kumtumia MM<sub>Z</sub>1g pesa kwenye simu. Katika kauli 3, SM<sub>N</sub>1g anasema, “sawa lakini?” Swali hili linaonyesha kuwa alihitaji idhini ya kuondoka kutoka kwa MM<sub>Z</sub>1g, ambaye alimwitikia katika kauli ya 4 na wakawa wamekubaliana. Fauka ya makubaliano yao, MM<sub>Z</sub>1g anazidi kumwahidi kuwa wataonana siku nyininge Mungu akipenda. Kauli ya 4 inamlazimu SM<sub>N</sub>1g kukubaliana na MM<sub>Z</sub>1g kisha anaondoka.

Katika mazungumzo mengine, muuzaji na mnunuzi walipokosa kukubaliana kuhusu bei ya miraa, mnunuzi aliondoka tu baada ya kuikagua kagua miraa na kukosa iliyo mpendeza.

Katika **mfano 15** ufuatao, sm<sub>N</sub>7a alitaka kuuziwa na miraa. Hata hivyo, anaigusa gusa na kuikagua kagua jambo linalomkasirisha mm<sub>Z</sub>1a ambaye katika kauli 5 anamrejelea sm<sub>N</sub>7a kama mjinga. Kubadilisha msimbo kwa mm<sub>Z</sub>1a katika kauli 4, ndiko kunakotufahamisha kuwa sm<sub>N</sub>7a hakuwa mteja wake wa siku nydingi.

#### **Mfano 15,**

1. sm<sub>N</sub>7a: wariah hakuna miraa? lete miraa na harakisha  
*please* kuna kazi nydingi sana leta
2. Mm<sub>Z</sub>3a: shika.. do you want this? (Unataka hii?)
3. mm<sub>Z</sub>1a: ka aregere kugura na aguraa uju? (Kwani amekataa kununua pale huwa ananunua huko 12?)
4. Mm<sub>Z</sub>3a: uriku? (Nani?)
5. mm<sub>Z</sub>1a: kiaa ki kiwitia miraa kii.. (mjinga huyu anayeitisha miraa )
6. :Aukinya njira aitaa ii? (Amekasirika akaenda eh?)

((sm<sub>N</sub>7a baada ya kukagua miraa kwa wakati mrefu anaondoka bila kuinunua))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Mm<sub>z</sub>3a anauliza katika kauli 3 mbona sm<sub>N</sub>7a hakuwa ananunua huko 12<sup>th</sup> ambako yeze alizoea kununua. sm<sub>N</sub>7a anagundua kuwa wauzaji hawana haraka ya kumhudumia kama alivyopenda na ndipo anaondoka bila kuaga au kusema neno.

**Mfano 16;**

1. Sm<sub>N</sub>9b: [ Shurba kubwa basi uzia ... tafadhali ]
2. Mm<sub>z</sub>5b : [ Sasa unaongea nini tena xxxxxx na wewe ]
3. Sm<sub>N</sub>9b: shurba kubwa nataka mimi.. tafadhali
4. Mm<sub>z</sub>5b: munenkere kubwa (Mpe hyo kubwa basi)  
:Lete ((akichukua pesa))
5. Sm<sub>N</sub>9b: Nataka hiyo uko nayo wewe. ((akipewa kisha anakagua kagua ))leta ile umenipatia kwanza.
6. : Hakuna kitu unaongeza?
7. Mm<sub>z</sub>5b : Bwana tuheshimiane Kuso na wewe bwana (ananyamaza na kuondoka)
8. Mm<sub>z</sub>6b: uyu ena thina imbia huju..kwi ntuku ancumburire mwaka ndatura ndamutia ni (huyu ana tamaa sana. Kuna siku alinisumbua hadi nikatoka mimi nikamwacha)

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 112)**

Katika **mfano 16** pia, Sm<sub>N</sub>9b anaondoka bila kuaga baada ya kupewa onyo kali na Mm<sub>z</sub>5b ambaye aliona kuwa alikuwa anamsumbuwa kwa kumwitisha miraa anakagua, anaitisha mingine vivyo hivyo. Jambo ambalo lilimkera Mm<sub>z</sub>5b .

Mazungumzo mengine, yalitamatishwa kwa kukubaliana baina ya muuzaji na mnunuzi. Kwa mfano, katika **mfano 17** ufuatao, Mm<sub>z</sub>1j na SM<sub>N</sub>1j walikubaliana kukamilisha mazungumzo yao kwa kusema, “baadaye.”

**Mfano 17,**

1. Mm<sub>z</sub>1j :baadaye baadaye..((akimkabidhi SM<sub>N</sub>1 miraa yake))
2. SM<sub>N</sub>1j: Na uache wasiwasi wewe.
3. :Sawa baadaye baadaye mzae. ((SM<sub>N</sub>1j anaondoka))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo j Uk. 122)**

Kuhusu utamatishaji wa mazungumzo katika biashara ya miraa, inadhihirika kuwa watafiti walibainisha kuwa washiriki hawakutoa maneno mwafaka ya kushukuru kama vile asante baada ya huduma. Kinyume na kawaida ya maongezi mengine ya miktadha ya kijamii, Schegloff na wenzake (1974), mazungumzo ya biashara ya miraa yalikamilika baada ya kulipia bidhaa na washiriki kukubaliana tu kukamilisha

mazungumzo yao kwa kusema ‘sawa.’ Pia, waliweka ahadi za kukutana baadaye (labda kesho yake) ambapo wangenunua miraa tena. Kuhusu utamatishaji wa mazungumzo ya biashara ya miraa wanakikundi walikuwa na haya ya kusema.

1. Mtf: je kuna maneno ambayo unaweza ukataja ya unyenyekevu katika biashara ya miraa?
2. JIBU LA WENGI: ((kicheko)) aa hakuna...
3. MM002B: si labda matusi..
4. (( kicheko cha wote))
5. MM003B: ee labda matusi. Hakuna hata kusema asante..
6. FM003B: ee matusi ndio nyingi. Asante ya nini.. wengine wanakuwa sawa mkundu.
7. SM004B: Asante ya nini, na hakuna tafadhali. Tafadhali ya nini? Ni leta miraa kwa sababu hakuna kuomba.

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 134)**

Kutokana na yaliyojadiliwa katika sehemu hii, muundo wa mazungumzo katika ununuzi wa miraa huwa huu; mnu

nuzi alifika dukani, kuomba miraa, kuikagua, kujadili bei na kukubaliana na kisha kuilipia na kuondoka. Imani kwamba ‘pesa ni yangu’ na ‘ni mimi ninanunua’ na wala ‘hakuna kuomba’ ndiyo sababu kuu ya kutotumia misamiati ya kushukuru baada ya kupata huduma. Ukataji kalima ulikuwepo kwa sababu ya uhitaji wa wanunuzi kupata huduma za haraka.

#### **4.3 Athari ya Kabilia na Jinsia kwa Muundo wa Mazungumzo mionganoni mwa Wauzaji na Wanunuzi**

Sehemu hii inashughulikia lengo la pili la utafiti huu, ambalo lilikuwa ni kutathmini namna muundo wa mazungumzo ulivyoathiriwa na kabilia na jinsia ya washiriki wa biashara ya miraa. Mtafiti alichunguza athari ya ukabilia na jinsia ya washiriki kwa muundo wa mazungumzo bila kujikita katika vijimada vya muundo kama alivyofanya katika lengo la kwanza la utafiti. Mifano ilitolewa kwa ujumla ili kuonyesha mabadiliko au mfanano wa muundo wakati lugha ilitumiwa na wanaume na wanawake katika mazingira ya biashara ya miraa. Mtafiti alishughulikia athari ya jinsia kwa muundo wa mazungumzo, kisha akaangazia athari ya ukabilia kwa muundo wa mazungumzo ya biashara ya miraa.

### **4.3.1 Jinsia na Muundo**

Kulingana na Tannen (1990) mazungumzo huchukua muundo tofauti yanapotekelezwa na kundi la wanaume au wanawake. Pia kuna utofauti wa semi zitolewazo na wanawake na vilvile wanaume katika mazungumzo yanayoshirikisha jinsia zote mbili. Tannen (1990) anatuasa kuwa wanaume na wanawake hufasiri matukio katika ulimwengu kwa njia tofauti sana. Utifauti huu wa kuutazama ulimwengu huwapelekea kutoa semi ambazo ni tofauti (Coates, 2004).

Mtafiti aliigawa mifanano na tofauti hizo katika vijisehemu viwili na kisha kutoa hitimisho kuhusu waliyobainisha kama ifuatavyo:

Katika mazungumzo wa biashara ya miraa, mazungumzo ya wanaume na wanawake yanadhihirisha utofauti wa namna fulani.

#### **4.3.1.1 Muundo wa Mazungumzo ya Wanaume katika Biashara ya Miraa**

Kulingana na Tannen (1990), wanaume hukatiza wanaume wenzao kauli kama njia ya kudumisha ubabe baina yao. Katika mfano 18, wazungumzaji walikatana kauli mmoja baada ya mwengine.

#### **Mfano 18,**

1. Sm<sub>N</sub>14e: Nataka miraa mzuri kabisa..
2. : Lete miraa mirefu
3. MM<sub>Z</sub>10e: ndio ilienda ya kwanza
4. MM<sub>Z</sub>9e : Sawa. Ooh
5. ((Sm<sub>N</sub>13e na SM<sub>N</sub>14e wakizungumza kwa kisomali))
6. SM<sub>N</sub>13e : leta gazeti((anafungiwa miraa yake kisha anaondoka))
7. SM<sub>N</sub>14e:mimi //nifungie yangu
8. Mm<sub>Z</sub>9e : unaenda wapi wewe Kwenda
9. SM<sub>N</sub>13e: xxxxxx
10. MM<sub>Z</sub>9e : eeh
11. SM<sub>N</sub>13e: ni mbili amechukua// Quarter mbili Moja na moja
12. MM<sub>Z</sub>9 e: wewe wacha haramu// wewe]
13. SM<sub>N</sub>13e: aa wewe wacha wewe bwana
14. SM<sub>N</sub>14e: //hii ni halali bwana]
15. SM<sub>N</sub>13e: hii ni halali angalia..
16. MM<sub>Z</sub>9e: ((akimkaripia SM<sub>N</sub>14)) wee kaa huko bwana..
17. : Kaa na miraa mbali huko sawa?

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 117)**

Katika **mfano 18**, SM<sub>N</sub>14e na SM<sub>N</sub>13e washiriki walikatizana kauli kila mmoja wao akijaribu kumwonyesha MM<sub>Z</sub>9e kuwa alichokisema ni cha kweli. Ukatizanaji kauli huu ni mojawapo ya sifa ambazo Tannen (k.h.j.) aliorodhesha kama idhibati ya ubabe baina

ya wanaume. Ukatizanaji kauli baina ya wanunuzi na wauzaji ilikuwa ni sifa moja iliyoonyesha athari ya jinsia ya kiume kwa uendeshaji wa mazungumzo katika biashara ya miraa. Matokeo ya utafiti huu kwa hivyo yalikubaliana na maarifa ya hapo awali ya Tannen (k.h.j.).

Mazungumzo ya wanaume pia yalisheheni ukavu (Yule 1996). Mtafiti alitambua hili kutokana na sentensi zao kudhibitiwa na kuamrisha na kutokuwepo na vinogezo vya sentensi kama zile zitolewazo na wanawake. Maarifa haya yalitokana na kauli walizotoa wanunuzi na wauzaji mtawalia.

### **Mfano 19,**

1. sm<sub>N</sub>7a: *wariah hakuna miraa?lete miraa na harakisha please kuna kazi nyingi sana leta*
2. Mm<sub>z</sub>3a: *shika.. do you want this? (Unataka hii?)*
3. mm<sub>z</sub>1a: *ka aregere kugura naa aguraa uju? (Kwani amekataa kununua pale huwa ananunua huko 12?)*
4. Mm<sub>z</sub>3a: *uriku? (Nani?)*
5. mm<sub>z</sub>1a: *kiaa ki kiwitia miraa kii.. (mjinga huyu anayeitisha miraa )*
6. : *Aukinya njira aitaa ii? (Amekasirika akaenda eh?)*
7. sm<sub>N</sub>7a: *((baada ya kukagua miraa kwa wakati mrefu anaondoka bila kuinunua))*

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Sm<sub>N</sub>7a anapofika dukani tu, ijapokuwa aliwapata wenzake wakipata huduma ile ile aliyokuwa akiitaka, hakusubiri nafasi yake ifikiwe. Alianza kwa kuwaliza katika kauli 1, “wariah hakuna miraa?lete miraa na harakisha...” Badala ya kuomba kufanyiwa huduma, yeye aliuliza iwapo hakukuwa na miraa na iwapo haikuwepo basi aelezwe haraka ili aende kwani kuna kazi nyingi alipaswa aifanye. Msamiatu aliotumia wa ‘Lete’ na ‘harakisha’ ndio ulioifanya kauli yake kuwa shurutishi. Hata hivyo, mijadala katika vikundi viini ilikanusha maoni hayo.

### **Mfano,**

1. SM002A: “Ayee si utupatie miraa mbwa wewe!” wanasema hivyo
2. MTF: Je wanapokuja kununua, huja na kutanguliza kuongea kwa salamu kama mambo-poa n.k.?
3. SM002A: Hakuna kawaida hapo, customer akikuja kwangu aanze hizo story za mambo, habari za watoto, najua hana pesa.

4. MM002A: Hiyo ni ya kuuza nguo ama vitu zingine, ama anakuja kukopa
5. SM001A: Huyo ni mtu hana shilingi, hana pesa
6. MM003A: Huyo ameamua hiyo siku kukopa
7. MM001A: Hyo mtu hana pesa. Mtu aka na pesa anakuja anagonga meza na kukwambia, Mbwa niuzie miraa, na siombi!
8. MTF: Na hiyo ndiyo kawaida yenu?
9. JIBU LA WENGI: Ee ni kawaida kabisa

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala katika Kikundi Kiini A Uk. 122)**

Wanaume pia walikatiza kauli wanawake walionunua nao kama njia mojawapo ya kuonyesha mamlaka, udhibiti na ubabe (West & Zimmerman, 1975). Katika mazungumzo baina ya jinsia mbili, mwanamke alionekana kusubiri wanaume wapewe huduma kwanza, kabla yake kupata huduma ile ile.

**Mfano 20,**

8.  $F_{S1}a$ : ..nitafutie miraa mzuri..
9.  $M_{M2}3a$ : [ai mimi sina miraa nyiningine mama.]
10.  $M_{M2}1a$ : [akizungumza kwa kimeru..rekana na kamuka kaa ka nthu kaa( achana na haka kamama kamwenda wazimu haka)]
11.  $S_{M6}a$ : tafuta mamiti mzuri. Leta mamiti..
12.  $S_{M7}a$  : madam songa weee
13. \_\_\_\_\_ :[leta na harakisha please
14. :wariah hakuna miraa?lete miraa na harakisha please kuna kazi nyangi sana leta
15. :wee madam songa weee ((akimzungumzia  $F_{S1}$ ))
16. :harakisha please wee..
17.  $S_{M8}a$ : leta shamba ya maana ...shamba ya maana leta..
18. :leta....leta miraa wariah lete miraa
19.  $S_{M2}a$ : miraa mimi siuzi..

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)**

Ijapokuwa  $S_{M7}a$ , alimpata  $F_{S1}a$  dukani alimwambia, “madam songa weee” ili auziwe kwanza, na hatumwonii  $F_{S1}a$  akinung’ unika wala kuikaidi amri ya kuambiwa asonge.

Pia,  $S_{M8}a$  anapofika dukani, anaitisha miraa yake bila kuwajali waliokuwa hapo awali. Huyo ni pamoja na  $F_{S1}a$  ambaye sasa ingembidi asubiri watu wawili wapewe huduma kabla yake.

#### **4.3.1.2 Muundo wa Mazungumzo ya Wanawake katika Biashara ya Mira**

Je, wanawake huzungumza kwa namna iliyotofauti au inayolingana na wanaume?

Mtafiti alilitathmini swali hili kwa kuzingatia mazungumzo ya biashara ya miraa.

Katika mazungumzo ya wanawake katika biashara ya miraa, mtafiti alibainisha yafuatayo; Mwanamke alipofika dukani hakuwa anafahamu miraa iliyomizuri kama wanaume wenza. Hivyo yeye anasema apewe miraa ya green ilhali wanaume wanaonunua husema miraa kwa jina miraa ambayo wanataka.

#### **Mfano 21,**

1. Fs<sub>N</sub>1a: Niuzie miraa wewe
2. Mm<sub>z</sub>1a: [Unataka nini wewe..  
: ((ka unenkerere shoka ii yite bwana))..shika umpe  
shoga huyu aende bwana..
3. Mm<sub>z</sub>3a: aa hapana ombaa..
4. Fs<sub>N</sub>1a: Pande gani.. niuzie miraa wewe
5. Fs<sub>N</sub>1a: sitaki hiyo, nataka rangi ya hii...
6. Mm<sub>z</sub>3a: [Hautaki rangi ya hiyo... unataka rangi ya ...  
Fs<sub>N</sub>1a: nataka rangi ya green..
7. Mm<sub>z</sub>3a: Unataka green? Green (nipee nydingine ya green-  
akimzungumzia mm<sub>z</sub>1)
8. Sm<sub>N</sub>6a: -ehe!kuna nydingine tena?
9. Mm<sub>z</sub>3a: {[Aa ulikuwa unataka hapa?
10. Sm<sub>N</sub>6a: [eeh..
11. Mm<sub>z</sub>3a: [aii Pole pole nilikuwa nahudumia mama hapa  
sikuwa nimekusikia mimi...
12. :[ ((Mm<sub>z</sub>3a akizungumzia mm<sub>z</sub>1)) Muka arienda ya green  
baba, nachanuki akarigara uyu nakumenya uu akuga.. (huyu  
mwanamke anataka ya green baba, amechanuka sana, anaelewa  
anachokisema)

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Mwanamke alipouza, alitumia lugha kwa njia iliyoonekana ‘kumtongoza’ mwanamume, jambo lililoonyesha unyonge wa mwanamke kwani alitumia jinsia yake kuwashawishi wanaume kununua tofauti na wanaume amba walitumia fujo nydingi na sentensi kavukavu katika kuuza (Tannen, 1990).

10. SM002A: Lugha yao ni tofauti sana na yetu. Hiyo yao haina lugha ya kutukanana. **Atauza ni kama anakukatiana ni kama anamgeuzia Kiswahili.** Ni ukweli yake kuwa **anakuangalia na zile macho na uchukue** miraa mbaya na pesa mob. Mwanamume kwa upande

mwingine, unamwangalia mpaka akupee kitu unataka na kwa pesa unataka.

11. SM004A: **Dame kabla auze miraa, watauza lakini watu watachoka na hiyo miraa haraka. Siwezi ambia dame vile naweza nikaambia mwanamume**
12. MM001A: Plus siwezi kumwambia miraa yake ni mbaya na vile ananiangalia na macho **zinakaa sijui aje sexy(( kicheko kutoka kwa wengi.))**
13. Jibu la wengi: eeeeeh inakuwanga hivyo ((kicheko tena cha wengi))
14. MM005A: Ni hivyo tu watu wanaongea. Ni hivyo tu  
**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala katika Kikundi Kiini A Uk. 125-126)**

Mwanamke pia alipofika dukani kununua miraa alikuja amejitanda kanga kwenye uso, au badala ya kusimama nje ya duka kwenye dirisha ambapo wengine (wanaume) walinunulia, yeye aliingia dukani kupitia mlango wa nyuma na kukaa ili auziwe akiwa ndani.

1. MM001B: Biashara yenyewe imechukuliwa kuwa ni ya wanaume na wanunuzi wengi ni wanaume.
2. MTF: Niligundua kuwa wanawake wanapokuja kununua huwa wanapita kwa mlango wa nyuma ilhali wanaume hununua wakiwa dirishani au kwa kutumia mlango wa mbele. Mbona hivyo?
3. Jibu kutoka kwa wengi: aaa kuna **wengine huwa hawatakangi kuonekana**
4. MTF: Kwani kuonekana kuna nini?
5. SM003B: aa unajua shida yao, mara ingine unaweza ukapata wanaume ndio wamejaa kwa dirisha na mwanamke huenda ni mmoja au wawili. **Sasa yeye ni kama hataki kusimama na hao wanaume au wanaume wale wako nje wanapelekwa sana sasa yeye anataka kuingia ndani ili aongee na muuzaji polepole au kwa utaratibu.**
6. MM003A: Lakini hiyo inalingana sana na tribe za kisomali. Kuna wale wanajua kuwa tribe zao **ziko hapo na anaogopa aonekane nao, na wale hawatakangi kuonekana na watu wao.** Lakini kuna yule, anajua kuwa hakuna mtu anamjua hapo kwa hivyo atakuja anunue tu, na kuna **either wale hupewa za**

*kujisaidia na miraa ni kitu ya starehe na akionekana akinunua hatawahi kupewa tena kwa hivyo anaingia ndani ili anunue.*

7. MTF: *Si dini, power au religion inafanya wafanye hivyo?*
8. Mm002B: *Yeye anaogopa kuonekana na watu wa kwao kama brother yake, au uncle, au mtoto wake. Huenda anaogopa kuonekana.*

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A na B uk.124, 144)**

Kuingia dukani kuliashiria mamlaka ambayo wanaume walikuwa nayo na mwanamke alikuwa hana. Mazingira ya miraa yalidhibitiwa na wanaume, kwa hivyo mwanamke alikuwa hatambuliwi. Hakutaka kuonekana na ndiposa aliingia dukani ili azungumze kwa upole na muuzaji. Kama alivyoeleza Carrier (2007) hata hivyo, idadi ya wanawake wanaoshughulika katika biashara ya miraa inaendelea kuongezeka kadri miaka inavyozidi. Aibu nayo, ya kuonekana na hata kujitokeza hadharani wakitafuna imeendelea kupungua na kuonekana kama jambo la kawaida. Haya ni matokeo yanayotofautiana na ya awali ya Labov (1972) kuwa wanawake wanatumia lugha ya upole.

*“...Lakini kuna wale pia wanakam direct tu kama wanaume na hata hawaogopi mtu wowote tu kama wanaume na wanasema lete miraa! Kama wanaume tu!” SM001B.*

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 126)**

Haya yanatokana na ukweli kuwa wanawake hasa wa jamii za Kisomali ndio huuza miraa kwa wingi kuliko wanaume wa jamii ya Somali.

1. MTF: Sijaona wanaume wa Kisomali wakiiza miraa kwa wingi.
2. SM002A: Huwa wanauzza Alele lakini si wengi. Hata ukienda Somali **95% ni wanawake ndio wanauzza. Wanawake ndio huuza sana.** Utawapata wanawake wengi kuliko wanaume. Business ya miraa haiwezi kutembezwa na wanaume. Wanawake ndio huweza kuuza sana. Nimeenda hata Somali pale miraa inatumwa na inauzwa. **Wamama ndio wanauzza huwezi ukapata wanaume kwa sababu wanaume watatafuna yote na hawatauzza hata! Wamama wako na discipline.**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini katika Uk. 135)**

Kutokana na hali hii, wanawake ndio walio na uwezo wa kuuza miraa, bila kuitafuna na kisha kupunguza mapato yao. Wanaume wakijapewa jukumu hilo, huenda wakaitafuna yote. Ndiposa wanawake wa Kisomali walionekana kama kiungo muhimu katika biashara ya miraa. Pia, waliuza miraa iliyo ya bei nafuu ikilinganishwa na ile inayouzwa madukani na wauzaji Wameru. Miraa hiyo ya bei nafuu ilisaidia wale ambao hawana pesa ya kutosha ili kununua iliyo ghali ilhali walihitaji kutafuna. Jambo ambalo lilileta usawa baina ya watu wote wa jamii ya watafunaji.

Kwa mfano, mwanammke alipofika dukani na kupata wanaume waliojaa dirishani pa kuuziwa miraa, alitulia kwanza kabla ya kuomba kuuziwa. Jambo la kimsingi katika biashara hii ni kuwa biashara yenyewe imedhibitiwa na wanaume. Kwa hivyo wanawake wachache sana au mmoja mmoja ndio walipatikana wakinunua au kuuza bidhaa ya miraa. Wanawake ambao waliuza kwa upande wake hawakumiliki maduka ya kuuzia kama walivyo wanaume, bali walipatikana mahali pa wazi au wameezeka vijibanda kando kando mwa barabara na kuuzia pale. Pia, waliuza miraa ambayo ilikuwa ya bei ya chini na isiyo ya dhamana kama ile inayouzwa na wanaume wenza. Hili huwaweka katika nafasi iliyobaguliwa wakilinganishwa na wanaume.

1. MM002B: **Lakini pia wanaume hawatambuangi macustomer wanawake sana. Kwa upande wa kununua ni mwanamume ako na buying power kuliko mwanamke.**
2. MM001B: Pia mwanamume akiamua kununua **atakuja hata kesho, lakini mwanamke atakuja mara moja kwa wiki au hata asikuje.**
3. SM001B: Na hata akiolewa na chali saa ingine anaambiwa aachane na miraa na anawacha miraa.
4. Jibu la wengi: ee Inakuwanga hivyo saa
5. MM004B: **Sasa utapata kuwa, macustomer wanaume ndio wanatambuliwa sana**
6. MTF: Wanaume wanatumbuliwa kwa sababu ya *consistency*?
7. MM004B: Ee imechukuliwa tangu kitambo kuwa biashara ya miraa ni ya wanaume. Kwa maana tuseme kutoka zamani wakati biashara ya miraa ilianza, wanawake wa Kimeru hawakuwa wameingia Nairobi. Hakuna wale walikuwa wanafanya hiyo biashara, hiyo biashara ilikuwa ya wanaume. Na ungeonekena ukifanya biashara kama hiyo ukiwa mwanamke, ungeonekena ukiwa mtu si wa kawaida.
8. MM003B: Ee wako, lakini si wengi

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 146)**

Biashara ya miraa imedhibitiwa na wanaume na hayo ndiyo maelezo makuu ni kwa nini kadri asilimia 99 % ya wanaume walipatikana wakinunua na kuuza miraa.

#### **4.3.1.3 Muhtasari Kuhusu Mfanano na Utuftauti wa Muundo Kutegemea Jinsia**

Wanawake walipooneka na wauzaji wakija walirejelewa kwa kiambishi ‘ka’. Na walipozungumza, waliita kwa sauti iliyolegea. Hawakuita kwa sauti ya kuamrisha kama walivyofanya wanaume.

Mfano,

1. Mm<sub>z</sub>4a: habari yenu? Niaje ?
2. Sm<sub>n</sub>5a: xxxxxx!
3. Fs<sub>z</sub>1a: niPatie, ..((sauti iliyolegea))
4. Mm<sub>z</sub>1a: ((akimzungumzia Mm<sub>z</sub>3 kwa Kimeru)).. tikau kamuka kangii aria nako tikau.. ndio hako kamwanamke kako kengine ongea nako)
5. Mm<sub>z</sub>1a: *Niatia miraa ikari ii indi* (Hii miraa inakaa aje hii sasa)
6. Mm<sub>z</sub>2a: *mbia ikura bwana..*(change imekosekana wewe..)
7. Mm<sub>z</sub>1a: sasa wewe unaniambia nini...

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Wanakikundi kiini A hata hivyo, walihisi kuwa wanawake na wanaume washiriki wa biashara ya miraa walitumia muundo sawa wa mazungumzo.

1. MTF: **Lakini lughya ya wanaume na wanawake hufanana, au nitofauti na ya wanawake?**
2. JIBU LA WENGI: **ni same ! ni same!**
3. MM003A: **Kwanza wamama ndio wanatukanana zaidi**
4. SM001A: **Hao kwanza ndio wako na matusi hapa**((akiashiria kwenye midomo))matusi yao!...
5. SM002A: “**Ayee si utupatiet miraa mbwa wewe!**” wanasema hivyo
6. MTF: Je wanapokuja kununua, huja na kutanguliza kuongea kwa salamu kama mambo-poa n.k.?
7. SM002A: Hakuna kawaida hapo, customer akikuja kwangu aanze hiso **story za mambo,habari za watoto,najua hana pesa.**
8. MM002A: **Hiyo ni ya kuuza nguo ama vitu zingine, ama** anakuja kukopa
9. SM001A: Huyo ni mtu hana shilingi, hana pesa
10. MM003A: **Huyo ameamua hiyo siku kukopa**
11. MM001A: **Huyo mtu hana pesa. Mtu ako na pesa anakuja anagonga meza na kukwambia, Mbwa niuzie miraa, na siombi!**
12. MTF: Na hiyo ndiyo kawaida yenu?
13. JIBU LA WENGI: Ee ni kawaida kabisa

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 125)**

Kwa kutamatisha, muundo wa mazungumzo ya wanaume na wanawake yalilingana kwa namna walivyoitisha na kulipia miraa, ila msamiati wa wanaume ulikuwa wa matusi na wa kuamuru wauzaji kuliko wa wanawake waliotumia sauti zilizolegea na kuwa na subira na (wakati mwingine kuonyesha sifa za ukavu na isiyo na subira). Matokeo yalikubaliana na ya De Klerk (1997) kuwa mtindo wa kuzungumza miongoni mwa wanaume na wanawake unaendelea kukaribiana huku wanawake wakionekana kuiga mitindo ya kiume ya kuzungumza.

#### **4.3.2 Ukabila na Muundo**

Katika mahusiano kati ya jamii mbili, muundo wa mazungumzo unaweza kufafana au ukatofautiana kutegemea athari za kimaingiliano (Liddicoat, 2007). Katika mazungumzo ya miraa, Wasomali na Wameru walionyesha kuwa na mtindo uliofanana. Wote walitumia sentensi za kuamrisha walipotaka kupata huduma.

#### **Mfano 22,**

- 13. sm<sub>N</sub>8a: leta shamba ya maana ...shamba ya maana leta..
- 14. :leta....leta miraa wariah lete miraa
- 15. Sm<sub>z</sub>2a: miraa mimi siuzi..
- 16. Mm<sub>z</sub>1a: ((Maongezi ya kando)) (nukwona kinya xxxx atikwenda umwenderia... gutiri ukwenda umwona.kuru ii guti muntu uticie waa bwake. Ontu igoro naracokerie miraa ugoro na akugite ekirwe. (Unaona hata xxxx hataki kumuuzia? Kila mtu hataki kumuuzia kwa sababu ya ujinga wake. Huyu ni mbwa huyu, hakuna mtu anataka kumwona. Kama jana alirejesha miraa masaa ya usiku na aliquwa amesema awekewe)
- 17. mm<sub>z</sub>1a: [ wee nini wewe miraa gani wewe]
- 18. sm<sub>N</sub>7a: [giza]giza mzuri kilo moja lete..
- 19. mm<sub>z</sub>1a: si umerudisha?
- 20. Sm<sub>N</sub>7a: leta kilo mzuri. Tafadhali.
- 21. :Iko Kazi mingi...wewe iko na mchezo eeh  
mm<sub>z</sub>1a: [wee shika
- 22. mm<sub>z</sub>1a :Wariah hakuna miraa

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)**

Katika kauli 17, 18 na 24 wanunuzi waliomba kupewa huduma kwa kusema ‘leta’. Muuzaji Sm<sub>z</sub>2a ijapokuwa ni wa jamii yake (Kisomali), naye alimwambia hauzi katika kauli 19. Jibu hilo ndilo lililomsukuma mm<sub>z</sub>1a kubadilisha msimbo ili kumtenga sm<sub>N</sub>8a katika mazungumzo. Mm<sub>z</sub>1a alisema katika kauli 20 kuwa hata hakutaka kumuuzia Sm<sub>z</sub>2a kwa sababu ya ujinga wa sm<sub>N</sub>8a .

Kutokana na mazungumzo haya, kutumia lugha ya mama ambayo  $sm_N8a$  hakuielewa, kungeonekana kama ni ubaguzi lakini ni mkakati mojawapo wa unyenyekevu alioutumia  $mm_z1a$  ili kumwepushia soni  $sm_N8a$ . Kwa sababu  $sm_N8a$  hangependa kusikia akisemwa kuwa “ana ujinga na kuwa  $Mm_z1a$  hakuna anapenda kumwona huyo mbwa...”

Katika mazungumzo mengine, ilionekana kuwa muuzaji Mmeru aliwahurumia wanunuzi walioshindwa kununua au hawakuwa na hela ya kutosha. Katika mfano 23, wasomali wawili walifika kununua miraa, mmoja wao alikuwa na mia tano na mwenzake alikuwa na mia tatu, wao walihitaji kuuziwa ‘quater’ ya miraa. Baada ya kuuziwa, mmoja wao aliamua kuchukua kiwango kikubwa kuliko mwenzake jambo lilimsukuma muuzaji (Mmeru) kumhurumia na kumuuzia *shurba* moja iliyokuwa akiomba.

### **Mfano 23,**

1.  $Mm_z6b$ : [Aii ..nyinyi mmezidi..]
2.  $Sm_N8b$ : [nani? sisi?]
3.  $Mm_z5b$ : [eeh nyinyi]
4.  $Sm_N8b$ : [sisi hapana zidi.]
5.  $Mm_z5b$ : [Miraa bei imeshuka halafu aii]
6.  $Sm_N8b$  : [Ni huyu tu.. Sio mimi mzee..]
7.  $Sm_N9b$  : eti unasema nini wewe, Eti mimi sina pesa.
8. :Kwani ni ajabu kuwa hakuna pesa?]
9.  $Sm_N8b$ : [ Sina pesa..mwambie tu
10.  $Sm_N9b$ : [nini wewe unaongea nini wewe.. shoqa wewe]
11.  $Sm_N9b$ : [Shurba kubwa basi uzia ... tafadhali]
12.  $Mm_z5b$  : [Sasa unaongea nini tena Kuso na wewe
13.  $Sm_N9b$ : shurba kubwa nataka mimi..  
tafadhalii
14.  $Mm_z5b$ : munenkere kubwa (Mpe hyo kubwa basi)  
:Lete ((akichukua pesa)
15.  $Sm_N9b$ : Nataka hiyo uko nayo wewe.((akipewa kisha  
anakagua kagua ))leta ile umenipatia kwanza.: Hakuna  
kitu unaongeza?
16.  $Mm_z5b$  :Bwana tuheshimiane Kuso na wewe bwana  
(ananyamaza na kuondoka)
17.  $Mm_z6b$ : *Huyu ena thina imbia huju..kwi ntuku*  
*ancumburire mwaka ndatura ndamutia ni* (huyu ana tamaa  
sana). Kuna siku alinisumbua hadi nikatoka mimi  
nikamwacha)

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 114)**

Kutokana na mfano huu, wauzaji waliwahurumia wateja wao wakati mwingine. Mnunuzi Sm<sub>N</sub>9b aliuliza katika kauli 16 “Na mimi sina pesa ingine..:Sasa nifanye nini... Nianze kushikashika watu wanapita kwa barabara?” Hali hiyo ndiyo iliyomsukuma Mm<sub>Z</sub>5b amwite Sm<sub>N</sub>8b angalau arudi ampe mwenzake Sm<sub>N</sub>9b miraa *shurba* moja. “((akimwita Sm<sub>N</sub>8b kwa sauti)). Wewe patia kuso moja wewe..:Wewe... mpatie moja..” Pia urafiki ulichangia katika kuadhere muundo wa mazungumzo baina ya muuzaji na mnunuzi. Ilibainika kuwa iwapo wazungumzaji walikuwa wamenunua na kuuziwa na mtu mmoja kwa kipindi kirefu cha wakati, basi mazungumzo yao yalikuwa na ukaribu. Kwa mfano, mazungumzo yafuatayo yalikuwa baina ya Mm<sub>Z</sub>7c na Sm<sub>N</sub>10c ambaye baada ya kununua miraa, hata alianza kujifungia kifurushi chake ndipo Mm<sub>Z</sub>7c akaanza kumfundisha kuifunga.

#### **Mfano 24,**

14. Mm<sub>Z</sub>7c: unataka karatasi ngapi leo
15. Sm<sub>N</sub>10c: Hapana leo mimi sitaki nyingi. Mimi nataka karatasi moja tu.
16. Mm<sub>Z</sub>7c: akiichukua miraa kutoka kwa sm11 na kuanza kuipanga ili amfungie
17. Sm<sub>N</sub>10c: nimeishika vizuri eeh. Nimejaribu,
18. Mm<sub>Z</sub>7c: na vile umeishika kama mtu anafunga mandazi au nini.Miraa unashika vizuri, sio kufunqa ikileqealeqea
19. Sm<sub>N</sub>10c: oooh miraa unashikanisha hivi kwanza eeh halafu unaweka eeh
20. Mm<sub>Z</sub>7c: Hata mgomba ukiishika wewe si itaisha yote?
21. Sm<sub>N</sub>10c: okey :Unashika vizuri eeh. Kumbe miraa haitaki pole pole.

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 115)**

Katika **mfano 24**, Mm<sub>Z</sub>1j alikiri kuwa SM<sub>N</sub>1j ni rafiki yake. Hata kama ulikuwa ujanja wa SM<sub>N</sub>1j kutaka kuja SM<sub>N</sub>1j alipotoa miraa mizuri kiasi kile wapi, inadhahirika kuwa walikuwa na uhusiano wa kiurafiki.

#### **Mfano 25,**

1. : ((anafika dukani huku ameshikilia miraa aliyonunua mahali kwingine. Mm<sub>Z</sub>1j anamwomba ili aiangalie.))
2. SM<sub>N</sub>1j: si wewe ni rafiki yangu?
3. SM<sub>N</sub>1j:ee
4. Mm<sub>Z</sub>1j: si ndio?
5. SM<sub>N</sub>1j: Ee
6. Mm<sub>Z</sub>1j: na hii umetoa wapi?
7. SM<sub>N</sub>1j:acha stori nyingi wewe
8. Mm<sub>Z</sub>1j : Huyu wewe ametoa upande gani?
9. SM<sub>N</sub>1j: nimwekwambia acha stori nyingi
10. Mm<sub>Z</sub>1j: nakuuliza umetoa 8th ama 12th?

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo j Uk. 121)**

Hali kama hii inaonyesha kuwa baada ya kutangamana kwa kipindi kirefu cha wakati, mahusiano baina ya watu kutoka khabila hizi mbili (Wameru na Wasomali) uliimariika na kukatokea ukaribu. Haya yalithibitishwa na maoni ya baadhi ya wanavikundi katika vikundi viini.

22. MTF: Je mnawenza mkaasemaje kuhusu uhusiano wa Wameru na Wasomali? Je ni miraa pekee inawaunganisha?
23. SM001A: Iko vitu mingi sana... kila kitu! Kila kitu!
24. MTF: Miraa ikijaondolewa siku moja, uhusiano wenu utaendelea ama utakatika?
25. JIBU LA WENGI: Aaaaaa sioni..
26. MM001A: Itakuwa lakini itakuwa *hostile*
27. SM001A: Iko, uhusiano iko
28. MM003A: Wengine ni watu wazuri sana. Kuna urafiki sio miraa pekee...
29. SM003A: Lakini ikiwa *the factor* ni miraa inawaunganisha *in one way or the other*
30. MTF: Miraa ikijaondolewa?
31. SM002A: **Inawafanya kwanza waunganike kuwa kitu kimoja na wakaanishe pamoja**
32. MM001A: Bila miraa mimi sioni kutakuwa na uhusiano na msomali wowote. Miraa ndio *catalyst*. Kwanza huku Eastleigh
33. MM004A: **Uhusiano wa mmeru na msomali huenda ukaendelea hata kama miraa haiko, lakini kitu kubwa ni juu ya miraa**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 130)**

Washiriki wa kikundi kiini walihisi kuwa shida zinazoikabili miraa kama vile kutangazwa kuwa ni mihadarati na kuhamarishwa katika nchi mbali mbali, kuliwaathiri watu wa jamii zote mbili.

Hata hivyo, walisema kuwa, “hata miraa ipigwe marufuku vipi, na bora kuna Wasomali wako na meno, basi miraa itatafunwa milele.” Kauli hii ni ishara tosha kuwa miraa na biashara zote zinazoizunguka miraa zitaendelea kuwepo siku za usoni.

Katika biashara ya miraa, hata palipokuwa na Mmeru na Msomali dukani, Wasomali waliokuja kununua walionelea ni heri wauziwe na Wameru kwani ndio walifahamu miraa bora. Wakati tu ambaa Msomali alikubali kuuziwa na msomali mwenzake, ni

pale ambapo alifahamu Kisomali tu na ikamwezesha kuzungumza lugha hiyo na msomali muuzaji ili apate huduma. Iwapo hakufahamu Kiswahili au Kiingereza azungumze na muuzaji wa jamii ya Ameru, basi alionelea auziwe na Msomali mwenzake. Kwa upande mwingine, wameru waliamua kuuziwa na wameru wenzao tu kwani wanaamini kuwa msomali hafahamu chochote kuhusu miraa.

1. MTF: Niligundua kuwa kama ni dukani, na kuna wauzaji wawili (msomali na mmeru) msomali hupendelea kuuziwa na msomali, je ni kweli?
2. JIBU LA WENGI: aaai hakuna
3. SM003B: Sio wengi. Na sio lazima
4. MM001B: hata pale unapata msomali anauza, saa ingine si eti ni juu ni msomali mwenzake, **wengine ni juu ya lugha ni kwa sababu wengine hawaongei kiswahili ama kizungu so wanaamua wauziwe na msomali ili waongee kisomali**
5. SM002B: Ee wengi wao wanajua kisomali pekee wengi wao. Hawaelewi lugha zingine. Kuna wale wametoka Somalia, wameingia Kenya kama hawajakaakaa kenya wajue Kiswahili, na wanajua kisomali pekee na ndio lugha wanaweza wakaongea na kuelewa, hapo ndio utapata msomali mwenzako kwa duka uamue ndiye anakuuzia
6. MM001B: **Maana msomali mwenyewe anaamini kuwa ni mmeru tu ndiye anajua miraa mizuri ya kumuuzia kuliko msomali**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 148)**

#### **4.3.2.1 Muhtasari kuhusu Utøfauti katika Muundo**

Katika utafiti huu, utøfauti wa muundo baina ya jamii mbili zilizotafitiwa katika mahusiano ya kibiashara ulidhihirika. Iligunduliwa kuwa wanaume ndio wamezama na kuboea katika biashara hiyo (kwa kununua na kuuza), ikilinganishwa na wanawake. Wanaume ndio walio na uwezo wa kifedha na ndiposa walikuwa wateja wa siku nyingi.

1. SM002B: Sisi dini yetu ya kiislamu vile inasema ni mwanamke na mwanamme si *equal*. Hatuko sawa. Hatutoshani. Mwanamke ni 50 na mwanamume ni 100. Yaani hata tuseme wakoseane mwanamke akujewe, watu wa hiyo familia yake watalipwa si *same*, kama ni *dame* watapewa 50, na kama ni *chali* 100.
2. MTF: Sasa tunaweza kusema kuwa ni dini inaleta tofauti hiyo?

3. SM001B: Ee dini ya kiislamu ni hivyo, wanaume ni *first level*. Na mwanamke anakuja nyuma.
4. MM002B: Lakini pia wanaume hawatambuangi macustomer wanawake sana. Kwa upande wa kununua ni mwanamume ako na *buying power* kuliko mwanamke.
5. MM001B: Pia mwanamume akiamua kununua atakuja hata kesho, lakini mwanamke atakuja mara moja kwa wiki au hata asikuje.
6. SM001B: Na hata akiolewa na chali saa ingine anaambiwa aachane na miraa na anawacha miraa.
7. Jibu la wengi: ee Inakwanga hivyo saa
8. MM004B: Sasa utapata kuwa, macustomer wanaume ndio wanatambuliwa sana
9. MTF: Wanaume wanatumbuliwa kwa sababu ya *consistency*?
10. MM003B: Ee either kwa kuuza na kununua sasa

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 148)**

Wanawake wa jamii ya Kisomali ndio waliouza miraa kwa wingi ikilinganishwa na wanawake wa Ameru.

SM002A: Wasichana wa Meru hawajawahi kuwa washiriki wa miraa, maybe wapike chai ya kutafunia. Hakuna mtu ashawahi kuelewa ni kwa nini ...wao hupika tu chai ili wapate pesa. Tena hii biashara haitaki uchukulie kila kitu mtu anasema ni ukweli. **Juu wanawake huwa wanasumbuliwa na opinion za mdomo na ukae juu jamaa atakuja akutukane akutukane na ukose kukasirika. Wanawake hukasirika ovyo so hawawezani na kuuza miraa kama wanaume.**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 134)**

Pengine wanawake wa Kisomali wanaiweza biashara hii kuliko wanaume wenza. Haya yanatokana na uvumilivu wao kazini.

34. MTF: Sijaona wanaume wa Kisomali wakiiza miraa kwa wingi.
35. SM002A: Huwa wanaiza Alele lakini si wengi. Hata ukienda Somali 95% ni wanawake ndio wanaiza. Wanawake ndio huuza sana. Utawapata wanawake wengi kuliko wanaume. *Business* ya miraa haiwezi kutembezwa na wanaume. Wanawake ndio huweza kuza sana. Nimeenda hata

Somali pale miraa inatumwa na inauzwa. Wamama ndo wanaauza huwezi ukapata wanaume kwa sababu wanaume watatafunaa yote na hawatauza hata! Wamama wako na discipline.

36. MM001A: Hakuna mtu huwaambia wasiuze, wanaume,
37. MTF: Wanawake wakija kununua na kuuza huwa *wamerelax* tu ikilinganishwa na wanaume
38. MM003A: *Mostly* wanawake wa Alele hawakujangi kununua *first time*, kuna mama anapiga simu anawekewa anakuja kuchukua tu. Hakuna kuongea. Si kama wanaume. Halafu bei ni *fixed* si kama hii ya kuja kuongea (*kunegotiate*) kama ni 1000 ni 1000. Yaani ingine unaweza *kunegotiate*. Ni tofauti.
39. MTF: lakini wanaume nimeona wanaauza mingi na wanauzia ndani ya nyumba na wanawake wanauzia nje. Kuna tofauti?
40. MM001A: Ni kama kuuza nguo ya karatasi na ya mtumba kwa *open market*. *Quality* si moja. Inamaanisha kama unaafford kulipa space ya kuuzia wewe uko na kitu ya maana.
41. SM002A: Yaani duka na yule wa nje, wa nje anatafuta watu wa kugonga na miraa mbaya.

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 133)**

Hata kama wanawake waliuza miraa kwa wingi, waliuza miraa iliyo ya kiwango cha chini. Fauka ya hayo, wao waliuzia kandokando mwa barabara ambapo waliweka meza na kwa msaada wa kivuli cha mwavuli. Hii ilikuwa ni ishara kuwa hawakuwa na uwezo wa kifedha kama walivyokuwa wanaume ambaa walikokodi nyumba (duka) la kuuzia.

Kwa hivyo, muundo wa mazungumzo wa Wameru iwapo aliyeuza ni Mmeru ulikuwa huu, alifika dukani na kuomba miraa kwa lugha ya Kimeru na kwa sababu hiyo alipata bidhaa nzuri. Iwapo aliyekuwa dukani ni mwanamume wa Kisomali, basi alihudumiwa naye kwa lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, Msomali alipofika dukani na kupata wauzaji wawili- Mmeru na Msomali, ( iwapo alifahamu lugha ya Kiswahili, basi aliuziwa na Mmeru kwa sababu aliamini kuwa Mmeru ndiye alifahamu miraa iliyo bora kuliko Msomali) na iwapo hakufahamu Kiswahili alizungumza Kisomali na Msomali

mwenzake ili ampe huduma. Lugha kwa hivyo, ilikuwa ni chombo muhimu katika kuamua muundo wa mazungumzo ya washiriki.

#### **4.3.2.2 Muhtasari Kuhusu Mfanano wa Muundo**

Jamii mbili zilizochunguzwa katika mazungumzo ya kibiashara, hujulikana na kutambulikana hapa nchini kama jamii za watu ambao wana ari kazini na wasio na subira nyingi. Ndiposa kukatokea kukatana kauli kwa kiwango kikubwa katika mazungumzo baina ya muuzaji na mnunuzi. Lakini ukataji kalima huo, haukuzuia kufanikiwa kwa mauzo na kila muuzaji na mnunuzi kuondoka dukani kama hajaridhika.

Kulingana na matokeo ya utafiti, ilibainika kuwa mazungumzo katika biashara ya miraa huchukua mipangilio mbalimbali ya ubadilishaji zamu. Mipangilio hiyo ilibadilika kutegemea wanunuzi waliofika dukani kwa wakati mmoja. Iwapo wanunuzi waliofika dukani ni wengi (kama sita), na walihitaji msaada wa muuzaji mmoja au wawili, basi palikuwa na ukatanaji kalima mwingi na zamu za mnunuzi mmoja zilibaki zimesubirishwa hadi pale ambapo mnunuzi mwingine alihudumiwa kwanza, kisha zamu yake kurejelewa. Si kwamba yule aliyeita kwa sauti ya juu ndiye aliyehudumiwa, bali wote walihudumiwa kutegemea mpangilio wao wa kufika pale dukani. Hatimaye, wanunuzi wote walishughulikiwa. Mpangilio huo wa zamu ulionekana kuwa changamano mno, na ultokana na udharura wa kuuza na kununua katika biashara ya miraa kutokana na hali ya kuharibika haraka kwa bidhaa hiyo (Carrier, 2005). Ingawa kusubirishwa kwa zamu kungeonekana kama sababu ya kuonyesha ujeuri kwa wanunuzi, washiriki walielewa kwamba wasingeweza kuhudumiwa wote kwa wakati mmoja na hivyo basi walikubali kusubiri bila kuudhika. Mpangilio wa moja kwa moja wa zamu pia ulidhihirika pale ambapo muuzaji hakuwa na wanunuzi wengi hivyo akawa na nafasi ya kuwasiliana na mteja wake kwa utaratibu.

Pili, biashara ya miraa mtaani Eastleigh ni biashara ambayo hufanyika kwa wakati maalumu. Limekuwa jambo la kimazoea kwa wauzaji na wanunuzi wa vizazi hadi vizazi kuwa miraa huwasili mtaani Eastleigh katika mida ya saa nane hadi saa tisa (kutegemea upatikanaji wake kule Meru au kutegemea ukasi wa gari lililotumika kama nyenzo ya usafirishaji). Katika ile mida ya saa tisa-saa kumi, biashara huwa imenoga na wanunuzi hutaka kufika madukani mapema ili wapate bidhaa iliyosafi (kwani miraa ni mmea unaokauka na kuharibika haraka hivyo kupoteza ladha yake kwa watafunaji). Udharura huu wa kufanya mambo ndio huchangia pakubwa katika matumizi ya lugha

legevu na hivyo kuifanya rejestra hii kuwa na upekee. Maadamu ni jambo ambalo limefanyika kwa miaka mingi, watu wanaojipata katika pilka pilka za biashara hiyo ‘hawajali’ namna wanavyozingatia lugha na kukatana au kutozingatia muundo wa ubadilishanaji zamu ulio na taratibu. Matokeo haya yanakubaliana na matokeo ya Miriti (2012) ambaye alieleza kuwa washiriki wa jamii hizi mbili wamekubaliana na wameshirikiana katika kufanikisha biashara baina yao kwa kutumia lugha kwa njia iliyo maalumu katika muktadha wa biashara hii.

#### **4.4 Mikakati ya Unyenyekevu**

Sehemu hii inashughulikia lengo la tatu la utafiti huu, ambalo lilikuwa ni kupambanua mikakati ya unyenyekevu iliyotumiwa na wauzaji na washiriki wa khabila na jinsia tafitiwa katika mazungumzo ya biashara ya miraa. Katika utafiti huu, mazungumzo baina ya wauzaji 10 na wanunuzi 10 waliokuwa wakitangamana moja kwa moja katika kujadiliana bei ya miraa walichunguzwa ili kutambua mikakati ya unyenyekevu iliyotumiwa ili kufanikisha mauzo.

Baada ya kutambua mikakati ya unyenyekevu kutoptana na mazungumzo, mtafiti aliwasaili wanakikundi 28 waliogawika katika vikundi vitatu. Mijadala hiyo ndiyo iliyotoa thibitisho au ufanuzi wa baadhi ya dhana ambazo mtafiti alikuwa amebainisha katika utazamaji wa shughuli ya kuuza na kununua. Mtafiti aliigawa na kuainisha mikakati ya unyenyekevu katika kategoria zifuatazo za wauzaji na wanunuzi ili kuonyesha umaratokezi wa kila mkakati:

<b>Mikakati</b>	<b>Mnunuzi</b>		<b>Muuzaaji</b>	
	Umaratokezi	%	Umaratokezi	%
Maamkuzi	10	10.5	8	5.8
Maneno ya heshima ya kutaja k.m, engineer, brother	12	12.6	25	18.2
Mzaha au utani	3	3.2	7	5.1
Vichekesho	5	5.2	5	3.6
Maombi	10	10.5	5	3.6
Kushukuru	6	6.5	10	7.2
Ubabilishaji msimbo	11	11.5	20	14.5
Makaribisho	3	3.2	13	9.4
Matumizi ya misamiati ya kibiashara	6	6.5	16	11.6
Upungukaji wa unyenyekevu	15	15.6	15	10.9
Matusi	5	5.2	6	4.3
Maagano	9	9.5	8	5.8
<b>Jumla</b>	<b>96</b>	<b>100%</b>	<b>138</b>	<b>100%</b>

*Jedwali 4: Mikakati ya Unyenyekevu katika Mazungumzo kutokana na deta iliyotunukuliwa na mtafiti*

Kutokana na jedwali 1, mikakati iliyotumika kwa asilimia kubwa zaidi 18.2% kwa upande wa wauzaji ni matumizi ya maneno ya heshima ya kutaja. Mkakati huo ulifuatwa na matumizi ya ubabilishaji msimbo uliochukua asilimia 14.5%. Mkakati uliokuwa wa tatu ni wa matumizi ya misamiati ya biashara na ukawa na asilimia 11.6%. Mkakati wa nne kwa wingi wa matumizi ni wa upungukaji wa unyenyekevu uliozoa asilimia 10.9%. Mkakati wa tano, ulikuwa wa makaribisho na ulikuwa na asilimia 9.4%. Kushukuru kukawa ndio mkakati wa sita kiutumikaji na kukachukua asilimia 7.2%. Mkakati wa saba ukawa ni wa maamkuzi na maagano uliowakilishwa kwa asilimia 5.8%. Mzaha na utani ukachukua asilimia 5.1% huku matusi yakizoa asilimia 4.3%. Mikakati iliyotumika kwa uchache zaidi ni ya maombi na vichekesho kwa asilimia 3.6 % mtawalia.

Kwa upande wa pili, wanunuzi walizingatia mikakati ya unyenyekevu iliyotumiwa na wanunuzi ni kama ifuatavyo. Mkakati uliotumika zaidi ni wa upungukaji wa

unyenyekevu uliochukua asilimia 15.6%, kisha matumizi ya msamiati wa kutaja wa heshima-asilimia 126%, kisha ubadilishaji wa msimbo 11.5%, halafu maamkizi yakazoa 10.5%, maagano yalichukua asilimia 9.5%, matumizi ya msamiati wa biashara pamoja na kushukuru yalikuwa na asilimia sawa ya 6.5%. Matusi na vichekesho vilikuwa na asilimia 5.2% kila mojawapo. Mikakati iliyokuwa na asilimia ya chini zaidi kimatumizi ni pamoja na mzaha na makaribisho ambayo yalichukua asilimia 3.2% pekee. Mtafiti alifafanua mikakati iliyoorodheshwa katika *jedwali 1* kwa kina katika vijisehemu vifuatavyo:

#### 4.4.1 Maamkuzi

##### **Msamiati uliotumika katika maamkuzi**

<b>Wauzaji</b>	<b>Wanunuzi</b>
Sema brother	Niaje, Vipi
Aye, sema	Aye, daddy
Sema boss	Vipi boss
Sema engineer	Itakuwaje, Sema

*Jedwali 5: Msambao wa misamiati iliyotumika katika maamkuzi*

Kutokana na kielelezo 1, wauzaji na wanunuzi walitumia maneno tofauti kuamkua wenzao kabla ya kupokea huduma.

#### Kwa mfano 26,

1. Sm<sub>z</sub>12e :aa sema wariah..
2. Sm<sub>N</sub>14e: Nataka miraa mzuri kabisa..
3. : Lete miraa mirefu

##### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 117)**

Katika **mfano 26**, Sm<sub>z</sub>12e ndiye alimwamkua Sm<sub>N</sub>14e kwa kumwambia, “sema wariah..” Maamkuzi kulingana na Wei (2010), humfanya mteja ahisi huru na kuwa mhudumu alikuwa tayari kumpa huduma. Katika **mfano 26** aliona ni vyema amuamkue mteja wake kwani angeanza tu kumuuliza alitaka nini angeonekana ni kana kwamba uwepo wa mteja ulimuudhi. Kwa hivyo angeonekana mjeuri jambo ambalo hangependelea kufasiriwa vile kwa sababu alihitaji yule mnunuzi arejee tena na tena pale dukani kwake kupata huduma zake. Brown na Levinson (1987), walieleza kuwa kumwamkua mteja kwa mfano, ni dhihirisho la unyenyekevu chanya, kwani muuzaji aligundua uwepo wa mnunuzi na kuwa alikuwa tayari kumkidhia mahitaji yake. Katika muktadha huu, Sm<sub>z</sub>12e kwa mfano aligundua uwepo wa binadamu mwenzake Sm<sub>N</sub>14e,

ambaye kufika kwake dukani kulikuwa ni ishara ya kutaka kununua miraa. Kwa hivyo, Sm<sub>z</sub>12e alijituma kumtimizia haja yake ya kumpa huduma na ndiposa akamwamkua katika kauli 1.

#### **4.4.2 Maneno ya Heshima ya Kutaja**

Brown na Levinson (k.h.j.) walibainisha kuwa, kutumia maneno ya mtajo ya heshima mazungumzoni ni mkakati wa unyenyevu na hulenga kuepushiana tahayuri baina ya wazungumzaji. Maneno ya heshima ya kutaja yanapotumika, huwa ni tendo la kimakusudi kwa anayetumia, kwani hudinda kuonekana kushinikiza maswala yake kwa mzungumzi mwenza. Matumizi ya maneno ya heshima ya kutaja ndio mkakati uliotumika kwa asilimia kubwa zaidi na wauzaji na wanunuzi walitumia 18.2% na 12.6% mtawalia. Kwa upande wa wauzaji kwa mfano,

#### **Mfano 27;**

1. MM<sub>z</sub>9e: Baba tafadhali tuheshimiane [ndugu yangu]
2. SM<sub>N</sub>14e:  [Sorry sorry]
3. MM<sub>z</sub>9e: Heshima ni kitu mzuri. Baba tafadhali, tafadhali,  
tafadhalu nakuomba. Nakuambia heshima ni mzuri,
4. SM<sub>N</sub>14e: eh ni mzuri
5. MM<sub>z</sub>9e: basi enda baba tafadhali. Enda ndugu yangu.

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 118)**

Muuza ji MM<sub>z</sub>9e alijaribu kumwomba kwa heshima SM<sub>N</sub>14e aondoke baada ya kushindwa kuelewana bei ya miraa. Alitumia maneno *tafadhalu*, *ndugu yangu*, *tuheshimiane* akimsihi mnunuzi aondoke pale biasharani. Alimkumbusha pia, katika kauli ya 3 kuwa heshima lilikuwa ni jambo zuri kwa hivyo akubali tu na kuondoka pale dukani mwake kauli 5. Asilimia 18.2% ilidhihirisha kuwa heshima katika kuwataja wanunuzi ilikuwa muhimu zaidi katika udumishaji wa wateja. Kwa upande wake, SM<sub>N</sub>14e alimwambia *sorry*, kuonyesha kuwa alikuwa amegundua makosa yake na kwa hivyo aliomba msamaha. Brown na Levinson (1987), walieleza kuwa kuomba msamaha ni tendo la unyenyekevu kwani mzungumzaji hugundua athari ya semi zake na kuomba msamaha kwa mpokezi wa usemi.

Katika **mfano 27** basi washiriki wa uzungumzi waligundua kuwa walikosa na ndipo walitumia maneno ya kuomba msamaha ili kuepushiana tahayuri na kuonekana kujali mahitaji ya wenzao. Kuhusu matumizi ya maneno ya heshima ya mtajo, Njambi (2015) aligundua kuwa wauzaji wa nguo mjini Thika walitumia mkakati wa kutaja kwa heshima kwa maneno kama vile: *ny'ina wa Njoki (mother to Njoki) au mai ndia (my*

*dear) au my sister ili kuwaonyesha heshima wateja wake. Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na yale ya awali ya Njambi (2015), kwani mtafiti pia aliwapata wateja waliofanyiwa uchunguzi wakitumia misamiati kama vile *baba*, *mzee*, *ndugu* *yangu* n.k.*

Katika **mfano 28**, *Mm<sub>z</sub>5b* alimrejelea mteja wake kama *baba* naye *S<sub>m</sub>N8b* akamwita *mzee*. Kutaja hivi, kulikuwa na lengo la kuwafanya wanunuzi wahisi kuwa wameenziwa kwani maneno waliyotumia kutaja yalibeba maana ya upendo na heshima kipragmatiki.

### **Mfano 28,**

1. *Mm<sub>z</sub>5b*: miraa ya mia nane huwezi pata **baba**
2. *S<sub>m</sub>N9b* na *S<sub>m</sub>N8b*: ((wanabadilisha msimbo na kuzungumza kwa Kisomali))
3. *S<sub>m</sub>N8b*: **mzee**, niwekee *yangu basi..*  
:nipatie hiyo *yangu basi...*  
i. .. :sawa?
4. *Mm<sub>z</sub>6b*: Sasa mtagawana shurba moja *basi muende*

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 113)**

Katika **mfano 29**, *Mm<sub>z</sub>3a* alimrejelea mnunuzi wa kike *F<sub>s</sub>N1a* kama *mum*. Tamko hilo la *Mm<sub>z</sub>3a* lilikuwa la kimakusudi ili amwonyeshe *F<sub>s</sub>N1a* kuwa naye pia alikuwa na dhamani kama wale wanunuzi wengine wa kiume. Kauli yake *Mm<sub>z</sub>3a* pia ilitokana na hali ya kwamba *F<sub>s</sub>N1a* alihisi kuwa amesahaulika na alikuwa ameanza kukasirika. Katika kauli 21 na 22, *F<sub>s</sub>N1a* anaonekana kujawa na hamaki.

### **Mfano 29,**

18. **Sema boss..**
19. *S<sub>m</sub>N1a*: (baada ya kusubiri hela yake kwa kipindi kirefu)... Mambo gani hii...
20. *Mm<sub>z</sub>1a*: kwani wee[wee..]
21. *F<sub>s</sub>N1a*: [wewe shi]da gani (kwa hasira) eeh...
22. :Kwani iko shida gani...((akisema kwa kutoridhika))
23. :niuzie miraa mzuri((akizungumza kwa sauti ya chini.))
24. *Mm<sub>z</sub>3a*: **nqoja niwashe taa mum**
25. *F<sub>s</sub>N1a*: Niuzie miraa wewe
26. *Mm<sub>z</sub>1a*: [Unataka nini wewe..  
: ((ka unenkerere shoka ii yite bwana))..**shika umpe shoga** huyu aende bwana..]
27. *Mm<sub>z</sub>3a*: aa hapana ombar..
28. *F<sub>s</sub>N1a*: Pande gani.. niuzie miraa wewe!
29. *F<sub>s</sub>N1a*: **sitaki hiyo, nataka rangi ya hii**

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)**

Katika kauli 65,  $F_{S1}$  anasema rangi ya miraa ambayo anaitaka yeye. Hili linaashiria kuwa pana mahitaji ambayo  $F_{S1}$  anayo, na anajua kuwa  $M_{M3}$  anao uwezo wa kuyatimiza. Kwa hivyo  $F_{S1}$  anazingatia mkakati wa unyenyekevu wa kusema waziwazi-kutaja anachokitaka, “sitaki hiyo, nataka rangi ya hii.” Hali hiyo inamshinikiza  $M_{M3}$  atende kwa namna  $F_{S1}$  anavyotaka (kwa kusudi la kuwa mnyenyekevu) kwa sababu kama muuzaji, yuko pale kwa ajili ya kutimizia wanunuvi wake haja zao.

#### **4.4.3 Mzaha au Utani na Vichekesho**

Mzaha na vichekesho katika muktadha wa biashara hii ulichukuliwa kuwa hali ambapo washiriki wa mazungumzo walitoa semi ambazo zilikusudiwa kudhahiki. Kutohakana na jedwali la umaratokezi, mkakati huu ulikuwa mojawapo ya ile ilichukua asilimia kidogo sana. Kwa mfano, upande wa wanunuvi, mkakati huu ulizoa asilimia 3.2% pekee, ilhali wauzaji walitumia kwa asilimia 5.1%. Vichekesho pia, vilichukua asilimia ndogo zaidi ambapo wanunuvi walitumia 5.2% na wauzaji 3.6%. Lengo kuu la wazungumzaji kutumia masihara katika biashara huwa ni kuzua ukaribu au kuvunja urasmi ambao mara nyingi huwepo baina yao (Grundy , 2000). Katika mazingira ya biashara ya miraa, mifano kama hii ilidhahiri;

#### **Mfano 30,**

1.  $SM_{N1g}$ : 1500 mimi iko nayo
2.  $MM_{Z1g}$ : Aaa huwezi sema hivyo *my brother*. 1500 kidogo sana
3. : (( baada ya kuzungumza na wauzaji wengine kwa dakika moja )) : Wariah umeamua aje
4. :((Kwa sauti ya chini))Elfu mbili leta na usiseme nimekuuzia hiyo bei
5.  $SM_{N1g}$ : XXXXXX ni hivyo? Ni XXXXXXXX?
6.  $MM_{Z1g}$ : **Wee hapana nani anaitwa XXXXXX hiyo pesa imeenda kwa kikuyu wewe bwana**
7.  $SM_{N1g}$ : itarudi tu. Sawa lakini?

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 121)**

Katika mfano 30, baada ya  $SM_{N1g}$  na  $MM_{Z1g}$  kukubaliana bei ya miraa,  $SM_{N1g}$  aliamua kumtumia pesa kwenye rununu. Hapo ndipo  $MM_{Z1g}$  alimdhahiki  $SM_{N1g}$  kuwa jina alilotamka  $SM_{N1g}$  si lake, bali ni la Kikuyu (kauli 6).  $MM_{Z1g}$  alikusudia kudhahiki kwa kusema kuwa jina lililosemwa na  $SM_{N1g}$  kuwa limepokea pesa si lake. Hata hivyo,

SM<sub>N</sub>1g hakuonekana kutishika kwani alisema kuwa hata kama hiyo pesa ilienda kwa Kikuyu, bado ingerudi (kauli 7). Kutopatwa na wasiwasi kwake SM<sub>N</sub>1g, kuliashiria kuwa alitambua utani wa MM<sub>Z</sub>1g.

Katika **mfano 31**, Sm<sub>N</sub>10c alipokabidhiwa miraa na Mm<sub>Z</sub>7c ajifungie, ndipo alipoeleza kuwa yeze hangeweza kufunga labda Mm<sub>Z</sub>7c amsaidie. Tunamwona Mm<sub>Z</sub>7c akimfundisha kufunga miraa kwa kumpa maelezo bayana katika kauli 7.

**Mfano 31;**

1. Mm<sub>Z</sub>7c: shika. ((Akimkabidhi sm11 ajifungie kifurushi chake cha miraa mwenyewe))
2. Sm<sub>N</sub>10c: Hapana. Wewe ndio utajua utafunga vipi. Mimi sijui.
3. Mm<sub>Z</sub>7c: wewe ndio utazoea kujifungia sasa
4. Sm<sub>N</sub>10c: eeh. Mimi nitazoea kuzishikashika. nitazoea. Next time mimi nitajifungia mwenyewe. Hakuna haja nikusumbue mimi daddy.. nitazoea tu.
5. Mm<sub>Z</sub>7c: akichukua miraa kutoka kwa sm11 na kuanza kuipanga ili amfungie
6. Sm<sub>N</sub>10c: nimeishika vizuri eeh. Nimejaribu,
7. Mm<sub>Z</sub>7c: na vile umeishika kama mtu anafunga mandazi au nini. Miraa unashika vizuri, sio kufunga ikileqealeqea
8. Sm<sub>N</sub>10c: oooh miraa unashikanisha hivi kwanza eeh halafu unaweka eeh
9. Mm<sub>Z</sub>7c: Hata mgomba ukiishika wewe si itaisha yote?
10. Sm<sub>N</sub>10c: okey
11. :Unashika vizuri eeh. Kumbe miraa haitaki pole pole.
12. Mm<sub>Z</sub>7c: lakini inataka kutolewa polepole
13. Sm<sub>N</sub>10c: Kuna siku nilikuwa na miraa kwa mfuko nikidhani miraa iko kumbe ni maganda iko tu... iliisha kitambo(akisimulia kichekesho)
  - a. ((kishaa anaondoka))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo c Uk. 115)**

Katika kauli 7, Mm<sub>Z</sub>7c alimweleza kuwa Sm<sub>N</sub>10c alikuwa amefunga miraa kama ‘mandazi’ kwa sababu ilikuwa imefungwa huku imelegea. Sm<sub>N</sub>10c aligundua utani huo, kisha akachecha. Kicheko hicho ndicho kilisababisha Sm<sub>N</sub>10c asimulie kisa (kauli 13) ambacho kilimchekesha Sm<sub>N</sub>10c.

Kutokana na takwimu katika jedwali 3, mikakati ya utani na vichekesho ilitumika kwa uchache zaidi. Hali hiyo ilisababishwa na uuzaaji na ununuzi wa miraa ulifanyika katika kipindi kifupi cha wakati baina ya mteja mmoja na mwengine, na kwa hivyo hamna muda mwengine wa kufanya utani au mzaha kati ya muuzaji na mnunuzi. Jambo

lililosababishwa na uharibikaji wa haraka wa bidhaa hiyo (miraa) Carrier (2015). Kwa hivyo, wateja walinunua mapema ili waanze ‘starehe’ zao za utafunaji mapema. Matokeo hayo ni sawia na yaliyodhihirishwa na wauzaji, ambao walitumia asilimia 3.6 pekee ya vichekesho. Ilibainika katika mijadala kuwa, hapana nafasi ya kutaniana kwa sababu hapana muda wa kufanya hivyo.

MM001B: Ee hiyo iko. Unajua unaweza sema hivyo, kwa maana unaweza kuja ile *peek hours*. Sasa wewe umekuja kupeana *story* nyingi badala ya kusema ile miraa unataka upewe. Na sasa ukianza kupeana *story* nyingi utasikia ukiambiwa “ni nini unataka, sema ile unataka ama uende.” Kwa sababu umekuja wakati ambayo biashara imeshika sana, na kuna wengine wako hapo (*customers*) wanangoja kuuziwa na wewe uko hapo na *story* zako nyingi. Lazima utakatizwa katikati.

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 143)**

#### **4.4.4 Maombi**

Katika biashara hii, maombi yalifanyika kwa namna tofauti baina ya wauzaji na wanunuzi. Mkakati huu wa unyenyekevu ulichukua asilimia chache kwa upande wa wauzaji walitumia 3.6% ya maneno ya kuomba. Kwa upande wao, wanunuzi walitumia mkakati wa kuomba kwa asilimia 10.5%.

Katika mfano 32, maombi aliyofanya Sm<sub>N</sub>9b katika kauli 1 ni kuwa auziwe *shurba* kubwa. Alifahamu kuwa Mm<sub>Z</sub>5b alikuwa na haki ya kutosikiliza na kutenda kama alivyoomba, na ndipo alitumia msamiati wa kuomba *tafadhalli* katika kauli 1 na 3. Brown na Levinson (1987), walifafanua kuwa maombi humtia soni mpokeaji wa kauli, kwani huhisi kuwa uhuru wake wa kuamua na kutenda jinsi anavyopenda huwa umetishwa. Maombi kwa hivyo ni mojawapo ya mikakati hasi ya unyenyekevu. Kutokana na uhuru wa Mm<sub>Z</sub>5b kutishwa na maombi yaliyotolewa na Sm<sub>N</sub>9b, alimweleza mwenzake Mm<sub>Z</sub>6b katika kauli ya 4 ampe hiyo shurba kubwa.

#### **Mfano 32,**

1. Sm<sub>N</sub>9b: [ Shurba kubwa basi uzia ... tafadhali ]
2. Mm<sub>Z</sub>5b : [ Sasa unaongea nini tena Kuso na wewe ]
3. Sm<sub>N</sub>9b: shurba kubwa nataka mimi..  
tafadhalli
4. Mm<sub>Z</sub>5b: ((akimweleza mwenzake, Mm<sub>Z</sub>6b)) munenkere kubwa  
(Mpe hiyo kubwa basi)

5. :Lete ((akichukua pesa)
6. . Sm<sub>N</sub>9b: Nataka hiyo uko nayo wewe. ((akipewa kisha anakagua kagua ))leta ile umenipatia kwanza.: Hakuna kitu unaongeza?
7. Mm<sub>Z</sub>5b :Bwana tuheshimiane Kuso na wewe bwana (ananyamaza na kuondoka)
- 8 Mm<sub>Z</sub>6b: Huyu ena thina imbia huj..kwi ntuku ancumburire mwaka ndatura ndamutia ni (huyu ana tamaa sana. Kuna siku alinisumbua hadi nikatoka mimi nikamwacha)

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo b Uk. 114)**

Hata hivyo, maombi ya Sm<sub>N</sub>9b kusikilizwa na muuzaji yalikuwa na mipaka. Hata baada Mm<sub>Z</sub>5b ya kusema Sm<sub>N</sub>9b apewe shurba kubwa, Sm<sub>N</sub>9b aliendelea kukagua miraa ( kauli 6) akirejesha jambo ambalo halikumpendezza Mm<sub>Z</sub>5b. Katika kauli 7, Mm<sub>Z</sub>5b alimtahadharisha kuwa, “Bwana tuheshimiane Kuso na wewe bwana (ananyamaza na kuondoka) Maombi ya Mm<sub>Z</sub>5b na Sm<sub>N</sub>9b ni tofauti. Maombi yaliyotolewa na Mm<sub>Z</sub>5b yalikuwa ya kumpa onyo Sm<sub>N</sub>9b kwani hakuwa anaridhika na alikuwa na tamaa nyingi kama alivyoeleza Mm<sub>Z</sub>6b katika kauli 8. Mm<sub>Z</sub>5b alikuwa amekasirishwa na tabia yake ya kutoridhika kila alipopewa miraa alikagua na kuirejesha.

Katika mfano 33, maombi ya yilikataliwa na Mm<sub>Z</sub>1a ijapokuwa sm<sub>N</sub>7a alitumia misamiati ya kuomba kama vile *please*.

**Mfano 33,**

1. sm<sub>N</sub>7a:[leta na harakisha please
2. Mm<sub>Z</sub>1a\_\_\_\_:wariah hakuna miraa?lete miraa na harakisha please kuna kazi nyingi sana leta
3. sm<sub>N</sub>7a :wee madam songa weee ((akimzungumzia FS<sub>N</sub>1))
4. sm<sub>N</sub>7a:harakisha please wee..

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)**

Ni kutokana na mfano huu 33, tulipobainisha matumizi mengine ya unyenyekevu kama alivyotambilisha (Grundy , 2000). Grundy alieleza kuwa kufafanua sababu za kutenda jambo fulani, ni mfanyiko wa unyenyekevu. Kwa hivyo sm<sub>N</sub>7a alitumia unyenyekevu alipoeleza kuwa alikuwa na haraka na alikuwa na kazi nyingi sana (kauli 2).

**Mfano 34,**

Katika mfano 34, kauli 7, MM<sub>Z</sub>9e alimwomba SM<sub>N</sub>14e aondoke pale dukani baada ya kushindwa kuelewana. Basi SM<sub>N</sub>14aliitikia maombi ya MM<sub>Z</sub>9e na kuondoka.

1. MM<sub>z</sub>9 e: Lete miraa wewe
2. SM<sub>N</sub>13e: Ngoja basi wariah wewe
3. :((kwa mzaha)) Iko hapa
4. MM<sub>z</sub>9e: Baba tafadhali tuheshimiane ndugu yangu//SM<sub>N</sub>14 Sorry sorry//
5. MM<sub>z</sub>9e: //Heshima ni kitu mzuri. Baba tafadhali, tafadhali, tafadhali nakuomba . Nakuambia heshima ni mzuri,
6. : eh ni mzuri
7. MM<sub>z</sub>9e: basi enda baba tafadhali. Enda ndugu yangu.  
(SM<sub>N</sub>14e anatoka dukani na kuondoka))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 118)**

#### **4.4.5 Ubadilishaji Msimbo**

Kubadilisha msimbo katika mazungumzo ya miraa baina ya wauzaji na wanunuzi. Mkakati huu wa unyenyekevu ulichukua asilimia kubwa sana ikilinganishwa na mikakati mingine iliyotumika. Wanunuzi kwa mfano walitumia asilimia 11.5% ya mkakati huu, huku wauzaji wakitumia jumla ya asilimia 14.5%. Mazungumzo katika utafiti huu yalishirikisha watu kutoka jamii na lugha tofauti. Kwa hivyo makisio ya kubadilisha msimbo yalikuwa ni ili mtumizi lugha awatenge waliokuwa wa lugha na jamii hiyo nyingine. Kwa mfano, kutoptera na mazungumzo ya mfano 35, mm<sub>z</sub>1a alibadilisha msimbo ili kumtenga Sm<sub>7</sub>a katika mazungumzo. Mm<sub>z</sub>1a alitambua kuwa alichokuwa anakusudia kukisema hakingempendeza kama mteja iwapo angekisema kwa lugha aliyoifahamu Sm<sub>N</sub>7a. Kwa hivyo, mm<sub>z</sub>1a walishirikiana na mm<sub>z</sub>3a ili wamtenge Sm<sub>N</sub>7a kwani walijali uteja wake. Ijapokuwa Sm<sub>N</sub>7a (katika kauli 7 na 9) alikuwa na tabia ambazo hazikupendeza, wauzaji walihitaji arejee pale siku nyingine kununua. Kujali huku kwa maslahi ya wazungumzaji wenza ni unyenyekevu kulingana na Goffman (1967). Ndiposa mm<sub>z</sub>3a alichagua kubadilisha msimbo ili asiweze kudhuru hisia za mwenzake katika mazungumzo.

#### **Mfano 35,**

7. mm<sub>z</sub>1a: *ka aregere kugura na aguraa nara 12 uju?* (Kwani amekataa kununua pale huwa ananunua huko 12?)
8. Mm<sub>z</sub>3a: *uriku?* (Nani?)
9. mm<sub>z</sub>1a: *kiaa ki kiwitia miraa kii..* (mjinga huyu anayeitisha miraa )
10. Sm<sub>N</sub>7a : *Aukinya njira aitaa ii?* (Amekasirika akaenda eh?)
11. : ((baada ya kukagua miraa kwa wakati mrefu anaondoka bila kuinunua))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 112)**

Katika mfano 36, ubadilishaji wa msimbo ultumika kama mkakati wa kumtenga mnunuzi pia.

### Mfano 36,

8.  $F_{S1a}$ : sitaki hiyo, nataka rangi ya hii...
9.  $M_{Mz3a}$ : [Hautaki rangi ya hiyo... unataka rangi ya ...  
 $F_{S1a}$ : nataka rangi ya green..
10.  $M_{Mz3a}$ : Unataka green? Green(nipee nytingine ya green-  
akimzungumzia  $M_{Mz1}$ )
11.  $S_{M6a}$ : -hey! kuna nytingine tena?
12.  $M_{Mz3a}$ : {[Aa ulikuwa unataka hapa?
13.  $S_{M6a}$ : [eeh..
14.  $M_{Mz3a}$ : [aai Pole pole nilikuwa nahudumia mama hapa  
sikuwa nimekusikia mimi..
15. :[ (( $M_{Mz3a}$  akizungumzia  $M_{Mz1}$ )) Muka arienda ya green  
baba, nachanuki akarigara uyu nakumenya uu akuga.. (huyu  
mwanamke anataka ya green baba, amechanuka sana, anaelewa  
anachokisema)

### (Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)

Katika kauli 15,  $M_{Mz3a}$  alibadilisha msimbo ili apate nafasi ya kumseng'enza  $F_{S1a}$ . Kutokana na usemi wake  $M_{Mz3a}$  ndipo tulielewa kuwa mwanamke akitambua rangi ya miraa iliyo bora 'green' basi ndiko walikoita 'kuchanuka'. Ni kauli hii iliyoonyesha kuwa iwapo mwanamke si makini katika biashara ya miraa basi huenda akajipata ameuziwa miraa mibovu kwa kutofahamu miraa iliyo bora.

### Mfano 37,

1.  $s_{M7a}$  : madam songa weee
2. :[leta na harakisha please
3. :wariah hakuna miraa?lete miraa na harakisha please  
kuna kazi nydingi sana leta
4. :wee madam songa weee ((akimzungumzia  $F_{S1}$ ))
5. :harakisha please wee..
6.  $s_{M8a}$ : leta shamba ya maana ...shamba ya maana leta..
7. :leta...leta miraa warrior lete miraa
8.  $S_{M2a}$ : miraa mimi siuzi..
9.  $M_{Mz1a}$ : Maongezi ya kando(*nukwona kinya xxxxx atikwenda umwenderia... gutiri ukwenda umwona.kuru ii guti muntu uticie waa bwake. Ontu igoro naracokerie miraa ugoro na akugite ekirwe.* (Unaona hata xxxxxx hataki kumuuzia? Kila mtu hataki kumuuzia kwa sababu ya ujinga wake. Huyu ni mbwa huyu, hakuna mtu anataka kumwona. Kama jana alirejesha miraa masaa ya usiku na aliquwa amesema awekewe)
10.  $M_{Mz1a}$ : [ wee nini wewe miraa gani wewe]
11.  $s_{M7a}$ : [giza]giza mzuri kilo moja  
lete..

### (Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 111)

Katika mazungumzo haya, ubadilishaji msimbo umefanywa na wauzaji ili wamtenge mnunuzi. Katika kauli ya 9, M<sub>m</sub><sub>z</sub>1a alieleza kuwa hata S<sub>m</sub><sub>z</sub>2a hataki kumuuzia S<sub>m</sub><sub>N</sub>7a (kauli 8). Hili linaonyesha kuwa wauzaji wote pasi kuegemea jamii yao, walishirikiana ili kupinga kuwapa huduma wanunuzi waliozua shida.

Katika utafiti huu wauzaji na wanunuzi wa jamii moja walibadili msimbo kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi lugha ya kwanza (Kisomali au Kimeru) ili kuwatenga wale wa jamii nyingine. Walipotumia lugha ya Kimeru kwa mfano, wauzaji wa jamii ya Wameru walitaka kuwaepushia tahayuri wanunuzi wa Kisomali.

#### **4.4.6 Makaribisho**

Makaribisho ni mkakati uliotumika kwa asilimia ndogo zaidi na wanunuzi 3.2% kwa sababu walifika dukani na kukaribishwa na wauzaji 9.4% ambao walikuwa dukani. Makaribisho yaliandamana na maamkizi katika mazungumzo. Kwa hivyo, mkakati huu wa unyenyekevu ulikuwa na uchache sana kwa sababu mazungumzo yalianza karibu na upeo wake ambapo mnunuzi aliitisha bidhaa na kuendelea na mazungumzo ya kujadiliana bei. Makaribisho yalifanyika kwa uchache na wanunuzi kwani walifika dukani na kuitisha bidhaa kwa kusema *leta*. Wakati mwengine, wanunuzi walipaaza sauti wakiwa mbali na duka lenyewe mradi tu ateket nadhari ya wauzaji ili akifika tu apate huduma.

#### **Mfano 38,**

1. M<sub>m</sub><sub>z</sub>3a: ingia// ingia ingia ingia iko
2. S<sub>m</sub><sub>z</sub>2a: Toka hapo toka hapo wewe
3. M<sub>m</sub>1a:  
[toka, shuka hapo wewe ] (( simu yake inalia, akiwa anazungumza kwa simu)).. sawasawa baba, sawa aye...)

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo a Uk. 109)**

Katika mfano 38, muuzaji aliwakaribisha wanunuzi katika kauli 1. Makaribisho ni njia mojawapo ya kufanya wanunuzi wahisi huru njia ya unyenyekevu ya kufungua mazungumzo (Liddicoat, 2007). Katika mfano 39, M<sub>m</sub><sub>z</sub>8d alimkaribisha S<sub>m</sub><sub>N</sub>11d kwa kumwamkua. Baada ya salamu, mazungumzo ya kawaida yaliendelea ambapo S<sub>m</sub><sub>N</sub>11d na M<sub>m</sub><sub>z</sub>8d walijadili bei ya miraa hadi mwishoni akanunua na kuondoka.

#### **Mfano 39;**

1. M<sub>m</sub><sub>z</sub>8d: Sema my brother (sema ndugu yangu)
2. M<sub>m</sub><sub>z</sub>8d: hii miraa mzuri kabisa
3. S<sub>m</sub><sub>N</sub>11d: haina maji?
4. M<sub>m</sub><sub>z</sub>8d: Hapana haina maji hata

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo d Uk. 116)**

#### **4.4.7 Matumizi ya Misamiati ya Biashara**

Mkakati mwingine wa unyenyekevu uliotumika katika mazungumzo katika biashara ya miraa, ni matumizi ya msamiati wa biashara. Kutumia lugha kutegemea muktadha maalumu kama alivyoeleza Brown na Levinson (1987), ni unyenyekevu kwani hupunguza nafasi ya kutokea mgogoro baina ya wazungumzaji. Wazungumzaji hutambua mazingira waliyopo na hivyo kubadilisha nadhari yao ikawa ya muktadha ule tofauti na mahali pengine kijamii. Mkakati huu ulitumiwa kwa asilimia 6.5% na 11.6% na wanunuzi na wauzaji mtawalia.

Katika **mfano 40**, baada ya  $SM_{N1g}$  kutaja kiwango cha pesa alichokuwa nacho,  $MM_{Z1g}$  alimweleza kuwa hawezi kusema hivyo katika kauli 2. Kauli hiyo ya  $MM_{Z1g}$  ilikuwa ni njia ya upole ya kusema kuwa pesa aliyoitaja  $SM_{N1g}$  ilikuwa kidogo sana ikilinganishwa na bidhaa aliyohitaji kununua. Katika kauli ya 3,  $MM_{Z1g}$  alizidi kutumia mkakati wa unyenyekevu ambapo alimnong'onezea  $SM_{N1g}$  kuwa angemuuzia ile bei kwa hisani bali asimweleze mnunuzi mwingine kuwa alinunua bei ile pale. Iwapo angehisi kuwa alifanyiwa mapendeleo basi angeondoka pale dukani huku amefurahia na huduma. Huu ni mkakati chanya wa unyenyekevu.

#### **Mfano 40,**

1.  $SM_{N1g}$ : 1500 mimi iko nayo
2.  $MM_{Z1g}$ : Aaa huwezi sema hivyo *my brother*. 1500 kidogo sana (( baada ya kuzungumza na wauzaji wengine kwa dakika moja))
3.  $MM_{Z1g}$ : *Wariah* umeamua aje:((Kwa sauti ya chini)) Elfu mbili leta na usiseme nimekuuzia hiyo bei

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 121)**

Katika **mfano 41**,  $Mm_{Z8d}$  alimwamkua na kuzidi kuisifu bidhaa yake kwa mnunuzi  $SM_{N11d}$  alipiga hatua mbele kumshawishi kuwa bidhaa yake ni nzuri na safi (kauli 2, 4 na 7).  $Mm_{Z8d}$  alichukua miti michache kutoka kwenye kifurushi alichokuwa anamwonyesha  $SM_{N11d}$  akatafuna katika kauli 2 ilimradi amdhihirishie kuwa ilikuwa mikavu na wala haikuwa na maji kama alivyosema  $SM_{N11d}$  kuwa hakutaka miraa ambayo ilikuwa na maji.  $Mm_{Z8d}$  alimuuliza maswali ya balagha katika kauli 6,7 na 8. Maswali haya yaliulizwa ili kumchochea  $SM_{N11d}$  kufikiria na kuamini kuwa bidhaa ile ilikuwa safi kabisa.

## Mfano 41,

1. Mm<sub>z</sub>8d: *Sema my brother* (sema ndugu yangu)
2. Mm<sub>z</sub>8d: hii miraa mzuri kabisa((akichukua miti michache na kuanza kuitafuna))
3. Sm<sub>N</sub>11d: haina maji?
4. Mm<sub>z</sub>8d: Hapana haina maji hata
5. Sm<sub>N</sub>11d: haiya haiya haiya
6. Mm<sub>z</sub>8d: Kwani unataka miraa kavu?
7. :Hii iko na maji?
8. :Wewe iko meno si ndio?
9. Sm<sub>N</sub>11d: aa hii ni safi
10. Mm<sub>z</sub>8d: Mbili?
11. Sm<sub>N</sub>11d: Nifunge hii moja eeh
12. Mm<sub>z</sub>8d: Haya sawa *Engineer*.Sawa brother (sawa ndugu) ((mnunuzi anaondoka))

### (Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo d Uk. 115)

Matendo ya Mm<sub>z</sub>8d yalikuwa ni matumizi ya lugha ya biashra kwa nia ya kumshawishi Sm<sub>N</sub>11d anunue bidhaa yake, na mwishoni alifanikiwa kumuuzia kwani aliagiza afungiwe katika kauli 10.

Katika **mfano 42** hapa chini, SM<sub>N</sub>13e alisema katika kauli 3 kuwa miraa ilikuwa *kama dawa*. Kwa kumpongeza SM<sub>N</sub>13e, muuzaji MM<sub>z</sub>9e naye alimweleza kuwa aliona kuwa ye ye alifahamu maana ya miraa (kauli 2) kwa sababu alichagua kifurushi kizuri kati ya alivyokuwa akiviiza MM<sub>z</sub>9e .

## Mfano 42,

1. SM<sub>N</sub>13e: xxxxxx.
2. MM<sub>z</sub>9e : Mimi najua, naona wewe unajua maana ya miraa wewe
3. SM<sub>N</sub>13e: Miraa kama dawa
4. MM<sub>z</sub>9e: Haya sawa baba aye
5. :((Akizungumza kwa simu)) Kilo mbili giza?
6. : Sawa sawa baba

### (Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 117)

Katika **mfano 43** SM<sub>N</sub>1g na MM<sub>z</sub>1g walilalamika kuwa kuna ukame na kuwa mambo ni magumu. Lengo la MM<sub>z</sub>1g lilikuwa ni ili auze miraa yake kwa bei iliyomletea faida. Kwa upande wake, SM<sub>N</sub>1g lengo lake lilikuwa ni ili MM<sub>z</sub>1g amhurumie “kwa kuwa kulikuwa na ukame na MM<sub>z</sub>1g alikuwa anaelewa,” ili akubali hela chache alizokwu na zo. Wote walizingatia lugha ya biashara ili kufanikisha mazungumzo baina yao, kila mmoja wao akitaka kuivuta kamba kwake.

### **Mfano 43,**

1. SM<sub>N</sub>1g: iko ukame si unaelewa?: eeh najua. Ukame iko kila mahali
2. MM<sub>Z</sub>1g: 2700 leta
3. SM<sub>N</sub>1g: 2700 mingi, mingi sana
4. MM<sub>Z</sub>1g: Hapana si mingi *brother*
5. :Sahii mambo ni ngumu, ngumu sana

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 121)**

Katika **mfano 44**, muuzaji alichukua vipande vichache vyaa miraa na kumkabidhi mnunuzi SM<sub>N</sub>1g atafune ili aridhike na bidhaa ambayo alitaka kununua. MM<sub>Z</sub>1g pia yeye alitafuna ili adhibitishie mnunuzi kuwa miraa ilikuwa miororo kama alivyopenda mnunuzi. Tendo la MM<sub>Z</sub>1g kumpa mnunuzi miraa achague aliyoipenda (kauli 1, 6) pia lilikuwa ni unyenyekevu kwa upande wa muuzaji, kwa sababu mnunuzi angeondoka pale dukani akiwa amefurahishwa na huduma. Kufurahi huku ndiko kungemfanya arejee pale dukani siku nyingine kununua na pia kuwapendekezea rafiki zake kununua katika duka hilo. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti wa awali wa Marriott (1993) aliyeleza kuwa huduma njema huwa ndilo lengo la kila mwanabiashara. Kupata na kupokea huduma njema hunawirisha biashara.

### **Mfano 44,**

1. SM<sub>N</sub>1g: Leta ingine bwana, hii mimi siwezi: achana na hii bwana mimi siwezi
2. MM<sub>Z</sub>1g: hii ni ngumu((akichukua kijiti kimoja kutoka kwa kifurushi alichokuwa akimwonyesha muuzaji na kuanza kutafuna))
3. MM<sub>Z</sub>1g: Tafuna miraa kwanza, huwezi kuangalia miraa kwa macho na useme ni ngumu
4. MM<sub>Z</sub>2g: hata hii ni safi sana
5. MM<sub>Z</sub>1g: hii ni ngumu?miraa migumu inakaa hivi?:Hiyo siyo ngumu.
6. SM<sub>N</sub>1g: Tafuta ingine...
7. MM<sub>Z</sub>1g: Tafuna miraa kwanza(akimpa vipande vichache vyaa kutafuna) :huwezi kuangalia miraa kwa macho na kusema miraa ni ngumu..

### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 120)**

Kwa hivyo, matumizi ya lugha ya biashara katika mazungumzo ya baina ya wauzaji na wanunuzi ulikuwa ni mkakati muhimu wa unyenyekevu uliotumika ili kudumisha wateja na kufanikisha mauzo kwa lengo la kujipatia mtaji hasa kwa wauzaji. Matumizi ya mkakati huu pia unatia nguvu utafiti wa awali wa King'ei (2010), kuwa sharti utoaji huduma uwe na nia ya kumridhisha mpokeaji huduma hiyo.

#### **4.4.8 Upungungakaji wa Unyenyekevu**

Maoni ya Brown na Levinson (1987) kuhusu upungukaji wa unyenyekevu ni kuwa washiriki wa uzungumzi hudhibiti hisia zao mradi kutotofautiana na kutowaudhi washiriki wenzao wanaotaka wachukue msimamo wao. Katika kufanya hivi, wazungumzaji wanaweza wakakubaliana na semi ambazo zimetolewa na wengine (ijapokuwa wakati mwingine kishingo upande) ili kuepuka migogoro ya kimazungumzo. Kama mkakati wa unyenyekevu, mzungumzaji hujaribu asitofautiane na mzungumzaji mwenzake anayeonekana kushinikiza mawazo yake kwake. Katika mazungumzo wa biashara ya miraa, mkakati huu ulidhihirika kimatumizi kwa asilimia 15.6% na 10.9% na wanunuzi na wauzaji mtawalia. Katika mifano ifuatayo watafiti walijadili na kutoa mifano katika mazungumzo ili kuonyesha mara ambapo upungukaji wa unyenyekevu ulionekana;

#### **Mfano 45,**

1. ((akimkabidhi MM<sub>z</sub>9e noti la shilingi elfu moja))
2. SM<sub>N</sub>13e:xxxxx, unaiza pesa ngapi hii,
3. MM<sub>z</sub>9e : Unanipatia pesa ngapi hii,
4. : Mimi nauza miraa 12,((1,200))
5. SM<sub>N</sub>13e :Sasa mimi niko na mia saba
6. MM<sub>z</sub>9e : Enda ukununue mia saba. sitaki hiyo mimi.
7. MM<sub>z</sub>9e: Giza achana nayo wewe chukua kangeta wewe bwana. Ukiona hiyo ni nyngi ((1,200))...
8. :ai acha bwana Nimesikia XXX akisema. Sio mimi
9. MM<sub>z</sub>9e: Achana basi nayo basi baba. Achana na Giza nunua kangeta basi.

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 118)**

Katika mfano 45, MM<sub>z</sub>9e alimpendekezea SM<sub>N</sub>13e anunue *Kangeta* kama hangeweza kununua *giza*. Katika kauli 7 MM<sub>z</sub>9e alimweleza SM<sub>N</sub>13e aachane na miraa iliyoghalli na achukue ya pesa zake zilivyokuwa ambayo ilikuwa *kangeta*. Kutolea mnunuzi wazo alikofanya MM<sub>z</sub>9e ilikuwa ni unyenyekevu kwani hakutaka kumwambia SM<sub>N</sub>13e kuwa pesa yake haikutosha na kuwa aondoke. Alimpa nafasi ya kuamua iwapo alipenda kutumia miraa mingine ambayo iligharimu pesa iliyoshabihiana na aliyokuwa nayo. Iwapo SM<sub>N</sub>13e angekubali kuchukua miraa aliyopendekezewa, angekuwa amefanya vile kwa hiari, kwa kuzingatia wasia wa MM<sub>z</sub>9e bila kushinikizwa. Kwa hivyo, kutoa wazo kwa MM<sub>z</sub>9e kuwa SM<sub>N</sub>13e achukue *Kangeta*, hakukumaanisha kuwa hela alizokuwa nazo SM<sub>N</sub>13e si za thamani au zilikuwa kidogo, bali ni kuwa miraa aliyokuwa akihitaji kununua ilikuwa ghali. Hata kama MM<sub>z</sub>9e alijua kuwa pesa ya SM<sub>N</sub>13e ilikuwa

kidogo ikilinganishwa na bidhaa aliyotaka, MM<sub>z</sub>9e hakumweleza SM<sub>N</sub>13e waziwazi bali alitumia njia ya mzunguko kusema vile. Huu ulikuwa mkakati wa unyenyekevu.

#### Mfano 46,

1. MM<sub>z</sub>9e: Hii haiwezi hata ukiimba. Hata uende pale uimbe wimbo wa kisomali siwezi
2. MM<sub>z</sub>9e: Unanunuanga pesa ngapi
3. SM<sub>N</sub>13e :Aki Mungu moja
4. MM<sub>z</sub>9e: Unanunuanga pesa ngapi? Acha kuniambia Mungu moja.

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 119)**

Katika **mfano 46**, SM<sub>N</sub>13e aligundua kinaya katika usemi wa MM<sub>z</sub>9e ndiposa alisema “Mungu moja” katika kauli 3. Katika kauli 1, baada ya MM<sub>z</sub>9e kumweleza SM<sub>N</sub>13e kuwa hawezি kumuuzia kwa pesa alizokuwa nazo, MM<sub>z</sub>9e alimuuliza huwa ananunua pesa ngapi. Huku kusaili SM<sub>N</sub>13e ili afahamu ni pesa ngapi yeye hununua katika maduka mengine, ilikuwa ni njia tu ya kutaka kumwelewa mteja wake ili amshawishi anunue kutoka kwake. Pia MM<sub>z</sub>9e kutumia maneno yasiyo ya waziwazi kusema kuwa hatamuuzia SM<sub>N</sub>13e katika kauli 1,ni mkakati wa unyenyekevu.

#### Mfano 47,

1. MM<sub>z</sub>9e :Basi acha
2. :Mimi nimekataa pesa yake.
3. SM<sub>N</sub>13e: Murithi wewe ndiye unanisumbua.
4. MM<sub>z</sub>10e: Yako si pesa. Pesa yako inanuka.
5. SM<sub>N</sub>13e:Pesa yangu inanuka sivyo? Wewe utaona kama utanipata hapa kesho
6. MM<sub>z</sub>9e: Tuma wewe utoke kwa nyumba
7. : XXXXXX toka upeleke nuksi(usumbufu) zako huko.  
Kisirani wewe
8. (( SM<sub>N</sub>13e Anaondoka.))  
Maongezi ya kando ((MM<sub>z</sub>9 watu kama hawa ni wezi hawa, wanaweza wakakuchanganya hadi miraa ipottee. Na ukiuzia wane kama hawa utachoka sana akili))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 120)**

Katika **mfano 47**, MM<sub>z</sub>10e alimwambia SM<sub>N</sub>13e kuwa pesa zake zinanuka. Kwenye kauli 4, SM<sub>N</sub>13e alirudia kauli ile ili kupunguza makali ya maneno yale, huku akitishia kutorudi pale dukani kununua tena keshoye.

#### 4.4.9 Matusi

Kulingana na Yule (1996), matusi ni mojawapo ya mikakati ya unyenyekevu chanya inayotumika na watu ambao wana uhusiano wa karibu au ambao wangependa kudumisha urafiki. Katika mazungumzo ya biashara ya miraa, matusi yalitumika kwa

wingi na watu ambao walikuwa ‘wamezoeana’. Katika mijadala ya vikundi viini, watafiti walibainisha kuwa matusi hayakuudhi waliotukwa.

42. MTF: Lakini lugha ya wanaume na wanawake hufanana, au ni tofauti na ya wanawake?
43. JIBU LA WENGI: **ni same ! ni same!**
44. MM003A: **Kwanza wamama ndio wanatukanana zaidi**
45. SM001A: Hao kwanza ndio wako na matusi hapa((akiashiria kwenye midomo))matusi yao!...
46. SM002A: “**Ayee si utupatie miraa mbwa wewe!” wanasema hivyo**
47. MTF: Je wanapokuja kununua,huja na kutanguliza kuongea kwa salamu kama mambo-poa n.k.?
48. SM002A: Hakuna kawaida hapo, customer akikuja kwangu aanze hizo story za mambo,habari za watoto,najua hana pesa.
49. MM002A: Hiyo ni ya kuuza nguo ama vitu zingine, ama anakuja kukopa
50. SM001A: Huyo ni mtu hana shilingi, hana pesa
51. MM003A: Huyo ameamua hiyo siku kukopa
52. MM001A: Huyo mtu hana pesa. Mtu ako na pesa anakuja anagonga meza na kukwambia, Mbwa niuzie miraa, na siombi!
53. MTF: Na hiyo ndiyo kawaida yenu?
54. MTF: Lakini huo ni unyenyekevu kweli?
55. MM001A: Ee ni unyenyekevu ya ajabu
56. SM002A: Wamezoea. Ni tabia yao yaani.
57. SM001A: Pia sisi(wanunuzi) tunajua ni kawaida na tuko sawa
58. MM001A: Hakuna mtu huchukulia au husikia vibaya
59. SM003A: Mahali mtu huwa hatukanani mtu huwa haendi, mahali mtu ataenda kununua na kukaa tu na hatukanwi, miraa haitashika
60. JIBU LA WENGI: Ee ni kawaida kabisaa

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 125)**

Kutokana na kauli 55 kutukanana katika biashara ya miraa kulionyesha unyenyekevu wa ajabu. Pia, katika kauli 59, iwapo mnunuzi alienda dukani ambapo hakukuwa na matusi hakupendelea kurudi pale kwa sababu huenda miraa haikuwa mizuri na hata ‘haingeshika.’ Matokeo haya yanakubaliana na aliyoyaeleza (Yule, 1996).

Pia, walihisi kuwa lugha ya wanaume na wanawake ilifanana na kuwa wanawake walitukanana kwa urahisi kama wanaume walivyotukanana (kauli 45,46, na 47). Haya

ni matokeo yanayokiuka tafiti za awali kuwa wanawake hutumia lugha ya upole na unyenyekevu kuliko wanaume (Eckert & McConnell-Ginet, 1992). Waliokosa kutumia lugha ya matusi walionekana kutokuwa na unyenyekevu katika mazingira hayo ya biashara ya miraa kwa sababu walitenda kinyume na yaliyozoleka na wengine. Walibezwa na kusemwa kuwa, “hawana kakitu” au walitaka kukopa miraa.

61. SM002A: Hakuna kawaida hapo, customer akikuja kwangu aanze hizo story za mambo, habari za watoto, najua hana pesa.
62. MM002A: Hiyo ni ya kuuza nguo ama vitu zingine, ama anakuja kukopa
63. SM001A: Huyo ni mtu hana shilingi, hana pesa
64. MM003A: Huyo ameamua hiyo siku kukopa
65. MM001A: Hyo mtu hana pesa. Mtu ako na pesa anakuja anagonga meza na kukwambia, Mbwa niuzie miraa, na siombi!

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 127)**

Matumizi ya matusi yalichukua asilimia ya wastani 5.2% na 4.2% ya mikakati ya unyenyekevu iliyotumika biasharani. Waliotumia matusi, walitaka kuonekana kama wamilisi wa lugha ya pale biasharani na pia ili wajitambulisha na wanakikundi-shiriki wa biashara ya miraa (in-group identity). Matokeo haya yanatia nguvu yale ya awali ya Yule (1996) ambaye alisema kuwa wanaume haswa, ndio hutumia matusi ili kujitambulisha na wanakikundi wenzao. Waliotukanwa nao, hawakuwa ni wageni bali ni watu (wanunuzi au wauzaji) waliopata kutangamana kwa wakati mrefu hivyo kujenga urafiki na pia mazoeano. Matokeo haya yalikubaliana na yale ya utafiti wa Miriti (2012) ambaye alibainisha kuwa Wameru na Wasomali hutumia matusi katika soko la miraa. Alifafanua kuwa, hakuna kikundi chochote kilihisi kuwa kimedhurika kihisia walipopokea au kutoa matusi kutoka kwa wenzao. Mukuni (2015), kwa upande wake aligundua kuwa Waembu katika soko la miraa la Kiritiri walitumia matusi kama mkakati maalumu wa kutaka kupunguziwa bei ya miraa, kwa sababu kutumia matusi kulimuunganisha mnunuzi na wanakikundi wengine wa miraa.

Katika utafiti huu, matumizi ya matusi yalitumiwa kwa wingi na wanaume, ambao walikuwa ni washiriki wakuu biasharani wakilinganishwa na wanawake.

1. SM001A: [Hata kama unaniuzia miti mbaya]. Hata kama natoka huko Meru kwa kukula kioski na nimekuta mmekaa chini nimeanza kukula miraa... na kama mimi haijanibamba, lazima nimtusi huyo mtu....
2. JIBU LA WENGI:ee
3. MM001A: **Kila matusi haikuwangi kwa ubaya. [Hiyo matusi**
4. SM002A: **[Si ubaya... hapo hakuna ubaya**
5. MM001A: Mimi hukuanga **side** ya kutukana lakini haikuwangi kwa ubaya  
 ((kicheko cha wote))
6. MM001A: Na tena haishiki. Mkiongea vizuri kama watu wanauziana nini, haitashika hiyo miraa. matusi isipokuwa .. hapo kazi hakuna.
7. SM002A: **Pia yeye lazima mwenye ananunua atukanane**
8. MTF: mbona?
9. SM002A: Anaona hiyo kutukanana si kitu..
10. SMM003A: **Kesho pia niko hapo kwa hapo nakwambia kumamako jana ulinipatia miraa aina gani?**  
 (( wote wanacheka))
11. SM003A: Unasikia? Hapo hakuna kitu...
12. MM002A: **Haikuwangi matusi ya roho mbaya. Saa ingine inakuwa for fun.**
13. SM001A: **haikuwi kwa roho mbaya ama nini... maanake ni kwa mdomo tu... ni kama anaenjoy**
14. MM001A: Hakuna mwenye huchukulia kama ni offence
15. SM002A: Cheki hakuna kufanya hivyo kwa mtu wowote
16. SM001A: **Hakuna kitu unaweza ukafanya bila. Hakuna kuomba.** Lakini yule mtu hajui anaweza fikiria mambo mbaya  
**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 124)**

Kulingana na wanakikundi, matusi yalifanya miraa iwapendeze watafunaji (kauli 6). Wanunuzi wasipotukanwa, waliamini kuwa walichouziwa kilikuwa cha thamani ya chini.

MM001A: **Na tena haishiki. Mkiongea vizuri kama watu wanauziana ninii, haitashika hiyo miraa. matusi isipokuwa .. hapo kazi hakuna.** **(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini A Uk. 124)**

Maoni ya wanakikundi wengine yalidhihirisha haya.

7. MTF: Je, mbona kuna matusi mengi katika mazungumzo?
8. MM003B: Matusi zingine ni za kukusifu. ((kicheko))
9. MM001B: mimi naweza sema, kulingana na lugha zote mbili-wasomali na wameru huwa kuna matusi. Kwa wameru enyewe unajua matusi ni kama kitu ya kawaida, na kwa wasomali pia matusi ni kama kitu cha kawaida. Sasa kwa ile biashara, inakuwa ni kama ni ya watu ambao wako na vitu zinarelate, kwa sababu wote wamezoea kutusiana. Kwa hivyo, hata matusi ikitolewa, hakuna mwenye anaona matusi ikiwa kitu kubwa.
10. MTF: Na matusi hazuui biashara kuendelea kwa sababu wamedhuriwa kihisia?
11. JIBU LA WENGI: **Aii hapana..hakuna kitu kama hiyo**
12. MM002B: Noo matusi haiwezi kuzuia biashara kuendelea..
13. MTF: Hatasema kwamba umenitusi sitakuja kununua kwako tena?
14. SM003B: **hapana.Kwanza ukimtukana ndio atakuja tena hata kesho yake. Hata ukitupa pesa yake huko kwa barabara, ataenda achukue ile pesa na aongezee nyingine hadi itoshe yenye unataka.hawezi jali, na hataenda kwa mwingine mwenye anauza miraa, atanunua hapoa hapo kwako tu.**

**(Rejelea kiambatisho cha Mjadala wa Kikundi Kiini B Uk. 139)**

#### **4.4.10 Kushukuru na Maagano**

Mtafiti alichanganua mikakati hii miwili kwa pamoja kwani mara nyingi shukrani zilitolewa na wauzaji au wanunuvi baada ya kupokea huduma, kisha wakaaga na kuondoka. Katika maingiliano baina ya wauzaji na wanunuvi katika biashara ya miraa, washiriki walitumia maneno ya kushukuru na kuaga kama mikakati ya unyenyekevu. Asilimia 6.5% na 7.2% ya wanunuvi na wauzaji walishukuru mtawalia. Wanunuvi na wauzaji walifunga mazungumzo kwa maagano ya asilimia 9.5% na 5.8% mtawalia. Matamko mengi ya wanunuvi yalizingatia misamiati iliyasheria shukurani baada ya kuuziwa. Maneno kama vile; *aye, sawa boss, kesho, poa* yalitumika. Kushukuru kulidhihirisha kuwa wanunuvi waliridhika na kupendezwa na huduma waliyopewa na kwa hivyo walitumia mkakati wa unyenyekevu wa kushukuru. Kulingana na Brown na Levinson (1987), shukurani huwa ni mkakati wa unyenyekevu chanya. Kwa hivyo, kushukuru kulikuwa ni njia moja ya kuleta makubaliano baina ya muuzaji na mnunuvi.

Maagano hutokea pale ambapo mazungumzo baina ya washiriki hufika kikomo, baada ya kila mmoja wao kusaidika na kutimiza mahitaji yake ya kimaingiliano (Grundy , 2000). Katika biashara ya miraa, lililowaleta pamoja washiriki ni kununua na kuuza miraa. Mkakati huu wa unyenyekevu ultumika kwa asilimia 9.5% kwa upande wa wanunuzi, na asilimia 5.8% kwa wauzaji. Asilimia hizi zilionyesha kuwa wanunuzi ndio walioaga kwa wingi, kwani walihisi kuwa wao ndio walikuwa wamepata usaidizi. Nao wauzaji waliwaaga wanunuzi wao, ilimradi wawakaribishe kununua kutoka kwao siku iliyofuata au ili wanunuzi wao wahisi kuwa muuzaji alishukuru kwa kununua kutoka kwao. Kuaga kulikuwa ni njia mojawapo ya kuonyesha unyenyekevu kwani kulisisitiza kujali maslahi ya mwenzake, kwa kutotaka mazungumzo yaktike tu kwa ghafla .

#### **Mfano 48,**

1. SM<sub>N</sub>1g: Xxxxxx ni hivyo? Ni xxxxxxxxx?
2. MM<sub>Z</sub>1g: Wee hapana nani anaitwa xxxxxx hiyo pesa imeenda kwa kikuyu wewe bwana
3. SM<sub>N</sub>1g: itarudi tu. Sawa lakini?
4. MM<sub>Z</sub>1g: Eeh ni sawa. Tutaonana siku ingine Mungu akipenda eeh
5. SM<sub>N</sub>1g: Eeh sawa((huku akiondoka))

#### **(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo g Uk. 121)**

Katika mfano 48, alimweleza mwenzake katika kauli 10 kuwa wangeonana Mungu akipenda, na mwenzake kukubali katika kauli 11. Hata hivyo, kuna mazungumzo mengine ambayo yalikamilishwa kwa kutofautiana baina ya muuzaji na mnunuzi. Katika mfano huu, SM<sub>N</sub>13e alielezwa atume pesa kisha aondoke na MM<sub>Z</sub>9e. Fauka ya hayo, SM<sub>N</sub>13e aliamrishwa aondoke kwani pesa zake zilinuka na aondoe kisirani chake pale dukani. SM<sub>N</sub>13e alitisha katika kauli ya 5 kuwa hangefika pale dukani kesho yake kununua miraa tena.

#### **Mfano 49,**

1. MM<sub>Z</sub>9e :Basi acha
2. :Mimi nimekataa pesa yake.
3. SM<sub>N</sub>13e: Murithi wewe ndiye unanisumbua.
4. MM<sub>Z</sub>10e: Yako si pesa. Pesa yako inanuka.
5. SM<sub>N</sub>13e:Pesa yangu inanuka sivyo? Wewe utaona kama utanipata hapa kesho
6. MM<sub>Z</sub>9e: Tuma wewe utoke kwa nyumba
7. : Xxxxxx toka upeleke nuksi(usumbufu) zako huko.  
Kisirani wewe

8. (( SM<sub>N</sub>13e Anaondoka.)) Maongezi ya kando ((MM<sub>Z</sub>9 watu kama hawa ni wezi hawa, wanaweza wakakuchanganya hadi miraa ipotee. Na ukiuzia wanne kama hawa utachoka sana akili))

**(Rejelea kiambatisho cha Mazungumzo e Uk. 118)**

#### **4.4.11 Hitimisho**

Katika kuhitimisha sehemu hii, ilibainika kuwa wanunuzi na wauzaji katika biashara ya miraa, walitumia miundo mbalimbali katika mawasiliano yao. Kwa upande mmoja kuna waliofungua mazungumzo yao kwa salamu na kuaga baada ya kupata huduma. Na kwa upande mwingine, kuna waliokosa kufungua kwa salamu wala kushukuru baada ya huduma. Hata hatua hizi za muundo zilipokosa kuwepo, haikuonekana kama kulikuwa na ukiukaji wowote wa muundo wala kuhujumu mawasiliano. Kulingana na washiriki iwapo mnunuzi alikuwa na haraka sana alihudumiwa na kutoamkua kwake hakukuwa na tatizo lolote. Muundo wa zamu ulibadilika kulingana na idadi ya wanunuzi waliofika dukani kwa kipindi kimoja. Zamu zingine zilitokea kwa hatua zilizo sahili, na nyingine zikatokea zikiwa zimechangamana (pale ambapo zilisubirishwa na kurejelewa baadaye). Washiriki waliepushiana soni kwa kuzingatia mikakati mbalimbali ya unyenyekevu kama vile; kuomba, kutumia misamiati ya kibiashara, kuamkua, kuaga, kushukuru ili wasionekane kama ambao walishinikiza wenzao kutenda jinsi walivyopenda. Washiriki walibaini ya kuwa katika biashara, kuna upande mmoja unaotoa huduma, na upande wa pili ukipokea huduma hizo. Hivyo kulikuwa na kutegemeana na sharti kila aliyeshiriki katika uzungumzi aridhishwe.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Katika sura hii, kama njia ya kuhitimisha tasnifu, dhana tafitiwa na zinazojibainisha katika sura tangulizi yanaangaziwa. Mtafiti anawaelekeza wasomaji wake kimuhtasari kulingana na malengo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafit wa baadaye.

#### **5.2 Muhtasari wa Matokeo**

Matokeo ya utafiti huu yalielezwa kulingana na madhumuni ya utafiti.

Katika lengo la kwanza, mtafiti alidhamiria kuchunguza muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi katika biashara ya miraa. Vipengele muhimu viliwyochunguzwa ni vifunguzi, ubadilishanaji zamu, ukataji kalima, urekebishaji na maagano.

- a) Ilibainika kuwa salamu kama ishara ya kufungua mazungumzo zilikuwepo na mara nyingine kutokuwepo. Jinsi salamu zilitolewa na washiriki, zilitegemea sana uhusiano uliokuwepo baina ya muuzaji na mnunuzi. Mara nyingine walipenda kujitambulisha na desturi za wanakundi-ndani ndiposa mara nyingine wakatumia hata matusi au kugonga meza. Matokeo haya yalikubaliana na aliyoeleza Yule (1996) kuwa wanakundi-ndani huamua na huwa na ufahamu wa sheria na kanuni zinazoongoza mazungumzo yao.
- b) Mazungumzo yalichukua miundo mbalimbali kutegemea wanunuzi waliohitaji msaada wa muuzaji kwa wakati mmoja hivyo kukaibuka zamu sahili na changamano. Zamu changamano zilikuwa zinakatizwa au kuwachwa wazi kwa muda iwapo wateja walikuwa wengi na kurejelewa baada ya kumaliziwa kwa mteja mmoja. Kusubirisha kwa zamu (kauli) hizi kulikuwa kwa makusudi kwani muuzaji angekosa kufanya vile angekanganyika na kukosa kupata pesa baada ya mauzo. Jukwaa la mazungumzo lilimilikiwa na wanunuzi wote, zamu hazikuzingatiwa na ukatizanaji wa kauli ulidhihirika.

Kuhusu lengo la pili, mtafiti alikusudia kutathmini namna ukabila na jinsia ya washiriki iliathiri muundo wa mazungumzo.

- a) Ilibainika kuwa kibadiliki cha jinsia kiliathiri muundo wa mazungumzo kwani wanawake walitumia sentensi fupifupi na sauti ya upole wakati mwingine ikilinganishwa na wanaume walitumia sentensi kavu na kuamrisha kwingi kila wakati. Wanunuzi wa kiume walimiliki jukwaa la mazungumzo na walikatana

kalima kwa wingi. Matokeo haya yalithibitisha yaliyoandikwa hapo awali na Coates (2013).

- b) Kwa kuwa wanaume ndio waliothibiti mazingira ya kibiashara, wazungumzaji wa kike walitoa kauli chache. Wanaume wa Kisomali kwa upande wao walikatiza kauli kwa wingi na kurekebisha kauli zao walipogundua kuwa zilikuwa na makosa au kudhuru hisia za wauzaji (Wameru). Wanunuzi wa Kisomali waliaga na kushukuru baada ya kupata huduma wakilinganishwa na wanaume wanunuzi kutoka jamii ya Wameru. Vigezo vyta ukabila na athari yake kwa muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi pia vilichanganuliwa katika lengo hili. Ilitambuliwa kuwa jinsia ya kiume kutoka jamii zote mbili (Wasomali na Wameru) ndio waliodhibiti biashara ya miraa ikilinganishwa na wanawake. Hali hii ilitokana na mipangilio ya kihistoria ya kijamii hasa ya Ameru (Carrier, 2007).
- c) Wanawake wachache sana walishiriki katika uuzaaji na utafunaji wa miraa. Wanawake walionunua, mara nyingi walikuwa hawajui miraa iliyo mizuri na waliishia kununua iliyo mibovu. Wanawake kutoka jamii zote mbili walitekeleza wajibu wa kiusaidizi kama vile upishi wa chai, uuzaaji wa maji, peremende, mifuko ya kufungia miraa au vitafunio vingine kama njugu karanga.
- d) Wanawake walitumia lugha iliyojaa mahaba walipowauzia wanaume ili wawapumbaze kifikra kusudi wanunue miraa yao iliyo ‘mibovu’. Wanawake wa jamii ya Kisomali waliuza miraa kwa wingi japo ilikuwa miraa ya bei iliyo ya chini ikilinganishwa na iliyouzwa na wanaume kutoka jamii ya Ameru.

Hata hivyo wanakikundi walikubaliana kuwa lugha ya wanawake na wanaume ilikuwa sawa na yenye matusi hivyo kukiuka baadhi ya sifa za utafiti wa awali kuwa lugha ya wanawake ni safi na sanifu na yenye unyenyekevu.

Katika lengo la tatu, mtafiti alichunguza mikakati ya unyenyekevu iliyotumika baina ya wazungumzaji na namna vigezo hivyo vilivyodhihirishwa na washiriki kutoka kabilalilivyojitekeza katika mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuzi wa biashara hiyo pia ulichunguzwa.

- a) Ilibainishwa kuwa mikakati ya unyenyekevu iliyotumika ni pamoja na: kutaja kwa heshima k.v. *boss, brother, engineer, ndugu, baba, mzee*, kuamkua washiriki wengine.

- b) Washiriki walizingatia mikakati mingine k.v. kutumia vichekesho na utani iwapo walikuwa marafiki, kushukuru na kuaga baada ya kupata huduma pamoja na kubadilisha msimbo wakati walitaka kusema maneno yasiyofurahisha na ambayo yangezua soni kama njia mojawapo ya kuepushiana tahayuri.
- c) Ingawa tafiti za awali zilionyesha kuwa matusi yanatumika kwa wingi katika soko la miraa, utafiti wetu umebainisha kuwa katika biashara ya miraa, pia kuna kiwango kikubwa cha lugha ya heshima ambayo hutumika na washiriki. Tofauti na Miriti (2012), na Mukuni (2016), ambao walitafiti biashara ya miraa katika soko, utafiti huu ulihusisha wauzaji na wanunuzi katika maduka mahususi na kwa hivyo kulikuwa na mikakati ya unyenyekevu zaidi kuliko matusi. Ikikisiwa kuwa matumizi ya matusi katika soko yalikusudiwa kuvutia wateja kwa kuvuta nathari za wanaopita.
- d) Pia, ilibainika kuwa lugha ya matusi ilipotumika na wauzaji kwa wateja wao, (wateja) waliamini kuwa bidhaa waliyouziwa ilikuwa bora kuliko wakati lugha haikuwa na matusi.

Katika maduka yapatikanayo Eastleigh, kuna uhusiano wa karibu kati ya wauzaji na wanunuzi, jambo ambalo lilidhihirishwa na unyenyekevu kama vile maamkuzi, kushukuru, makaribisho na hata matumizi ya maneno ya heshima ya mtajo. Matusi yalikuwa ni mojawapo ya mikakati ya unyenyekevu ambayo walitumia kujitambulisha na washiriki wengine walio wa kikundi-ndani katika soko la miraa. Hivi kwamba waliozingatia lugha ‘safi’ na ya heshima walionekana kuwa ni wageni katika biashara au walikuja nia mbaya- ya kukopa miraa. Matusi, ingawa kwa kiasi kidogo yalitumika kama mkakati wa kuonyesha utangamano kwa ambavyo hakuna mshiriki aliyeonekana kukasirika baada ya maneno ya matusi.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu ni awamu ndogo tu katika uchanganuzi wa muundo wa mazungumzo na umebainisha utajiri wa kiisimu katika biashara ya miraa. Tasnifu hii inahitimisha utafiti huu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti ifuatavyo:

#### **5.3.1 Muundo wa Mazungumzo katika Biashara ya Miraa**

- a) Ilibainishwa kuwa muundo wa mazungumzo hubadilika kutegemea udharura ambao mnunuzi huwa nao anapofika dukani. Iwapo mnunuzi alikuwa na haraka sana, hakujikita katika baadhi ya hatua za mazungumzo kama vile salamu,

- ubadilishanaji zamu au urekebishaji kwa sababu alifika na kuomba miraa na kukabibidhiwa, kuikagua kuilipia na kisha kuondoka.
- b) Kwa upande mwingine, muundo wa mazungumzo ulikuwa taratibu iwapo mnunuzi na muuzaji walikuwa marafiki waliozoeana. Hali hii ilipotokea, palitokea zamu za karibu na za moja kwa moja. Kulikuwa na utani na vichekesho baina ya washiriki waliokuwa wamejenga uteja wa muda mrefu.
  - c) Jukwaa la mawasiliano lilimilikiwa na watu wote ndiposa kukatokea ukatanaji na ukamilishianaji wa kauli.
  - d) Muundo wa ubadilishaji zamu ulikuwa unazingatiwa hata kama wateja waliofika dukani walikuwa wengi kwa kipindi cha wakati. Hata kama zamu nyingine zilisubirishwa, mzungumzaji alizirejelea na kuziendelesha alipoziachia.
- Hali hii ilitokea pale ambapo mnunuzi alipokabidhiwa miraa na kuanza kuikagua huku amenyamaza. Baada ya kuikagua na kuamua miraa ambayo ataibeba, basi aliendelesha uzungumzaji wake na muuzaji ambaye wakati wote huu (wakati yule wa kwanza alikuwa akikagua na kufanya uamuzi ) alikuwa kimuuzia mteja mwingine. Matukio haya ya kukabidhiwa na kukagua kwa bidhaa kwa wateja wengi kwa wakati mmoja ndiko kulisababisha kuwepo kwa uchangamano wa zamu pamoja na ukatanaji wa kauli.
- e) Mtafiti aliwasilisha baadhi ya maneno yaliyotumika na washiriki katika kufungua maingiliano baina yao, kisha alieleza baadhi ya mipangilio ya upishanaji zamu baina ya washiriki. Mnunuzi alihakikisha kuwa aliyefika dukani na aliyehitaji huduma ya dharura alihudumiwa kwanza. Katika kufanya hivyo aliwahifadhi wateja wake. Kwa wale ambao walichelewa kukubaliana bei waliyoelezwa na muuzaji, hata kama walikuja saa moja kabla ya wanunuzi wengine, wale waliokubali bei ya miraa walihudumiwa kwanza na kuondoka. Muuzaji hakujali muda ambao mteja alisimama pale dukani mradi tu mteja huyo ali pe pesa ambazo alipaswa kulipa kabla ya kuibeba bidhaa. Kuna wateja ambao walipaaza sauti zao lakini hilo halikuzuia mnunuzi kuendelea kumhudumia aliyefika kwanza. Muuzaji aliendelea kumhudumia yule aliye kuwa akihudumiwa kwanza na aliyepaza sauti alibidika kusubiri zamu yake.
  - f) Maagano baada ya wauzaji na wanunuzi yalifanyika kwa uchache sana kwani baada ya huduma, wanunuzi waliondoka tu na kwenda zao. Muundo wa

mazungumzo katika biashara ya miraa hauzingatiwi kwa kina kwani shughuli zote zinazozingira bidhaa ya miraa hufanywa kwa upesi kwa sababu ya uharibikaji na upotezaji wa ladha wa miraa. Udharura huo huendelezwa hata katika harakati za uuzaji na ununuzi na huathiri muundo wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuizi.

- g) Utozingatiaji wa hatua za muundo wa mazungumzo kwa hivyo haukuzuia kukamilika kwa maingiliano mionganoni mwa washiriki wa biashara ya miraa. Ilibainika kuwa washiriki hawakujali hata hatua hizo za kimuundo zilipokosa kuzingatiwa.

### **5.3.2 Mikakati ya Unyenyekevu katika Biashara ya Mira**

Kimsingi inabainika kuwa washiriki wa biashara ya miraa walizingatia mikakati anuwai ya unyenyekevu ili kufanikisha utangamano wao bila migogoro. Mikakati hii ilitumiwa na wauzaji na vilevile wanunuizi. Kama ilivyoonyeshwa katika sura ya nne, asilimia ya utumizi wa mikakati hiyo ilibadilika badilika. Mikakati hiyo ilikuwa ni kama vile:

- a) Kuamkua wakati wa kufungua mazungumzo kama njia ya kulinda uhuru wa mtangamanaji-mwenza kupendelea kushiriki katika mazungumzo. Maamkuzi yalitekelezwa kwa njia tofauti kama vile kutaja jina la mshiriki iwapo walifahamiana, katika maingiliano mengine kuitisha miraa tu ilikuwa ni njia ya kuamkua.
- b) Matumizi ya msamiati wa kibiashara, kubadilisha msimbo ili kumwepushia mshiriki wa khabila jingine soni. Mkakati huu ulijitokeza sana kwa sababu maingiliano yaliyochunguzwa yalishirikisha washiriki wa jamii-lugha mbili tofauti. Kimsingi, washiriki hawa hutumia lugha mbili tofauti (Kimeru na Kisomali). Kubadilisha msimbo kutoka kwa Kiswahili hadi kwa lugha za kwanza baina ya washiriki basi ilikuwa ni njia moja ya kuwatenga wale ambao walikuwa wa jamii-lugha hiyo nyingine. Ilibainika kuwa kila walipochagua kubadilisha msimbo, walikusudia kutoa semi ambazo iwapo zingesemwa kwa Kiswahili, huenda zingewakera washiriki-wenza. Mkakati huu ulitumika kimaksudi ili kuepushiana tahayuri mionganoni mwa washiriki.
- c) Kushukuru baada ya kupata huduma, na kuagana baada ya kukamilisha mazungumzo ili kumpa muuzaji nafasi ya kuwashudumia wanunuizi wengine.

- d) Matumizi ya matusi kama mkakati maalumu, ulionyesha kuwa washiriki walifahamu matakwa ya wanakundi-ndani katika biashara ya miraa. Washiriki walifahamu na kukubali kuwa matumizi ya matusi katika biashara hii na waliotumia au kuyatoa walifanya vile kimakusudi ili wakubalike katika biashara hiyo ya miraa. waliopokea matusi nao kwa kutohisi kuwa tahayuri zao zilikuwa zimedhurika, ilikuwa ni ishara kuwa lugha katika biashara ya miraa ni legevu kama zilivyo sajili nyingine zisizo rasmi.

Utafiti wa tasnifu hii umefanikiwa katika kufafanua dhana ya unyenyekevu na unavyotekelawa na washiriki katika biashara ya miraa wajipatao katika mazingira sawa ya kimazungumzo katika jamii. Aidha, umefanikiwa katika kueleza muundo wa mazungumzo ya kibiashara.

#### **5.4 Mapendekezo Kutokana na Utafiti**

Baada ya kufanya uchanganuzi wa mazungumzo baina ya wauzaji na wanunuvi wa bidhaa ya miraa kwa minajili ya kupambanua muundo wa mazungumzo na mikakati ya unyenyekevu iliyozingatiwa na washiriki wa jinsia na ukabila tofauti, mtafiti anapendekeza yafuatayo:

- a) Kwanza, utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari ya umri kwa muundo wa mazungumzo baina ya washiriki wa makabila mawili yaliyochunguzwa.
- b) Pili, utafiti wa ziada kuhusu lugha inavyotumika wakati makabila mengine yanaposhiriki katika ununuvi na uuzaji wa miraa nchini Kenya.
- c) Tatu, utafiti kuhusu nafasi ya lugha ya matusi katika ufanikishaji wa biashara ya miraa katika jamii.
- d) Nne, kuwe na utafiti wa kina kuhusu nafasi ya lugha yenyeye mamlaka katika biashara ya miraa.

## MAREJELEO

- Anderson, D. M., Beckerleg, S., Hailu, D., & Klein, A. (2007). *The Khat Controversy: Stimulating the drugs debate*. Oxford: Berg Press.
- Baariu, N. S., & Malaku, C. G. (2015). Mapping (Khat) by Remote Sensing in Meru County, Kenya. *International Journal of Remote Sensing Applications (IJRSA)*, Volume 5, doi: 10.14355/ijrsa.2015.05.006.
- Beckerleg, S. (2009). Khat chewing as a new Ugandan leisure activity. *Journal of East African Studies*, 3(1), 42-54.
- Beckerleg, S., & Sheekh, N. (2005). A view from the refugee camps: new Somali Khat use in Kenya. *Drugs & Alcohol today*, Vol 5 issue 3 pp 25-27.
- Benard, F. (1972). *The East of Mount Kenya:Meru Agriculture in Transition*. Munich: Weltforum Verlag.
- Benveniste , E. (1971). *Problems in General Linguistics*. Coral Gables F.A.: University of Miami Press.
- Boyce, C., & Neale, P. (2006). Conducting In-depth Interviews: A Guide for Designing and Conducting In-depth Interviews for Evaluation Input. *Monitoring and Evaluation -2*, 1-16.
- Brown, G., & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis*. New York: Cambridge University Press.
- Brown, P., & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language usage*. Cambridge: Cambrige University Press.
- Brubaker, R. (1999). The Menichean myth: Rethinking the distinction between civic and ethnic nationalism. Kwenye K. A. In Hanspeter Kriesi, *Nation and National Identity*. Chur, Switzerland: Rugger publishers.
- Cameron, D. (2001). *Working with Spoken Discourse*. London: Sage Publishers.
- Carrier, N. C. (2007). *Kenyan Khat; The Social Life of a Stimulant*. Boston: Brill Leiden.
- Carrier, N. M. (2005). The Need for Speed: Contrasting time- frames in the social life of Kenyan miraa. *Africa*, 75(4) 539-558.
- Chanler, W. (1893). *Through Jungle and Desert :Travels in Eastern Africa*. London: Macmillan.

- Coates, J. (2003). *Men Talk : Stories in the Making of Masculinities*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.
- Coates, J. (2004). *Women, Men and Language : A Sociolinguistic Account of Gender Differences in Language; third edition*. London: Pearson Education Limited.
- Coates, J. (2013). *Women, Men and Everyday Talk*. London: Palgrave Macmillan.
- Coates, J. (2013). *Women, Men and Language: A Sociolinguistic Account of Gender Differences in Language (3rd ed)*. New York: Routledge Publishers.
- CRA. (2013). *County Budgets: 2013-2014*. Nairobi, Kenya: A Publication of the Commission on Revenue Allocation (CRA).
- Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches*. London: Sage publications Ltd.
- De Klerk. (1997). Expletives and Masculinity. *Johnson, Sally & Meinhof, Ulrike (eds)*, 144-158.
- Dornyei, Z. (2007). *Research Methods in Applied Linguistics: Qualitative, Quantitative and Mixed methodologies*. Oxford: Oxford University Press.
- Eckert, P. (2003). *Language and Gender*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Eckert, P., & McConnell-Ginet, S. (1992). Think practically and look locally :language and gender as community-based practice. *Annual Review of Anthropology*, 21:461-90.
- Edelsky, C. (1981). Who's got the floor? *Language in Society*, Vol 10 (3) pp. 383-421.
- Fraser, B. (1990). Perspectives on Politeness. *Journal of Pragmatics* 14(2), 219-36.
- Fromkin, V. (1971). The Non-Anomalous Nature of Anomalous Utterances. *Language*, 50-72.
- Garfinkel, H. (1967). *Studies in Ethnomethodology*. Engelwood Cliffs NJ: Prentice hall.
- Gee, J. P. (1999). *An Introduction to Discourse Analysis: Theory and Method*. Psychology Press.
- Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual: Essays on Face-Face Behaviour*. Garolen City, New York: Anchor/ Doubleday.
- GOK. (June 1996). *Catha Edulis (Mira)* : A Detailed Review focusing on Its Chemistry, Health Implication, Economic, Legal, Social, Cultural, Religious, Moral Aspects and Its Cultivation. Nairobi: National Council for Science and Technology; NCST NO.40.

- Goldsmith, P. (1988). *The Production and Marketing of Miraa in Kenya. In Satisfying Africa's food needs* (ed). R. Cohen, London: Lynne Rienner Press.
- Goldsmith, P. (1994). Symbiosis and Transformation in Kenya's Meru District. *Symbiosis and Transformation in Kenya's Meru District*. PHD Thesis University of Florida.
- Goody, E. (1980). *Questions and Politeness: strategies in social interaction*. Cambridge: Cambridge Press.
- Grice, H. (1975). Logic and Conversation. In P. Cole, *Syntax and Semantics* (pp. Volume 3 pp 113-127). New York: Academic Press.
- Grundy , P. (2000). *Doing Pragmatics 2ed*. London: Arnold Publishers.
- Gumperz, J. (1982). *Language and Social Identity*. United Kingdom: Cambridge University Press.
- Habwe, J. (2010). Politeness Phenomena: A Case of Kiswahili Honorifics. *Swahili Forum*, 17: 126-42.
- Hassan, A. (2000). *Communication in Intercultural Discourse. Unpublished M.A. Thesis*. Nairobi: Kenyatta University.
- Heritage, J. (1984). Conversation Analysis and institutional talk: analysing data. Kwenye D. Silverman, & (ed), *Qualitative Research: Theory, method and Practice* (kur. 161-182). London: Sage Publishers.
- Heritage, J. (1984). *Garfinkel and ethnomethodology*. Cambridge: Polity Press.
- Hjort, A. (1974). *Trading Miraa:From School Leaver to Shop Owner in Kenya*. Lausanne: The International Council on Alcohol and Addictions.
- Hjort, A. (1979). *Savanna Town: Rural Ties and Urban Opportunities in Northern Kenya*. Stockholm: The International Council on Alcohol and Addictions.
- Hoffman, C. (1991). *An Introduction to Bilingualism*. New York: Longman Inc.
- Hutchby, I., & Wooffit, R. (2002). *Conversation Analysis: Principles, Practices and Applications*. Cambridge UK: Polity Press.
- Jambi, C. (2015). An Analysis of Politeness Strategies in Gikuyu: A Case of Thika Sub-County, Kenya. *Kenyatta University a Unpublished Thesis*.
- Jefferson, G. (1973). A case of precision timing in ordinary conversation : overlapped tag-positioned address terms in closing sequences. *Semiotica*, 9: 47-96.
13. Mm<sub>z</sub>1j: nakuuliza umetoa 8th ama 12th?
14. ((Maongezi ya kando huku akikagua miraa))
15. Mm<sub>z</sub>2j: leo ni siku ya timu bry eeh
16. Mm<sub>z</sub>1j: ee oo leo ni siku ya timu kubwa ee?
17. Mm<sub>z</sub>1j ((akimzugumzia Mm<sub>z</sub>2j kwa lugha ya kwanza)) aaa i miraa e nguvu. Ina aumite na ii? (aaa hii ni miraa ya nguvu sana. Ametoa wapi hii?)
18. SM<sub>N</sub>1j: Unafanya miraa yangu nini?  
:eti unafanya namna hii[
19. Mm<sub>z</sub>2j: yaani atigwitikia (yaani haamini)
20. Mm<sub>z</sub>1j :Eti nafanya namna gani?

21. : pole. Pole.  
 22. SM<sub>N</sub>1j: wewe mzee wewe.  
 23. : wewe ongezea[ kidogo acha mambo ya pole.  
 24. Mm<sub>Z</sub>1j: pole.[  
 25. SM<sub>N</sub>1j: ongezea] wewe acha mambo ya pole. Kwani pole  
     ni msichana kwa kitanda?  
 26. : ongezea.  
 27. Mm<sub>Z</sub>1j :baadaye baadaye..( (akimkabidhi SM<sub>N</sub>1 miraa  
     yake))  
 28. SM<sub>N</sub>1j: Na uache wasiwasi wewe.  
 29. :Sawa baadaye baadaye mzae.  
  
 ((SM<sub>N</sub>1j anaondoka))

## **KIKUNDI KINI A**

1. MTF: Ningependa kujua vile mahusiano yenu huwa baina  
     ya wasomali na wameru[  
 2. SM001A: [Hata kama unaniuzia miti mbaya]. Hata kama  
     natoka huko Meru kwa kukula kioski na nimekuta mmekaa  
     chini nimeanza kukula miraa... na kama mimi  
     haijanibamba, lazima nimtusi huyo mtu....  
 3. JIBU LA WENGI:ee  
 4. MM001A: Kila matusi haikuwangi kwa ubaya. [Hiyo matusi  
 5. SM002A:[Si ubaya... hapo hakuna ubaya  
 6. MM001A: Mimi hukuanga side ya kutukana lakin  
     haikuwangi kwa ubaya  
     ((kicheko cha wote))  
 7. MM001A: Jamaa amekupatia pesa yake nyingi ukampatia  
     tuvitu au tumiti tundogo umfungie hata akikutukana  
     hakuna ubaya hapo.  
 8. SM001A: Eee hakuna ubaya hapo...  
 9. MM001A: Na tena haishiki. Mkiongea vizuri kama watu  
     wanauziana nini, haitashika hiyo miraa. matusi  
     isipokuwa .. hapo kazi hakuna.  
 10. SM002A: Pia yeye lazima mwenye ananunua atukanane  
 11. MTF: mbona?

12. SM002A: Anaona hiyo kutukanana si kitu..
13. MM001A: Kwanza uulize huyu ni customer yangu..  
lazima mtu atukanane kila saa
14. MFT: na mtu hachukulii kama...
15. JIBU LA WENGI: aaa hapana
16. SMM003A: Kesho pia niko hapo kwa hapo nakwambia  
kumamako jana ulinipatia miraa aina gani?  
(( wote wanacheka))
17. SM003A: Unasikia? Hapo hakuna kitu...
18. MM002A: Haikuwangi matusi ya roho mbaya. Saa  
ingine inakuwa for fun.
19. SM001A: haikuwi kwa roho mbaya ama nini...  
maanake ni kwa mdomo tu... ni kama anaenjoy
20. SM001A: Hapo ni kama unaenjoy tu sister!
21. MTF: Lakini ni kama ni sawa kweli?
22. MM001A: Hakuna mwenye huchukulia kama ni offence
23. SM002A: Cheki hakuna kufanya hivyo kwa mtu wowote
24. SM001A: Hakuna kitu unaweza ukafanya bila. Hakuna  
kuomba. Lakini yule mtu hajui anaweza fikiria mambo  
mbaya
25. JIBU LA WENGI: Ee ni kweli
26. MM001A: mtu anayesimama kando hawezি elewa kile  
mnafanya...
27. SM002A: Anaweza dhani hata watu hawa wanapigana  
ama nini! Watadhania hivyo
28. SM001A: Unasikia sisty? Hiyo ni biz yetu
29. MTF: Lakini lugha ya wanaume na wanawake  
hufanana, au ni tofauti na ya wanawake?
30. JIBU LA WENGI: ni same ! ni same!
31. MM003A: Kwanza wamama ndio wanatukanana zaidi
32. SM001A: Hao kwanza ndio wako na matusi  
hapa((akiashiria kwenye midomo))matusi yao!...
33. SM002A: "Ayee si utupatie miraa mbwa wewe!"  
wanasema hivyo

34. MTF: Je wanapokuja kununua, huja na kutanguliza kuongea kwa salamu kama mambo-poa n.k.?
35. SM002A: Hakuna kawaida hapo, customer akikuja kwangu aanze hiso story za mambo, habari za watoto, najua hana pesa.
36. MM002A: Hiyo ni ya kuza nguo ama vitu zingine, ama anakuja kukopa
37. SM001A: Huyo ni mtu hana shilingi, hana pesa
38. MM003A: Huyo ameamua hiyo siku kukopa
39. MM001A: Huyo mtu hana pesa. Mtu ako na pesa anakuja anagonga meza na kukwambia, Mbwa niuzie miraa, na siombi!
40. MTF: Na hiyo ndiyo kawaida yenu?
41. JIBU LA WENGI: Ee ni kawaida kabisaa
42. MTF: Lakini huo ni unyenyekevu kweli?
43. MM001A: Ee ni unyenyekevu ya ajabu
44. SM002A: Wamezoea. Ni tabia yao yaani.
45. SM001A: Pia sisi(wanunuzi) tunajua ni kawaida na tuko sawa
46. MM001A: Hakuna mtu huchukulia au husikia vibaya
47. SM003A: Mahali mtu huwa hatukanani mtu huwa haendi, mahali mtu ataenda kununua na kukaa tu na hatukanwi, miraa haitashika
48. MTF: Je kuna mpangilio kweli katika mazungumzo ya kuza miraa?
49. JIBU LA WENGI: eeee
50. MM004A: Kuna mpangilio kwa sababu akiuliza ni pesa ngapi nami nitamjibu. Lazima nimuulize unataka ngapi, anachukua miraa anakagua, akiipenda anakwambia kama ni ¼ ama ni ½ unamfungia
51. MM003A: Anataka giza ama kangeta ngapi kwanza,
52. SM001A: Maswali iko, unataka kiasi gani, miraa gani?
53. SM003A: Unataka shurba moja moja, mbili..

54. MM001A: Hata bei mnanegotiate..
55. SM001A: Hata bei ni kuamua..
56. MTF: Je mnaweza mkasemaje kuhusu uhusiano wa Wameru na Wasomali? Je ni miraa pekee inawaunganisha?
57. SM001A: Iko vitu mingi sana... kila kitu! Kila kitu!
58. MTF: Miraa ikijaondolewa siku moja, uhusiano wenu utaendelea ama utakatika?
59. JIBU LA WENGI: Aaaaa sioni..
60. MM001A: Itakuwa lakini itakuwa hostile
61. SM001A: Iko, uhusiano iko
62. MM003A: Wengine ni watu wazuri sana. Kuna urafiki sio miraa pekee...
63. MM004A: Ukisikia msomali akiongea, utasikia uhusiano yao na wameru unafaa usikie... ukiletea msomali pesa yao kwa miraa, nao wameru wanapeleka pesa yao kwa duka kununua manguo. Kwa hivyo hawawezi kukosana, kwa hivyo ni mandugu
64. SM003A: Lakini ikiwa the factor ni miraa inawaunganisha in one way or the other
65. MTF: Miraa ikijaondolewa?
66. SM002A: Inawafanya kwanza waunganike kuwa kitu kimoja na wakaanishe pamoja
67. MM001A: Bila miraa mimi sioni kutakuwa na uhusiano na msomali wowowte. Miraa ndio catalyst. Kwanza huku Eastleigh
68. SM001A: Kwanza ukienda huko Meru, huko town ya Meru, unawaona Wasomali wengi sana vile wanakaanga na kuishi
69. MM004A: Uhusiano wa mmeru na msomali huenda ukaendelea hata kama miraa haiko, lakini kitu kubwa ni juu ya miraa
70. MM001A: Urafiki ulianza juu ya miraa hata kama siku hizi imekuwa kawaida... ilianza juu ya miraa

71. MTF: Miraa ilianza kuuzwa na wameru na wasomali lini hivi?
72. MM002A: Tuseme 1950, 60 huko
73. MM001A: Kumaanisha hakukuwa na biashara ... imeevolve kama biashara zingine.. biashara imeanza kuwa recognised kitu 1970. Miraa ilianza kuuzwa Eastleigh peke yake na watu wachache. Lakini Wasomali wanunua siku hizi hadi kwa mashamba. Anakodisha shamba, ananunua miraa na kutafuta watu wa kuchuna hadi iende sokoni. Lakini kwa hii yote, lazima akuwe na wingman mmeru.
74. SM001A: Lazima, lazima awe na mmeru wa kumsaidia.
75. MM001A: Lakini msomali ndiye ako na pesa yako ya miraa kwa mfuko na ... zamani ilikuwa mpaka Mmeru awape hadi miraa ya kupeleka Mogadishu...
76. SM002A: Kila mtu aka na mtu wake. Kama ni msomali, aka na mmeru wake.
77. SM003A: Lakini biashara imechange sana, si kitambo sana, inflation imeaffect kila biashara. Hakukuwa na kuuza chini ya kilo. Nusu haikuwa inauzwa, ulikuwa unanunua kilo kama shilingi 500, 600 lakini sahii ni maelfu. Giza ilikuwa inauzwa 600 kilo. Na kila mtu angeafford
78. SM002A: Siku hizi ni shurba. Kuna time hata hatukuwa tunajua mambo ya shurba na quartre. Kilo tu ndio ilikuwa inauzwa. Hata nusu ilikuja hivi karibuni. Ilikuwa inauzwa makilo tu
79. MM001A: Unawauzia kilo wanaenda kukatana huko mbele. Lakini siku hizi hata shurba moja unauba, ama mbili
80. MTF: Mbona watu wengine hurusha pesa? Je, huo ni upole kweli?
81. MM001A: Yaani kurusha haikuwangi rudeness. Kwa miraa hiyo si rudeness

82. SM002A: Wanakuanga wamezoeana. Ni kuzoeana.  
Haikuwangi rude. Kama ni mara ya kwanza yake kununua  
kwako, atakupea kwa mkono na kwa heshima.
83. SM005A: hakuna hiyo
84. MM001A: Lakini kama mmezoeana na customer wako  
wa kila wiki ambaye hata akiwa mbali anakupigia  
anakwambia umwekee miraa basi hata kurusha pesa si  
mbaya
85. MTF: Nikagundua kuwa wameru wamejifunza maneno  
ya lugha ya kisomali, na wasomali wakajifundisha  
maneno ya kisomali
86. SM002A: Ee ni ukweli. Kwa mfano nikiuja dukani  
niambie xx "leta maanka poa wewe." Na ni mmeru,  
ataelewa kwa sababu anajua maanka ni miraa tamu
87. MTF: Mbona watu wa tribe moja hubadilisha lugha  
na kutumia lugha yao ya kwanza wanapokuwa wakinunua?  
Ni ili wale wengine wasisikie?
88. SM002A: ee ni ukweli. Ni ukweli
89. MM001A: Saa ingine ni kwa sababu kuna customer  
hajui Kiswahili au Kiingereza sasa itabidi ujifunze  
majina mbili tatu za kisomali kwa sababu ako na pesa  
yake alipie kitu anataka aende
90. MTF: Lakini mbona wengine nilisikia wakiitana  
nywele ngumu wakirejelea wameru? Huo si ukabila?
91. JIBU LA WENGI: aaaaaa hapana haikuwangi kwa ubaya
92. :Aaaa hiyo ni utani tu... hapana
93. MM002A: Hiyo si matusi, ni kama kuita mtu mkono  
mmoja—mkono mmoja juu ako na mkono mmoja. Hiyo ni  
culture yao. si kwa ubaya na sio matusi. Inakuwanga  
brutal honesty.
94. MTF: Mbona wanawake wakikuja kununua wankuja na  
mlango wa nyuma badala ya mlango wa mbele?
95. SM002A: Wengine hawataki kununua pamoja na watoto  
wao, wengine hawataki kuonekana na brother,

- sister, baba au watu wa familia yake. Wengine hawataki kuonekena na watu wao juu ya legacy
96. MTF: Si kwamba mwanamke hapaswi kununua?
97. JIBU LA WENGI: Aaa hapana. Huwa inategemea na duka gani
98. SM002A: Yaani ni nafsi yake, wanaona wasionekane na uncle, cousin, watoto au watu watamchukulia vibaya. Lakini kuna wengine hawaogopi mtu wowote na anachukua kama wanaume wengine
99. MM001A: Wanunua kwa duka ambayo hawajulikani na wanunua kutoka mbele ama aulize kama kuna mahali fulani hapo auziwe...atumane
100. SM004A: Kama anaona ni aibu kuonekana, atakwambia kwa kinjaro umsundie(umfichie)
101. MTF: Si mambo na dini au gender?
102. MM001A: Si mambo na gender au dini, kuna wanaume wengine hujificha pia
103. SM002A: Wanaume wengi wanakulanga kama wamejificha, ama anasimama kwa gate na anajua utajua anataka nini
104. MTF: Nilidhani huenda wanawake wa Kisomali hawapaswi kuchew?
105. SM002A: Wameru hata ndio hawachew. Wasomali huchew kwanza sana
106. MM001A: Hakuna mtu huwakataza wa kimeru kutafuna, lakini hawatafunangi
107. MTF: Sijaona wanaume wa Kisomali wakiuza miraa kwa wingi.
108. SM002A: Huwa wanauza Alele lakini si wengi. Hata ukienda Somali 95% ni wanawake ndio wanauza. Wanawake ndio huuza sana. Utawapata wanawake wengi kuliko wanaume. Business ya miraa haiwezi kutembezwa na wanaume. Wanawake ndio huweza kuuza sana. Nimeenda hata Somali pale miraa inatumwa na inauzwa. Wamama ndo

wanaauza huwezi ukapata wanaume kwa sababu wanaume watatafunu yote na hawatauza hata! Wamama wako na discipline.

109. MM001A: Hakuna mtu huwaambia wasiuze, wanaume,
110. MTF: Wanawake wakija kununua na kuza huwa wamerelax tu ikilinganishwa na wanaume
111. MM003A: Mostly wanawake wa Alele hawakujangi kununua first time, kuna mama anapiga simu anawekewa anakuja kuchukua tu. Hakuna kuongea. Si kama wanaume. Halafu bei ni fixed si kama hii ya kuja kuongea(kunegotiate) kama ni 1000 ni 1000. Yaani ingine unaweza kunegotiate. Ni tofauti.
112. MTF: lakini wanaume nimeona wanaauza mingi na wanauzia ndani ya nyumba na wanawake wanauzia nje. Kuna tofauti?
113. MM001A: Ni kama kuza nguo ya karatasi na ya mtumba kwa open market. Quality si moja. Inamaanisha kama unaafford kulipa space ya kuuzia wewe uko na kitu ya maana.
114. SM002A: Yaani duka na yule wa nje, wa nje anatafuta watu wa kugonga na miraa mbaya.
115. MTF: Lakini bado wako na customer wao bado? Wameru hununua kwa wanawake wa kisomali?
116. MM003A: Wameru hutafuna miraa si quality, hawezni akaenda kununua miraa quality. Ananunua veve ya mia tano. Lakini hanunui mbaya
117. SM002A: Wasomali wa Alele hununuliwa na watu hawakuji kila siku, huwa wanalipa hata per month. Yaani wanawake wanakupatia deni unamlipe hata mwisho wa mwezi.
118. SM005A: Kwa duka mara nyingi lazima ulipe cash, hata ikiwa ni deni itafika mahali isimame baada ya siku kama mbili. Mwanamke huwezi ukacheza na kazi yake kwa hivyo lazima ulipe deni yake

119. SM002A: Wasichana wa Meru hawajawahi kuwa washiriki wa miraa, maybe wapike chai ya kutafunia. Hakuna mtu ashawahi kuelewa ni kwa nini ...wao hupika tu chai ili wapate pesa. Tena hii biashara haitaki uchukulie kila kitu mtu anasema ni ukweli. Juu wanawake huwa wanasumbuliwa na opinion za mdomo na ukae juu jamaa atakuja akutukane akutukane na ukose kukasirika. Wanawake hukasirika ovyo so hawawezani na kuuza miraa kama wanaume
120. MM001A: kwa duka mara nyangi unaafaa ulipe cash, hata ikiwa ni deni itafika mahali isimame baada ya siku kama mbili. Lakini mwanamume huwezi ukacheza na biashara yake.
- 121.
- SM002A: Lugha yao ni tofauti sana na yetu. Hiyo yao haina lugha ya kutukanana. Atauza ni kama anakukatiana ni kama anamgeuzia Kiswahili. Ni ukweli yake kuwa anakuangalia na zile macho na uchukue miraa mbaya na pesa mob. Mwanamume kwa upande mwengine, unamwangalia mpaka akupee kitu unataka na kwa pesa unataka.
122. SM004A: Dame kabla auze miraa, watauza lakini watu watachoka na hiyo miraa haraka. Siwezi ambia dame vile naweza nikaambia mwanamume
123. MM001A: Plus siwezi kumwambia miraa yake ni mbaya na vile ananiangalia na macho zinakaa sijui aje sexy(( kicheko kutoka kwa wengi.))
124. Jibu la wengi: eeee inakuwanga hivyo ((kicheko tena cha wengi))
125. MM005A: Ni hivyo tu watu wanaongea. Ni hivyo tu...

((Mjadala ulikamilika baada ya saa moja. Mtafiti aliwashukuru wanakikundi kwa mchango wao katika kuufankisha utafiti wake.))

## KIKUNDI KINI B

1. MTF: Je, mnawenza mka sema nini kuhusu uhusiano wa wameru na wasomali katika biashara ya miraa?  
Je uhusiano wenu ni wa ndugu-ndugu au ni biashara ya miraa inawaunganisha?  
Hilo ndilo swal la kwanza ambalo ningependa tulijadili leo
1. MM001B: Ebu rudia swal tena
2. MM003B: Tunaweza tukasema hiyo biashara ndio factor kubwa ile imewashikanisha. Lakini si yote kwa sababu kuna biashara nyine ndogondogo zile zinawaunganisha kama vile za nyumba, za manguo, za usafiri pia zimewaunganisha. Lakini miraa ndio ile main
3. MTF: Na miraa ikijaondolewa, tunaweza tukasema kuwa mipaka ya wameru na wasomali ni hii.. kiutangamano?
4. MM001B: No uhusiano wetu na wasomali umeanzia kwa miraa. miraa ndio pioneer. miraa imekuwa msingi wa uhusiano wetu. Haya mambo mengine yamekuja yamepata uhusiano ambao umejengwa na miraa. kwa hivyo hata miraa ikijaondolewa leo, uhusiano unaweza ukaendelea lakini utakuwa umedidimia.
5. SM001B: Lakini hauwezi ukadidimia kabisa juu kuna wale hata wameoana. Kuna wasom wengi sana wenye wameoana.
6. JIBU LA WENGI: eee kuna wengi sana ambao ni wasomali wameolewa na wameru
7. MM002B: Kwanza wengi wameoana wale wanakaa maua. Wengi sana.
8. JIBU LA WENGI: hata sisi tunapanga kuona wasomali bado.. ((kicheko))

9. SM001B: Eee inakuanga hivyo
10. MTF: Kwa hivyo uhusiano wa Wameru na Wasomali si ule tunaweza kusema ni wakulazimisha bali huwa automatic
11. MM004B:Eeh huwa ni automatic kwa sababu kama ungekuwa wa kulazimisha haungekuwa umekaa huo muda wote
12. MTF: Je mnaweza mkasema nini kuhusu lugha katika biashara ya miraa? Kwa mfano mimi nimegundua kuwa saa nane saa tisa hivi eastleigh huwa iko standstill. Watu wote wanaenda Pumwani kungoja miraa na kuna heka heka nyangi tu.
13. MM004B: Generally miraa kutoka kwa shamba huwa ni vigorous. Wale wa kutransport nao wana wanakuanga hivyo hivyo na masaa yao, wa kungoja pia wako na masaa yao , wa kupeleka mtu wa kukula hivyo hivyo.. hadi miraa itemwe.
14. MM001B:Ee mpaka ifike mahali pake yaani
15. MM002B: miraa haina polepole, miraa inachunwa haraka, ipolekwe kwa magari haraka, magari ikuje haraka, itolewe kwa magari haraka na inunuliwe kwa haraka
16. MM004B: Generally miraa iko na hiyo tabia ya kukua vigorous sana
17. MTF: Je, tunaweza tukasema kuwa hiyo biashara vile inafanywa chapchap ndio inasababisha robust language use?
18. SM002B: Unajua hiyo ni kama kawaida kwa sababu ni kama na ikitoka hukomiraa inahitaji haraka. Kutoka kwa shamba, juu inaharakishwa kwa shamba, pia utakuwa unaharakishwa kuchuna, ukitoka huko, pia inapelekwa kwa gari mbio, nayo gari inaondoka mbio inaleta hapa,nao customer ambao wanaletewa,wataacha kazi zingine ili wakuje hapa haraka na hawataki kuwastiwa

- time ili watoke mahali hapo. Haraka haraka iko kila mahali. Kwa hivyo generally ni kazi ya haraka haraka.
19. MTF: Hii haraka haraka inaletwa na nini?
20. MM003B: miraa ni kitu inaharibika haraka. Miraa, Quality ya miraa inaendana na time zake. The more miraa iko fresh, the more iko na quality mzuri.
21. SM002B: ee the more iko fresh. Ndio maana unaona, usipoipeleka haraka hata ifike jioni na iwe haijahiribika, haitakuwa na the best quality kama ile ilifika mapema. Miraa vile imetolewa tu kwa shamba na vile itapelekwa hadi ifike mahali itakuwa inapelekwa haraka ndio itakuwa na quality the best.
22. MM003B:Miraa ikilala inachange hata taste.
23. SM002B:Ee inachange taste kabisa. Hata ikifika late,huwa imechange taste.
24. SM001B:Na kuna mwenye pia anatakanga ikiingia tu mapema, achukue haraka,aanze haraka, ndio amalizane nayo haraka ndio aende kulala mapema. Juu wengine kesho yake wako job na kitu kama hiyo.
25. SM002B:Ee juu kuna wengine wako na kazi za serikali hivi, kuna mahali wengine wanafanya kwa maorganisation hivi..
26. SM003B:Kuna pia ujeuri mwangi sana wa watu katika miraa
27. MM003B: ee kweli naturally kwa miraa kuna kaviolence unique
28. SM003B:Lakini mara nyngi huwa inadepend na customer
29. MM003B: Miraa ni unique kwa commodities zingine. Ukiuza vitu zingine unabembeleza customer, unafanya etc lakini kwa miraa, mwenye anauza na mwenye ananunua wote hawabembelezanangi...
30. MM002B:Wote wanatukanana..

31. SM001B:ee ujeuri wa miraa unaanza kwa roots, ukikuja hata kwa shamba, wakati mtu anachuna, utasikia mtu ameenda polepole unaskia amepewa tusi kubwa, wewe nini na nini wewe harakisha..juu hata kwa gari bado matusi iko.. wewe nini nini panga miraa haraka..
32. SM002B: Ee lazima umtusi ili afanye haraka.. ni kama unamharass hivi, hakuna mambo ya polepole...
33. MM003B:Ee miraa ikiwekwa kwa gari lazima ujeuri uko.
34. MM001B:Hata wakati wa kutoa kwa gari.. ujeuri uko.
35. SM001B: Na hata customer mwenyewe akiuziwa anatusiwa bado, na ye ye pia atusiana kwanza anakuja anabang meza..
36. SM003B:Lakini mara nyingi huwa inadepend na customer. Unajua customer mpya hauwezi ukaanza tu kumtukana. Hapana. Mpaka muwe mmezoeana. Lakini mtu mmezoeana naye, unaweza ukamtukana.
37. SM001B: lakini eeh inadepend na customer. Customer mpya atakuja tu auziwe poa, hivyo hivyo.. lakini kama mimi xx anaweza akanitukana na mimi pia nimtusi....(kicheko)
38. MM002B:Lakini mtu sijui siwezi nikamtusi...
39. SM002B:Lakini sikiza, kila mtu anaconsumingi miraa huwa anajua nikienda kila mahali lazima nitusiwe hata nikiwa mgenia au si mgeni
40. MM003B: Lakini kuna wale ambao hawatusiwi
41. MTF: Lakini tunaweza tukasema kuwa lugha ya wanaume na wanawake inafanana au inatofautiana kwa kiwango chochote kile?
42. SM002B: Ee tunaweza tukasema tofauti tu ni kidogo. Unajua wanawake hawasimamangi hapo kwa mlango
43. MM001B:ujeuri ikifika kwa upande wa wanawake inapungua kwa maana hata wao wenyewe wakati wanakuja

- kununua miraa, hawakuji na ujeuri ule, kwa maana biashara yenyewe imechukuliwa kama ni ya wanaume na hata wanunuzi wengi ni wanaume
44. MTF: Basi mbona wanawake wanakuja kununua wakitumia mlango upande wa nyuma?
45. SM003B: Wengine huwa hawataki kuonekana..
46. JIBU LA WENGI: Ee ((kicheko)) wengi huwa hawatangi kuonekana.
47. MTF: Kwani kuonekana kuna nini?
48. SM003: aa unajua shida yao, mara ingine unaweza ukapata wanaume ndio wamejaa kwa dirisha na mwanamke huenda ni mmoja au wawili. Sasa yeye ni kama hataki kusimama na hao wanaume au wanaume wale wako nje wanapelekwa sana sasa yeye anataka kuingia ndani ili aongee na muuzaji polepole au kwa utaratibu.
49. SM001B: Inaweza kuwa vevye yeye ameingia ndani, kuna mtu wowote hata wasomali wengine, kuna wenye hawatakangi wajulikane kama wanakula miraa. Sasa akikam anaweza akaingia ndani au na mlango wa nyuma au akuonyeshe ile anataka. Au pia asimame mbali huko kwa gate aambie mtu leo anasikia kukata na anatumaa mtu amchukulie kwa sababu hataki wasomali wengine wajue. Inakuwanga hivyo yaani hawataki waonekane ka anakula miraa. Wengine pia hupiga simu ili waletewe miraa hadi kwa nyumba. Bora tu wasijulikane wanatafuna. Lakini kuna wale pia wanakam direct tu kama wanaume na hata hawaogopi mtu wowote tu kama wanaume na wanasema lete miraa! Kama wanaume tu!
50. MM003B: Lakini hiyo inalingana sana na tribe za kisomali. Kuna wale wanajua kuwa tribe zao ziko hapo na anaogopa aonekane nao, na wale hawatakangi kuonekana na watu wao. Lakini kuna yule, anajua kuwa hakuna mtu anamjua hapo kwa hivyo atakuja anunue tu, na kuna either wale hupewa za kujisaidia na miraa ni

kitu ya starehe na akionekana ukinunua hatawahi kupewa tena kwa hivyo lazima aingie ndani ili anunue au aingie na mlango wa nyuma.

51. SM001B: Lakini kuna wale wanunua na pesa yao so haogopangi mtu wowote
52. MM003B: Eeh wale wako independent hawaogopangi mtu
53. SM001B: Na bado inaweza kuwa ni vile tu ako na heshima yake na hataki aonekane, yeye binafsi yake kwa sababu yeye ni mwanamke lakini hataki aonekane akinunua miraa
54. MTF: Si dini, power au religion inafanya wafanye hivyo?
55. SM002B: Sisi dini yetu ya kiislamu vile inasema ni mwanamke na mwanamme si equal. Hatuko sawa. Hatutoshani. Mwanamke ni 50 na mwanamume ni 100. Yaani hata tuseme wakoseane mwanamke akujiwe, watu wa hiyo familia yake watalipwa si same, kama ni dame watapewa 50, na kama ni chali 100.
56. MTF: Sasa tunaweza kusema kuwa ni dini inaleta tofauti hiyo?
57. SM001B: Ee dini ya kiislamu ni hivyo, mwanaume ni first level. Na mwanamke anakuja nyuma.
58. MM002B: Lakini pia wanaume hawatambuangi macustomer wanawake sana. Kwa upande wa kununua ni mwanamume ako na buying power kuliko mwanamke.
59. MM001B: Pia mwanamume akiamua kununua atakuja hata kesho, lakini mwanamke atakuja mara moja kwa wiki au hata asikuje.
60. SM001B: Na hata akiolewa na chali saa ingine anaambiwa aachane na miraa na anawacha miraa.
61. Jibu la wengi: ee Inakuwanga hivyo saa
62. MM004B: Sasa utapata kuwa, macustomer wanaume ndio wanatambuliwa sana

63. MTF: Wanaume wanatumbuliwa kwa sababu ya consistency?
64. MM003B: Ee either kwa kuuza na kununua sasa
65. MTF: Lakini niligundua kuwa wanawake wengi wa Kisomali ndio wanaiza miraa na sio wanaume?
66. MM003B:Ee wasomali.. lakini wasomali wengi hawanunui kwa wanawake!
67. MTF: Mbona?
68. SM001B:Upande ya business ya wasomali, yaani upande wa miraa,wanawake ndio wako top. Vile wanawake wanatembeza siku hizi vyenye iko, vile wanawake wanatembeza hiyo miraa, mwanaume hawezi temebeza. Vile ile doh ataingiza chali hawezi ingiza hivyo.
69. MM001B:Chali atakula
70. SM001B:Ee chali atakula veve..
71. MM003B:Ee lakini kwa msomali na mmeru, msomali atachagua mmeru kwa sababu ya ile notion ya mmeru ndiye anajua miraa poa
72. SM01B:Lakini msomali hatatoboa kwa
73. MM001B: Lakini hata mwanamke aweke miraa hapo nje, wale wengi wasomali watachagua kuuziwa na mmeru. Wengi..si kusema ni wote lakini
74. SM003B: Hata wenyе wanatuma miraa Somalia wengi ni wanawake ndio wako na hiyo job
75. MM001B: Ee wengi
76. SM001B: Ee kwanza siku hizi,
77. MTF: Kwa upande wa Wameru nao niligundua kuwa wanaume ndio wanaiza miraa kwa wingi.
78. MM003B:Ee 99%
79. MTF: ee 99% ni wanaume.Na kwa wanawake ni mmoja mmoja..
80. SM002B: Na kwa upande wa wasomali 90% ni wanawake

81. MM001B: Sababu kubwa ya wasomali ni kuwa wanaume watakula ile miraa. Watakula hadi ile wanauza na hata faida.
82. ((Kicheko cha wengi))
83. SM001B: ee yaani business ya miraa hawataweza kumaintain
84. MM003B:Ee hawawezi kumaintain sababu utatuma kilo tano, watakula tatu ((kicheko))
85. SM001B: Ee lakini si biashara zote, ni ya miraa tu watashindwa kumaintain. Kwa sababu yeye upande wa miraa ni ule upande yake yeye anaenjoy. Kwa hivyo atakuwa ameipangia kwa ukubwa
86. FM001B: Lakini pia kwa upande wa wameru kuna wanawake huchuna miraa huko meru
87. MTF: kuna wenye huchuna ee.. lakini kwa kuza huku eastleigh sijaona wengi..
88. FM002B: Kuna wale huwa kwa soko, lakini si wengi bado..
89. MTF: Sababu ya wanawake wameru kuwa wachache yaweza kuwa ni ipi? Je, ni kwamba mwanamke hapaswi?au nini?
90. MM004B: Ee imechukuliwa tangu kitambo kuwa biashara ya miraa ni ya wanaume. Kwa maana tuseme kutoka zamani wakati biashara ya miraa ilianza, wanawake wa Kimeru hawakuwa wameingia Nairobi. Hakuna wale walikuwa wanafanya hiyo biashara, hiyo biashara ilikuwa ya wanaume. Na ungeonekena ukifanya biashara kama hiyo ukiwa mwanamke, ungeonekana ukiwa mtu si wa kawaida.
91. MM003B:Ee wako, lakini si wengi
92. MTF: Je, katika biashara kuna unyenyekevu kweli...
93. MM001B: Hakuna! hapo nayo si ni kama unakuja kununua miraa na unataka deni?

94. MTF: Kwa hivyo ukiona mtu akija aanze kusema sasa-poa, habari ya kwako n.K. Haipo?
95. SM001B: Ee iko, kuna wale wanakuja hivyo kwa upole wanakusalimia poa, wanakupigia story na bado atabuy miraa, iko ee iko
96. SM003B: Lakini unajua bado italingana na vile mtu ameingia...
97. MM001B: Lakini wale wanakujanga hivyo ni wale hawana pesa ya kutosha na wanataka deni au ni wageni katika biashara hiyo...
98. SM003B:Kuna wale wanakuja kwa upole na wengine wanakuja wakiwa rude...Mtu mwenye ameingia rude..
99. SM001B: lakini iko kama 10% wenye wanaingia na upole na wanakuuliza habari yako, oo habari ya watoi na kukugotea, iko..
100. MM002B: Lakini wale wanakuja hivyo, wengi wao ni wenye wanataka kukopa. Wakikuja na upole wao ujue wanakuja kukukopa
101. MM003B: Ama hawana pesa inatosha..huwanga ni hivyo..
102. MTF: mnaweza mkasemaje kuhusu interruption, yaani kukatana kauli katika mazungumzo?
103. MM001B: Ee hiyo iko. Unajua unaweza sema hivyo, kwa maana unaweza kuja ile peek hours. Sasa wewe umekuja kupeana story nydingi badala ya kusema ile miraa unataka upewe. Na sasa ukianza kupeana story nydingi utasikia ukiambiwa "ni nini unataka, sema ile unataka ama uende." Kwa sababu umekuja wakati ambayo biashara imeshika sana, na kuna wengine wako hapo(customers) wanangoja kuuziwa na wewe uko hapo na story zako nydingi. Lazima utakatizwa katikati.
104. MTF: Je, mbona kuna matusi mengi katika mazungumzo?
105. MM003B: Matusi zingine ni za kukusifu.((kicheko))

106. MM001B: mimi naweza sema, kulingana na lugha zote mbili- wasomali na wameru huwa kuna matusi. Kwa wameru enyewe unajua matusi ni kama kitu ya kawaida, na kwa wasomali pia matusi ni kama kitu cha kawaida. Sasa kwa ile biashara, inakuwa ni kama ni ya watu ambao wako na vitu zinarelate, kwa sababu wote wamezoea kutusiana. Kwa hivyo, hata matusi ikitolewa, hakuna mwenye anaona matusi ikiwa kitu kubwa.
107. MTF: Na matusi hazuii biashara kuendelea kwa sababu wamedhuriwa kihisia?
108. JIBU LA WENGI: Aii hapana..hakuna kitu kama hiyo
109. MM002B:Noo matusi haiwezi kuzuia biashara kuendelea..
110. MTF: Hatasema kwamba umenitusi sitakuja kununua kwako tena?
111. Jibu la wengi: aaa hapana.
112. SM002B: Hakuna kitu kama hiyo
113. SM003B: hapana.Kwanza ukimtukana ndio atakuja tena hata kesho yake. Hata ukitupa pesa yake huko kwa barabara, ataenda achukue ile pesa na aongezee nyingine hadi itoshe yenyе unataka.hawezi jali, na hataenda kwa mwingine mwenye anaiza miraa, atanunua hapoa hapo kwako tu.
114. MTF: Je wauzaji hudumishaje wateja? Yaani anafanyaje ili mtu anunue kwake kila siku?
115. MM003B: Hiyo mimi naonanga, the main issue ya kumaintain customers wako ni ile quality ya miraa yenyе utampatia. Kwa biashara ya miraa, ile imani ndio inafanyanga mtu akuwe customer wa mtu kabisa. Saa ingine ukimuuzia miraa mzuri, hata siku utaanza kumpatia miraa mbaya, imani tu itakuwa ya miraa yako tu ni mzuri
116. MM002B: Naturally, biashara ya miraa inakuanga na kitu inaitwa loyalty. Hiyo ni trait ile kubwa sana

- katika biashara ya miraa. mtu anajua miraa ya fulani na fulani ni mzuri, na hivyo na ni hivyo, na kama si hiyo hakuna. Sasa hiyo ndio imekuwanga kwa miraa sana.
117. SM001B: kuna yule anakuja kununua na juu amezoea kununua hapo na anajua miraa ni poa, hata aangalii..anachukua tu anaenda
118. MM003B: Lakini kuna pale ataenda kununua, na juu hajazoea ataangalia zaidi na hata bado akiitafuna haimbambi na ni juu si ya yule amezoea kula kwake.
119. SM003B: Lakini akienda kwa xx na anajua huwa anampatia kitu poa, haangalii hata, atafunga tu akienda
120. MM003B: Lazima mketi na customer wako,mkae na yeye ndio ucreate hiyo loyalty
121. MM001B: Lazima ujenge jina. Jina inauza, ndio mtu akisikia miraa imetoka kwako, anajua kuwa ni kitu mzuri bila hata kuonja. Customer akisikia tu miraa ni ya duka fulani ataamini ni mzuri hata kama ni mbaya
122. SM002B: Unajua kama huwa anachukua miraa kwa duka yako, hata iuzwe pesa ngapi lazima achukue. Unaweza ukasikia inauzwa kwingine 1000 na ni the same quality of miraa, na yule wake anaiza 2000, bado ataenda kwa wake wa 2000 juu amezoea kununua huko, juu anaamini miraa yake ni poa
123. MTF: Niligundua kuwa kama ni dukani, na kuna wauzaji wawili( msomali na mmeru) msomali hupendelea kuuziwa na msomali, je ni kweli?
124. JIBU LA WENGI: aaai hakuna
125. SM003B: Sio wengi. Na sio lazima
126. MM001B: hata pale unapata msomali anauza,saa ingine si eti ni juu ni msomali mwenzake,wengine ni juu ya lugha ni kwa sababu wengine hawaongei kiswahili ama kizungu so wanaamua wauziwe na msomali ili waongee kisomali

127. SM002B: Ee wengi wao wanajua kisomali pekee wengi wao. Hawaelewi lugha zingine. Kuna wale wametoka Somalia, wameingia Kenya kama hawajakaakaa Kenya wajue Kiswahili, na wanajua kisomali pekee na ndio lugha wanaweza wakaongea na kuelewa, hapo ndio utapata msomali mwenzako kwa duka uamue ndiye anakuuzia
128. MM001B: Maana msomali mwenyewe anaamini kuwa ni mmeru tu ndiye anajua miraa mizuri ya kumuuzia kuliko msomali
129. SM001B: Na si eti na madame pekee huwa wanajifichanga, kuna hata machali wanakulanga miraa, wengi tu. Najua hata xx anawajua, huwa hawatakangi kuonekana wakinunua kwa sababu hawajulikani kwao kuwa wanatafuna miraa. Kwa hivyo nikitaka kununua miraa nitaita mtu kama xxx nimwambie niaje kamanimesimama mbali kama huko DAY TO DAY huko, nimwambie niaje ebu nikamishie huko leo nakata, ananikamishia juu sitaki kusimama kwa shop ili nionekane. Juu wengi pia huwa hapo
130. SM002B: mavijana tu rika yangu wanakuwa wanajificha, juu hawataki kuonekana. Wanakuwanga hivyo
131. MM002B: Lakini hii story ya pikipiki ama cab imeleta vitu za kama customer hakuji dukani. Anakaa nyumbani, anapiga tu simu na miraa unaletewa miraa yako.
132. MTF: kwa hivyo customer wengine hawafiki dukani?
133. MM002B: Ee wengi hawakuji kwa hivyo ni rahisi sana kuwaretain customer kama hao.
134. SM003B: Lakini kitu tunasema ni kuwa kwa biashara zote, hakuna ingine iko na imani kama biashara ya miraa. Kwa maana mlaji wa miraa anaweza

kuwa ndio anataka kuanza au hata anatoka mahali pengine anapata kuwa mimi hununua mahali fulani. Mimi nitamweleza mahali mimi hununua miraa na ataamini hiyo miraa ni mizuri, nimpee namba ya simu na apige simu aitishe miraa na hajawahi fika kwa hiyo duka, na ataamini ni miraa nzuri kabisa

135. SM002B: Na utamwambia pesa unatoanga unamwambia mimi hutoa pesa fulani, na hiyo ndio atatoa pia yeye.

136. MTF: Tunaweza tukasema nini kuhusu future ya miraa?

137. MM003B: Technology imeanza kuchange biashara ya miraa, sio kama zamani. Sahii si lazima customer afike kwa duka, sahii hata pesa inalipwa kwa Mpesa, na wengine wako na till number, wengine wanaitisha mpaka picha kwa whatsapp anaangalia, saa ingine anakwambia nitumie picha ya miraa ile iko nione quality yake nikiwa hapa, si lazima akuje kwa duka. Kwa hivyo, future ya miraa inaonekana kuwa technology pia itaffect sio kama ile ya zamani mtu alikuwa anakuja anashika, anakurushia. Anaamini kuwa miraa yako ni mzuri tu hata kama ameona picha pekee kwa simu. So si kama zamani

138. MTF: Imani ni muhimu sana ee? Hivi kwamba..

139. MM002B: Loyalty sana, sio ile fake. Hivi kwamba ikiwa utamkosea, na mwingine amfurahishe anahamia huko tu hivyo

140. MTF: Uhusiano wa Wameru na wasomali ni upi? Kuna mipaka kwa njinsi wanavyotangamana?

141. MM001B: In terms of market na loyalty, tukisema tu ukweli, wasomali ndio the main market. Watu wengi wanunua miraa kabisa ni wasomali. Hata London, Kenya au mahali miraa yote tu huendanga wengi

ni Wasomali, hata hapa Eastleigh.Kwa Mmeru, msomali ndio namba one, lakini kuna kabilia zingine lakini hakuna wengine wanaaminiana kama wasomali na wameru. Sana sana, juu mmeru hawezi akampa mtu wa kabilia zingine deni lakini msomali atapewa deni, na yeze atalipa.Msomali anaweza akaenda shambani Meru ananunua miraa kwa shamba, anasema nitaleta pesa nikipeleka miraa na anakubaliwa. Na analeta. Lakini kabilia zingine hawezi enda na afanye hivyo....

142. FS001B: Na analeta akisema ataleta.
143. SM001B:Hawezi enda huko na achukue kwa shamba, aa hapana hata apewe au akubaliwe..
144. MM002B: So kuna hiyo chemistry imekuwa kwa miaka mingi kati ya mmeru na msomali.
145. MM001B:Unajua zamani kulikuwa na hiyo boarder sasa ulikuwa unaulizia. Boarder ilikuwa kuwa Wasomali hawaendi meru kutafuta miraa, hiyo ndio ilikuwa boarder, kuwa ni sisi wameru tuwaletee miraa na nyinyi mtununulie, lakini wakafanya wameru wakawa na imani nao, mpaka wasomali wameruhusiwa hata wanaenda kununua kwa mashamba sasa
146. MM003B: Hata London ulikuwa unatumia mtu haujui miraa,na inaenda tu na anakulipa na hakujui na hajai kukuona na wewe hujawahi kumwona. Mnafanya biashara yenu nyinyi wawili, Msomali na Mmeru na hamjawahi kuonana na biashara inaendelea tu kama kawaida. Ni ngumu sana kwa hizi kabilia zingine. Ni ngumu.
147. SM001B: wewe tu unasianga tu jina yake.  
Mpaka amiss tu one day mpaka akuje
148. MTF:Na wanawake je,wa Kisomali wakiuza lugha iko vipi ?
149. SM003B: wanawake wanatumia lugha ya kukatiana na lugha tamu.. ee tamu..inakuanga hivyo kwa

wanawake wa kisomali wakiuza. Lugha yao ni ya kufurahisha siyo lugha ya kutusiana hata. Juu ni dame unajua hata ukiona ikiwa si sawa hauwezi ukamtusi, juu ni dame. Utaona ni aibu

150. MM003B: iko difference kwa lugha kati ya mwanaume na mwanamke, juu at the end of the day, quality ya miraa ndio itaamua pale utanunua na urudi kesho na hata kesho kutwa. Nikienda nikule kwa mwanamke aniongeleshe vizuri na nikienda kwa mwanamume aniongeleshe vibaya, ile miraa nitasikia ikiwa mzuri ndio nitarudi tena

151. FM002B: Lakini si tulisema kuwa wanaume hata wakiongea mbaya si eti huwa wanamean vibaya..

152. MM003B: Ee.. lakini, kwa kununulia mwanamke au mwanamume, ile miraa tu mzuri ndio utarudi ununue. Wanawake wanaiza ndio, lakini hawanunuliwi sana, kwa sababu hatuwezi kusema kuwa wanaiza kuliko wanaume.

153. MM002B: Na biashara ya miraa sio kama zile zingine kama nguo utasema, wakati nilienda kununua nguo pale yule mwanabiashara pale alioniongelesha vizuri. Miraa ni quality. Hata urushiwe, utarudi pale pale tu!

154. MM003B: Watu husema kuwa miraa ya yule ni mzuri, miraa ya yule ni mzuri. Hiyo ndio lugha ya miraa. Miraa yake inakuwanga mzuri.

155. MTF: si ni nani aliuza?

156. JIBU LA WENGI : aaaa hakuna.. no no no

157. SM001B: No. Ni miraa. Ni quality

158. MTF: Na miraa ikijabaniwa, nani anaumia zaidi, ni mmeru, msomali au ni serikali?

159. JIBU LA WENGI: Ni wote. Ni wote

160. FS001B: Ni wote ndio wataumia

161. SM001B: Ni wote lakini sana sana ni Wameru juu ndio wengi wanategemea source of income.
162. MM002B: Wameru wataumia juu ndio wamepanda. Lakini kwa biashara pia kuna wasomali wataumia juu wanategemea pesa ya miraa sana
163. Kama ni biashara ya Somali hata wengi wataumia ni wasomali kwa sababu kama London 90% walikuwa ni wasomali. Kama somali 99% ni wasomali. So ikibaniwa, though haiwezi baniwa saa hii juu ni cash crop, hata ikijabaniwa nchi zingine. Losers bado wako, kwanza miraa inaingiza pesa nydingi sana nchini, kwa hivyo serikali pia itaumia,ile ya London ilikuwa inaingiza 3 million saa hii hakuna,so lazima nyinyi wote mlose
164. FS002B:Lakini sana sana Wameru. Si unaona duka zingine sasa wanauz a maji, na walikuwa wanauz miraa vile ilibaniwa huko
165. MM001B:Lakini kitu unapaswa kujua, miraa si miraa peke yake. Mtu anauza njugu,anafaidika juu ya miraa kununuliwa, mtu anauza sigara, mtu anauza maji, chai,soda mwenye ploty juu amerentisha duka,mtu wa kuza gunia, box za kupack miraa ya majuu, hata mtu wa ndege, weny gari, cess juu gari za miraa hulipa cess, mtu wa piki piki watu wengi wa kabilia zingine weny nyumba ambazo zimerentiwa na wameru na wasomali, siyo wameru na wasomali tu wataumia.. wote wanaumia indirectly through miraa
166. SM002B: Nilikuwa nataka kurudia kuhusu hii ya mwanamke akiuza miraa. Sasa hiyo, kuna vyenye pia wanauzanga, unaonanga wale macustomer wake weny huwa anauzia,wanajuana ni kabilia moja yeye hawez lipe daily ile pesa. Sasa huyu atahold ile pesa yake huku akilipia customer yake akimpea na deni,huyu akichukua dolar yake per month tuseme ni sister yake au mama

yake amemtumia kutoka majuu, ndio anakuja anampee doh yake tuseme ni kama 10,000 ama ni 20,000 yenye anamundai analeta hiyo yote per month. Hiyo month mzima huyo msichana ndiye atamlipia, atakaa na hiyo gharama yake. halafu alipwe pesa yake. wengi wao wanakuwanga hivyo.

167. MTF: Hii ni imani kubwa sana, kama vile mlisema.
168. JIBU LA WENGI: Ni ukweli.
169. Na utapata hiyo ndiyo analisha watoto wake nayo na anasurvive hivyo tu.
170. MTF: Na ukiulizwa kutaja majina ya unyenyekevu yanayotumika katika biashara ya miraa unaweza ukaorodhesha kama yapi?
171. JIBU LA WENGI: ((Kicheko)) aa labda matusi
172. FM002B: aa matusi ndiyo mengi.
173. JIBU LA WENGI: Hakunanga hata kusema asante. ((Kicheko))
174. FM001A: wengine husema tu sawa mkundu.. na wanaenda ((kicheko cha wote))
175. SMO03B: Ee wengine hata mtu akishamuuzia yeye hata anakutusi
176. SM001B: Hakuna hata pole au tafadhali
177. MM003B: biashara hii hainanga asante, pole au tafadhali. Tafadhali ya nini. Ni ulete.
178. SM002B: Wengine utapata hata amekuongezea hata shurba ya juu na unamwambia asante mkundu
179. MM001B: Hata kama hana pesa, anakuambianga tu sina pesa ingine na kwani utafanya nini?
180. FS002B: Ama aseme, jana uliniuzia miraa mbaya anakwambia we kwenda ukununue mahali ingine usinilet ee wewe
181. MM004B: Lakini jina ya heshima yenye iko kwa wingi labda mtu akuite baba pekee

182. MM002B:Ee. Ama hii pesa umeleta kama ndio  
utakuja nayo kesho basi usikuje
183. MTF: Huo ndio unyenyekevu e?
184. FM002B:Ama ukiletta swara, kama hakuna  
pesa, kesho hakuna miraa ingine
185. MM002B: ee. Ama kesho miraa itapanda.  
Usikuje kama hautaongeza pesa
186. MTF:Sasa hayo ndiyo maagano ya leo e?
187. MM002B:Ee hivyo tu na hakuna kusema  
asante.
- ((Mjadala ulikamilika baada ya dakika hamsini. Mtafiti  
aliwashukuru wanakikundi kwa mchango wao katika kuufankisha  
utafiti wake.))